

# VISA NA HADITHI.

---

STORIES AND TRANSLATIONS IN SWAHILI.

S.P.C.K.

# VISA NA HADITHI

(SWAHILI READER)

*MISCELLANEOUS STORIES AND TRANSLATIONS*

SOCIETY FOR PROMOTING CHRISTIAN KNOWLEDGE,  
LONDON: NORTHUMBERLAND AVENUE, W.C.

1899

mem

AQE0280

PL

8702

V47

1899

## VISA VILIVYOMO

						UKARASA
1.	BUDDHA	...	...	...	...	7
2.	WASINZIAJI	...	...	...	...	42
3.	KRISTOFER	...	...	...	...	47
4.	MAKARIO	...	...	...	...	48
5.	VITALI	...	...	...	...	49
6.	YOVINIANO	...	...	...	...	55
7.	GUIDO MTUMISHI	...	...	...	...	61
8.	MFALME NA MLAFI	...	...	...	...	65
9.	MTAWA NA MALAIKA	...	...	...	...	66
10.	FULJENTIO	...	...	...	...	69
11.	SEMIRAMISI	...	...	...	...	73
12.	SANAMU TATU	...	...	...	...	79
13.	EUSTASIO	...	...	...	...	80
14.	GUIDO SHUJAA	...	...	...	...	87
15.	VIBWETA	...	...	...	...	95
16.	MANENO MATATU	...	...	...	...	99
17.	KUNGURU	...	...	...	...	102

				UKARASA
18.	ISKANDER NA HARAMIA	...	...	104
19.	ISKANDER NA NYOKA	...	...	104
20.	MFALME MKARIMU	...	...	105
21.	RAFIKI	...	...	106
22.	NA TENA?	...	...	106
23.	JUMBE	...	...	107
24.	DAWA YA UGOMVI	...	...	108
25.	KUNGU	...	...	108
26.	SULTANI HAKKUM	...	...	109
27.	SULTANI ORUNGZEBI	...	...	110
28.	SULTANI MAHMOUD	...	...	110
29.	WATOTO NA MISALABA	...	...	111
30.	WATOTO NA MAUA	...	...	114
31.	MTOTO NA PAKA	...	...	116
32.	MTOTO NA MBAAZI	...	...	123

# VISA NA HADITHI

---

## 1. KISA CHA BUDDHA.

BUDDA (maana yake, Mwenyi nuru) ni nabii wa Asia. Hatta siku hizi pana watu wengi sana washikao mafundisho yake na dini yake, ndio watu wa Sina na Korea na Japan na pande zote za mashariki za Asia. Na zamani makabila ya Hindi pia wali-mwamini, baadae wakamwacha wakaifuata dini yao wenyewe. Bassi huyo Buddha nabii mkubwa sana.

Ni vigumu kupata hakika ya mambo yake na maisha yake, lakini twajua ya kwamba zamani pali-kuwako Hindi watu wenyi asili moja na watu wa Europa na maneno sawa, wakatengana na ndugu zao wakakaa Punjab penyi mto Indus. Baadae wagine wakaondoka, wakaenda njia ya mashariki wakaingia inchi sawa ya mto Ganjis wakatua humo karibu na milima Himalaya ; na watu hawa jina lao Wasakya. Wakalima mashamba wakachunga ng'ombe na kondoo wakakaa. Na mji wao mkuu ndio Kapilavastu kando la mto Kohana, karibu na Benares mji mtakatifu wa Hindi.

Na kisa cha Buddha tulichohadithiwa na watu wa kale ndio kama hivi.

## 1.

Siku za Wayahudi walipokirudia Yerusalem tokà Babel, wakajenga tena hekalu Yerusalem, wakasikia maneno ya manabii Haggai na Zekaria—siku zile paliondokea mfalme mmoja wa Wasakya, jina lake Suddhodana, akaoa mke, jina lake Maya, asipate mtoto lakini. Hatta mwanamke yule akalala usiku akaota ndoto, na ndoto yake, nyota nzuri, nyekundu, yenyi ncha sita, nayo yang'aa sana, ikaruka kama mshale ikaja ikampenya tumboni, ikawmamsha.

Yule mwanamke akafurahi, ulimwengu ukapata nuru, milima ikatetemeka, mawimbi yakatulia, maua yakachipuka, ikawa kama sauti ndogo kusema, “Enyi wafu watakaofufuka, enyi wazima wafao, ondokeni kasikieni, amekuja mwenyewe ndiye Buddha.” Hatta wanajimu na waganga wakamtafsiria ndoto mfalme, wakasema, “Maya atazaa mtoto mwanamme, mwenyi akili, na mponya watu wote, atakaewaokoa katika ujinga wao. Ama akitaka mwenyewe, atautawala ulimwengu wote.”

Na uzazi wake umehadithiwa hivi. Wakati ulipowadia, mamae akapita bustanini akakaa chini ya mti, mti ukainamisha matawi yake kumzunguka, inchi ikatoa maua tele, mwamba ukatoka maji mazuri, akazaa mtoto mume pasipo utungu.

Wakaleta machela, wakamchukua nyumbani kwa mfalme, na waliomchukua si watu: kama watu, lakini malaika wakuu wane wa pembe 'nne za inchi wakajigeuza watu wakamchukua. Asisikie vema mfalme habari hizi, akafadhaika atakuwaje mtoto huyo wa ajabu. Wakaja waalimu wake wakamwonya ya kwamba mtoto atakuwa mfalme mkuu, hakuna mwenziwe katika muda wa miaka elfu, mwenyi ishara saba, pete na almasi na frasi na tembo na waziri na jemadari na mke mzuri. Mfalme aka-

furahi akapiga mbiu watu wote wafanye siku kuu. Wakaupamba mji wakacheza ngoma, wakaiathimisha sana siku ile. Wakaja matajiri waliotoka mbali, wakaleta zawadi zao. Hatta akaja mtu, nae mzee na mtawa sana, kiziwi lakini mwenyi kusikia nyimbo za mbinguni walizoimba malaika juu ya mtoto huyo.

Bassi alipokaribia, Mfalme akamwondokea, akataka mtoto awekwe mbele ya miguu yake apate mbaraka ; asikubali mzee, akasema, " Sio " ; akamwabudu mtoto akasema, " Naam. Ndiwe Buddha, utahubiri torati, utaokoa watu. Heri nyumba hii ; lakini na huzuni yake ipo karibu." Bassi siku ya saba mamae akalala akafariki dunia akaingia rahani.

Wakakaa miaka saba. Mwaka wa nane yule mfalme akasema, " Nataka mwalimu amfundishe mtoto wangu yampasayo yote." Wakubwa wake wakajibu, " Mwalimu yuko, ndio Viswamitra, ndiye ajuae yote." Akaenda kuletwa, wakapiga bao, wakachagua siku yenyi ndege njema, mtoto akashika kibau chake na kalamu akasimama mbele ya mwali-mu. Mwalimu akamwambia, " Mtoto, andika maneno haya." Marra mtoto akayaandika maneno yale si kwa lugha moja tu, lakini kwa harufu nyingi za ginsi zote, akayasoma vema kwa tamko la killa lugha sawa sawa. Hatta mwalimu akasema, " Basi tena. Sasa kuhesabu. Sema, Mosi, pili, tatu, 'nne, hatta kumi ; tena asharini, thelathini, arubaini, hatta mia, na elfu, hatta lakki." Mtoto akasema zote sawa sawa hatta mia elfu, asisimame lakini akaendelea moja kwa moja hivi kwa kihindi, " Na baada ya lakki, koti ; na baada ya koti, nahuti ;" tena ninna-huti, na khamba, na ababi, na kumudi, hatta paduma, ndio ya kuhesabia mchanga mwembamba sana ; tena katha, ya kuhesabia nyota ; tena kotikatha kwa matone ya maji yaliyomo baharini ; tena kwa mchanga wote wa mto Ganjis marra elfu elfu fi elfu kumi.

Pana tena asankya, ndiyo ya kuhesabia matone ya mvua yote ikinya killa siku, siku kwa siku, ulimwenguni mwote miaka elfu kumi. Mwalimu akasema, "Vema. Na urefu je ? Pima." Mtoto akajibu kihindi, "Paramanu marra kumi, ndio parasukshwa ; parasuksha marra kumi, ndio trasareni ; trasareni marra saba ndio urefu wa vile vidogo vya hewani kama uvumbi ; na hiyo marra saba ndio ncha ya unyoya wa panya ; na hiyo marra mia, urefu wa chembe moja ya shairi ; tena wanda, tena mkono, tena pima, tena mkuke ; na hiyo marra mia nne ndiyo yojana. Basi jumla ya mavumbi, kusema vidogo vingapi katika yojana moja, ndio hii." Akasema barabba. Kumbe mwalimu amelala fulifuli mbele ya mtoto amsujudu, "Ndiwe mwalimu wa walimu, wala hukosi adabu ya mwanafunzi mzuri." Asiwe na kujivuna mtoto mwenyewe, akawaheshimu sana waalimu wake, akawa mpole na mzuri na mwenyi haya na adili, si mwoga, mtu wa kucheza, kuwindanyaama, kushindana kwa magari pamoja na wenziwe.

Lakini zaidi sifa yake ndio hii, mtu wa huruma, huruma ikamzidi siku kwa siku. Pangine akiwinda paa, humwacha paa, kwani paa amechoka. Pangine akishindana kwa frasi, huzuia frasi, kwani frasi wanatweta sana. Hatta pana siku palitokea kundi la ndege, mabata makubwa meupe mazuri sana, wanaruka kwenda milimani, wakiitikana, wakiimbiana. Marra Devadata, ndugu ya mtoto, akapinda upinde akapachika mshale, akafiga ; mshale ukampata ndege mmoja ya bawa, akaanguka akitoka damu. Mtoto akamtwa ndege, akamtuliza, akang'oa mshale, aka-mganga, akatia dawa. Akautwaa mshale akajichoma mwenyewe wa mkono apate kuona maumivu yake, akalia, akashika kumwuguza yule ndege tena, ginsi alivyomhurumia sana. Halafu akaja mtu akasema, "Bwana wangu ataka ndege yake." Akamwambia,

“ Ndege si yake, mzima bado ; hakumua, bawa tu limevunjika.” Devadata akasema, “ Ndege yangu. Ilikuwa juu, nikapiga, ikaanguka chini. Basi yangu. Lete.” Akamwambia, “ Hakuna. Yangu, kwani ndio haki. Na mimi, nina huruma. Lakini haidhuru. Twende kwa wazee, tukasikie maneno yao.” Wakaenda. Wakabarizi sana wakasema wengine hivi na wengine hivi, wasilikate neno. Hatta kuhani mmoja akaondoka akasema, “ Afadhalii aponyaε uzima, amiliki kitu kizima, kuliko afishae. Haya, mpe ndege.” Wote wakakubali, wakampa. Na yule kuhani asionekane, amegeuka nyoka akatoka, kwani malaika.

Siku nyigine mfalme akamwita mtoto akasema, “ Twende kutembea shamba, kwani baadae utarithi. Basi angalia kazi ya kulima na kuvuna na kupata mali.” Wakaenda, wakaona watu wanalima kwa ng’ombe, na wengine wanapanda. Tena ndege wakiimba na kuitikana na kufukuzana, na sungura waki-cheza na wajusi na nyuki na wadudu, na watu wakipiga ngoma, killa kitu na furaha yake, vizuri sana. Mtoto akaona akafurahi nae. Halafu aka-fikiri moyoni, akaona killa furaha na ina huzuni mwe-nziwe. Wale wakulima, kazi yao shidda, tena jasho; ng’ombe nao wakachoka wakapigwa ; hatta mjusi hula wadudu, na nyoka humla mjusi na mwewe humla nyoka—vivi hivi tu. Hatta habari yote ndiyo humwua auae na huuawa, bas. Mtoto akaugua, akakaa faraghani chini ya mti, fikira zake zikamzidi, “ Ginsi gani huzuni hii, asili yake, dawa yake nini ? ” Hatta roho yake ikachukuliwa kwa chechele, huruma ika-mshika, pendo likamwaka, kama moto wa kumtakasa ndani, akajaliwa pale pale kujitiisha nafsi, asiwe na haja illa kutaka kuponya wana Adamu na huzuni yao. Ndio mwanzo wa kuinuka juu na kuonja maisha ya baadae na kuingia njia yake. Akakaa sana katika fikira zake.

## 2.

Basi mtoto alipopata umri wa miaka themantashara, mfalme alimjengea nyumba tatu, zote nzuri, na killa nyumba mbali kwa namna yake. Mtoto akafurahiwa sana, akajikalia kwa anasa na michezo siku kwa siku. Lakini marra kwa marra fikira zake zikamrudia, babae akaangalia, akawaita wazee, akawaambia, "Naona mashaka juu ya mtoto huyu atakuwaje, kwani nampenda sana, nae hana buddi kuchagua mawili. Ama atakuwa mfalme mkuu mwenyi enzi, ndiyo nitakayo mimi, ama maskini na fukara mwenyi utawa na usufi. Bassi toeni shauri, tufanyeni tupate kumtia tamaa ya enzi na nguvu kuu ?" Mzee wa kwanza akamwambia, "Naona dawa ya kufukuza fikira hizi nzito, na ya kumtamanisha maisha nzuri, ndio mwanimke." Mfalme akasema. "Lakini tukimchagulia mtu asitake mwenyewe, je ?" Mzee wa pili akajibu, "Amrisha siku kuu, kaite wanake vijana wanawali wazuri wote waje kutazamiwa uzuri wao na kushindana. Kiishakupambanua walio wa kwanza, marra wapite mbele yake mmoja mmoja wapate kupewa zawadi na kuonana na mwenyewe. Ndipo utaangalia sana yupi ampendezae akamtia furaha, tutamchagulia aliemchagua kwa macho yake." Shauri hili likampendeza mfalme sana akapiga mbiu, akamrisha siku kuu, akawaita wanawali walio wazuri wote waje watazamiwe na kupewa zawadi zao. Wakaja wengi, killa mtu amejipamba akapiga urembo akavalia vizuri na marashi na hina na killa kitu, wakapita mbele ya kijana kwa haya na unyenyekevu, kwani walimwogopa, ginsi alivyo-kuwa mzuri na uso wa fikara nyingi na moyo wa kukumbuka mambo ya juu. Wakapita wakapewa zawadi wakaisha illa mmoja, jina lake Yasodhara ; nae alipokaribia, yule mtoto akashtuka, na yeze mwanimke haogopi, akasimama mbele yake, akajipakata

mikono kifuani, akamwambia, "Basi hapana zawadi yangu?" Akasema, "Zimekwisha, lakini mimi nina kitu cha kukupa." Akatwaa mkufu wake wa shingoni akamtolea, wakapendana sana.

(Baada ya siku nyingi, yule Buddha alipokwisha kuhitimu elimu yote, walimwuliza kwanini walipendana vile marra moja, akajibu, "Naona maisha hii ninayoishi sasa si maisha yangu ya kwanza katika dunia; kwani zamani sana nalikuwa na maisha mangine, nikawa mtoto nikakaa mwituni nikamchagua huyule kuwa mke wangu. Ndio maana twalitambuana tena.")

Marra babae akafurahi akatuma watu kwenda kumtaka yule mwanamke, kwani binti mfalme, tena wengi waliotaka kumoa. Baba yake akaleta majibu kusema, "Tushike dasituri yetu ndiyo hii. Ashindae wote kwa kupiga upinde na kucheza upanga na kupanda frasi, huyu amoe. Lakini kijana chako mtawa sana, labuda hajui kucheza." Mfalme akaona uchungu, kwani Devadata ndiye ajuae kupiga upinde, na Nanda ndiye ashindae kwa upanga na Ajuna kwa kupanda frasi. Lakini kijana alimwambia, "Mambo haya nimeyajua. Waite wote waje kushindana. Labuda nitampata mwanamke huyu." Siku ya saba wakaja watu wengi sana, wakubwa kwa wadogo, akaja na yule mwanamke amechukuliwa juu juu kwa gari la ng'ombe wenyi taji za maua na dhahabu pembeni, wakaja na Devadata na Nanda na Ajuna, akaja mwenyewe amepanda frasi wake Kantaka, akasema, "Haya, tushindane. Ashindae amtwa, kwani amestahili." Wakashindana. Nanda akaweka shabaha yake mbali kama mikono miteen, na Ajuna sawa sawa, na Devadata mbele kidogo, lakini yule kijana aliwekewa shabaha yake yapata mikono mia tatu. Akapiga Nanda, asikose shabaha yake, akapiga Ajuna asikose shabaha yake, hatta Devadata alistaajabisha wote

ginsi mshale wake ulivyopenya shabaha kwa nguvu sana. Mwanamke akaogopa, akasema "Labuda mtu wangu atashindwa." Akatwaa upinde mzuri sana, akauvuta kwa nguvu sana, ukapasuka, akautupa akasema, "Haufai neno. Hapana mwingle?" Wakasema, "Uko mmoja, umewekwa tangu hapo hekaluni, upinde wa Sinhabanu, lakini hakuna awezae kuupinda." Akasema, "Lete." Ukaenda letwa. Nao upinde wa ajabu, chuma wote, chuma pua, mweusi sana, mtoto akaushika akawambia wenziwe, "Jaribieni," wasiweze kuupinda hatta kidogo. Marra akautwaa akaupinda, akaliza uzi wake, watu wakasikia mbali kwao nyumbani wakasema, "Nini hii?" Wakaambiwa, "Upinde wa Sinhabanu, mtoto wa mfalmo ameupinda leo." Akapiga, mshale ukaenda, ukapenya shabaha katikati, ukaenda zake mbali sana usionekane tena kabisa.

Baadae panga. Devadata akachagua mti wa nussu shibiri unene wake akaukata tharuba moja, na Ajuna zaidi. Hatta Nanda akaukata mti wa shibiri kamili. Bassi kijana akachagua miti miwili, killa mti shibiri kamili, nao imeota pamoa, akapiga, akaikata miti yote miwili, isianguke, ilisimama vile vile, ginsi upanga ulivyo mkali, na pigo jepesi. Hatta upopo ukavuma kidogo, miti ikainama ikaanguka.

Tena frasi wakaletwa, Kantaka akawashinda wote kwa kwenda mbio sana. Kwenda kwake, kwa kope la juu na chini amekwisha kwenda urefu wa mikuke asharini. Hatta Nanda akasema, "Haifai kushindana na Kantaka. Lete frasi asiyefugwa." Wakala frasi mweusi ndume mkali sana, hana matandiko, amefungwa minyororo mitatu. Wale watatu wakapanda juu yake, marra wakaangushwa chini, kwani frasi mkali mno, hakubali kupandwa na mtu. Illa Ajuna tu alikaa kidogo, akamzuia frasi akamkimbiza, hatta frasi akafanya wazimo, akamuma mguu akata-

funa kwa meno, akamwangusha, akataka kumkanya-ga, akazuiwa na watu. Marra mtoto akasema, "Ondoeni minyororo. Nimshike kishungi cha kitwa-ni tu." Akamshika, akamsemea frasi neno kwa upole, akamtuliza, akampapasa kwa mkono shingoni na mgongoni, frasi akashindwa akainama kitwa kama akimtambua Buddha akimwabudu. Mtoto akapanda akamkimbiza. Wote wakamshangilia wakapiga ke-lele, "Huyu ameshinda, huyu." Akaondoka baba yake yule mwanamke, akamwambia, "Ndivyo tuliv-yotaka sisi, lakini ulipataje kushinda usipofundishwa, hatujui. Twaa iliyoyako." Marra Yasodhara akasi-mama, akajitia shela, akaja kwa mtoto, nae amesima-ma na frasi yule, akamwinamia, akasema, "Tazama, nipo, mimi kipenzi chako."

Marra harusi ikafanyika kwa dasituri ya Wasakya, karamu na zulia na maua na mkate mtamu na wali na kuzunguka moto marra tatu na sadaka na nyimbo na kufunganisha mavazi ya bwana harusi na bibi harusi. Asiwe radhi mfalme, babae akasema, "Tumemfunga moyo, tumfunge na mwili pia." Akajenga gereza, ndio nyumba nzuri mno isiyo na kifani kabisa kwa uzuri wake, katika bustani chini ya mlima Himalaya, yenyi mto na miti na killa kitu kizuri. Tena nyumba ya marmar na kioo na mawe ya tunu ginsi zote na matao na nguzo na vyumba vingi, na chumba kimoja cha ndani chapita vyote ginsi kilivyo fanywa na nakshi na taa na kazi nzuri na maua na vyakula. Tena wajakazi wengi wengi, nao wote wazuri mno, wazuri nyuso, wazuri na mioyo, wakitumika waki-cheza wakiimba na kupiga ngoma na vinanda na vinubi. Tena humo nyumbani mwote hakuna hatta kunena mambo ya huzuni na taabu. Ukinena utaa-dhibiwa, tena ukiwa huwezi, utaondolewa. Hatta maua yakifisia, marra hutupwa nje, kwani mfalme amesema, "Tumsahaaulishe uchungu wote na taabu ya

dunia. Labuda atakubali kutawala kuliko umasikini." Akaongeza tena kuzungushia shamba boma kubwa lisilopitika na mtu, na mlango mkubwa mzito wa shaba, kazi ya watu hamsini kuusindua mlango, na mshindo wake kama ngurumo, na ndani yake mlango wa pili na ndani yake mlango wa tatu, yote yenyi mapingo na makomeo, na kwa killa mlango walinzi wake wenyi kuamrishwa, "Usipishe hatta mtu, angawa mtoto wangu, msipate kufa."

### 3.

Buddha akakaa siku nyingi raha mstarehe, isipo-kuwa pangine usiku akilala na mkewe angstuka kama kwa ndoto, akalia, "Ee ulimwengu ! Ee ulimwengu wangu ! nasikia, najua, naja." Mkewe akaogopa akamwuliza, "Unani, bwanangu ?" kwani uso wake wenyi huruma isiyonenenekana, kama huruma ya Muungu. Asijibu lakini vema, hucheklea, huamuru kupiga zeze, zeze hilo likalizwa na pepo, likalia vizuri sana, lakini maana yake haitambulikani illa na mwenyewe, ikamfikirisha zayidi habari za maisha ya waana Adamu. Hatta siku moja wakakaa akaondoka mjakazi mmoja akawasumulia hadithi ya inchi za watu weusi pande za magaribi mbali sana, yule mtoto akaugua akasema, "Kama zeze lile, vile vile na kisa cha mjakazi inanifikirisha mambo mengi. Bassi nini ? waonaje ? inchi iko huko magaribi, nzuri na yenyi ajabu, na watu wake kama sisi, wengi, tena wenyi taabu, tupate kuwapenda na kuwafariji ? Hatta nataka mimi kuwa na mabawa ya tai nikapande kule juu ya mlima hatupe jicho huko na huko, hatazame nini iliyo nje ya milango." Akajibiwa, "Kwanza mji, bwana, mahekalu, bustani, miti, tena mashamha, makonde, msitu, mwitu, jangwa ; tena

inchi ya mfalme Bimbisara; tena ulimwengu huu mpana na sawa wenyi watu kama mchanga kama tope." Akasema, "Bass. Mwambie Channa atandike gari. Kesho aththuuri natoka kwenda kutazama." Wakamwambia mfalme, "Mtoto wako ameamuru kutandika gari kesho, aende kutazama watu nje." Mfalme akasema, "Vema, afathali. Wallakini asikari waende kwanza wakatangaze habari, wapambe mji, wala mgonjwa wala kilema wala kiwete wala mwenyi ukoma wala mtu thaifu asionekane kabisa." Marra watu wakafagia kote kote wakatia maji, wakapamba nyumba, wakapaka chokaa na rangi, wakatengeneza sanamu hekaluni, mji wote ukawa kama umeingia peponi.

Asikari wakapita huko na huko wakatangaza amri ya mfalme.

Hatta keshoye Buddha akaja amepanda gari zuri la ng'ombe wawili, watu wote wakampigia vigelegele, wakamtupia maua, wakamsalimu kwa furaha na kicheko, hatta akasema, "Kweli mzuri ulimwengu mwenyewe, na watu wazuri na wema, na mimi sikuwatendea hatta neno, lakini wanafurahi na umasikini wao na kazi nyingi. Haya ! twende." Wakapita ndani ya mji. Marra akatokea njiani katikati mtu, atoka kibandani, atambaa chini, kwa shidda na polepole, amevaa rakaraka, amegonda na taka sana, mzee mkongwe, na ngozi yabis imekauka na juu, kama ya ngamia, na mifupa wazi na kipofu, mgongo umemwinama, mvi zimemshuka mabegani, macho mekundu na machozi yatoka, meno hana, taya ikatetemeeka kwa ugonjwa na hofu ya kuona watu wengi wanapita na furaha yao. Akashika mkongojo kwa mkono mmoja akijiegemeza akitetema, na wa pili unamsonga mbavu, akavuta pumuzi kwa shidda na maumivu. Akasimama akiomba, "Bakshishi, bwana ! bakshishi bwana ! kesho kufa, labuda kesho kutwa,

sijui." Kikohozi kikamkaza pumuzi, asiweze kune-na, akanyosha mkono, akaugua kwa huzuni yake, "Bakshishi!" Marra watu wamsukumia mbali, wamsonga, "Toka wee! ondoka! huoni? ingia tunduni, mbwa!" Marra Buddha akasema, "Acha! acha! Channa, kitu gani hicho kama mtu, kama si mtu, ginsi alivyoinama na huzuni na hamu na maumivu? amezaliwa hali hii? asemaje, kesho kufa, kesho kutwa? hana chakula? kwani amekonda vile? nini iliyompata?" Channa akasema, "Mtu huyo, bwana, mtu mzee tu. Yapata miaka themanini, akawa kijana mzuri mwili na macho: sasa miaka ile mengi imemwibia uzuri, ikamteka nguvu zake, ika-mpunguza akili na moyo. Kama taa huyu, isiyo na mafuta, utambi unakwisha, inasinzia inakufa. Ndio uzee haswa. Bassi haithuru." Akamwambia, "Je? wote hupatwa hivi ao mmoja mmoja tu?" Akamwambia, "Ee bwana, wote hao vile vile wakijaliwa kuishi sana."

Akamwambia "Hatta na mimi pia, na mke wangu, na wale vijana vijakazi, wote watakuwa wazee hivi?" Akasema, "Naam." Akamwambia, "Rudi. Twende zetu kwetu. Nimeona nisiyothani kuona." Wakarudi, mtoto asile kitu wala kucheka wala kunena neno, hatta mkewe akamwangukia miguuni akasema, "Na mimi sina la kukufariji?" Akamjibu, "Faraja iko, mke wangu, faraja ya kunichoma rohoni, kwani itakwisha. Tutakuwa wazee sisi, hatuna buddi, wazee na thaifu wa akili na mwili. Tukiwa kama pete na kidole, sharti mwisho tusipendezane. Hatta moyo wangu una hofu na giza, na moyo wangu una mashaka, na moyo wangu hauna shauri ya kuukomboa upendano usiharibike na maisha mengi." Akakaa akikesha, usingizi hapana, wala faraja.

Hatta usiku ule mfalme akaota ndoto saba, zikamtia hofu sana. Ya kwanza, bandera kubwa nzuri ngafu,

kukaja upopo, ukaipasua, ukiangusha chini, wakaja watu wakaichukua kwa mashariki. Ya pili, matembo kumi marefu, wenyi pembe za fetha, wakatetemesha inchi kwa miguu wakapita njia ya kusini. Na mtoto wa mfalme amempanda yule aliyetangulia. Na ya tatu, gari la frasi wanne, moshi mweupe ukawatoka puani na popu jekundu kwa kutafuna meno, gari likang'aa mno hatta kutia kiwi machoni ; na juu ya gari mtoto wa mfalme. Na ya nne gurudumu, gurudumu likazunguka-zunguka, lenyi dhahabu kati na vito vya thamani, likaandikwa maneno ya kigeni, likaenda kama likiwaka na kulia. Ya tano, ngoma ya ajabu kati ya mji na mlima, mtoto wa mfalme akaigonga, ikatoa sauti kama ngurumo na mvua na tufano kuu. Ya sita, mnara, mnara ukapanda juu kwa juu kule mjini ukapenya mawingu uking'aa, na juu ya mnara mtoto wa mfalme amesimama, atapanya kwa mikono miwili lulu na almasi na feruzi na killa kito cha tunu, wakaja walimwengu wote wakadaka pande zote kwa juhudi na kushindana. Ya saba, sauti ya maombolezo, ndio watu sita wakilia wakisaga meno, na mikono juu ya kinwa, wakienda kwa huzuni yao.

Wasiweze waalimu hatta mmoja kuzitafsiri ndoto, hatta mfalme akaghathabika akasema, "Mabaya yanakuja nyumbani kwangu, nanyi hamwezi kueleza." Akaja mzee mtawa, vazi lake ngozi ya paa akasema, "Nichukue kwa mfalme, nitamfasiria ndoto zake." Akaletwa akasikia ndoto akasema, "Ndoto hizi zote furaha. Bandera, ndio dini ya kale itaondolewa, dini mpya itaingia. Tembo kumi, ndio karama kumi za hekima, na inchi itatetemeka, kwani iliyo kweli imekuja, imeletwa na mtoto wako. Frasi wanne, ndio wema ginsi nne, zitamtia mtoto wako nuru na furaha. Gurudumu la thamani, ndio torati ya thamani, naye ataiendesha ulimwenguni mwote. Ngoma, ndio ma-

hubiri yake. Mnara, ndio mafundisho yataenea sana, watu wote watapata fayida kubwa kwayo. Watu sita ndio waalimu sita walionyamazishwa na mtoto wako, kwani wapumbafu, naye maneno yake mazuri na yasiyokanikana. Ndiyo ndoto yako.” Mzee aka-sujudu marra nane chini akageuka akatoka, mfalme akataka kumpelekea zawadi, asipatikane. Wajumbe wakasema, “Aliingia hekaluni, tukamtafuta, hamna mtu, illa bundi tu akaruka akatoka nje. Kama ndiye hatujui. Labuda Muungu, tena amegeuka bundi.” Mfalme akaweka walinzi wa mlango wengi kuliko kwanza, mtoto wake asikimbie.

Lakini roho ya mtoto ikawaka tena, akaomba, “Nataka kuutazama mji wetu ulivyo hali yake ya siku zote, si kama siku ile tu, ulipojitia furaha makusudi. Nataka kutembea tu mimi na mtumishi wangu, nione desturi za watu na maisha yao na kazi, hapate urathi moyoni ao labuda kujua mengi.”

Mfalme akakubali, kwani alisema, “Labuda atazoea ; hivi moyo wake utamtulia.” Mtoto akajigeuza tajiri wa mji, na Channa ndiye karani wake, wakatoka wawili, wakazunguka mjini wakaona mengi sana , soko limejaa watu, tena wachuruzi madukani na wanunuzi wakipigana bei, na dalali na magari na mitumba na ng’ombe na mahamali na wajakazi wenyi mitungi na watoto wamebebwa pajani na washoni na wasaga ngano, na wahanzi, na wajume na wafua chuma na maseramala na waana chuoni na asikari na wafinyanzi na michezo na harusi. Walipokwisha, marra wakasikia kilio, “Shime, bwana ! shime ! nisike nifike kwangu nisipate kufa njiani.” Yuko mtu, ameshikwa na marathi mbaya sana, amelala chini ajinyonganyonga na kujipindapinda matopeni, na mwili wote upele na vidonda na malengelenge ; jasho likamtoka pajini mwa uso, na kinwa upande na macho ya wazimo, kwani maumivu yamuma sana.

Akakokota pumuzi, ataka kusimama, akasimama kidogo, akaanguka kwa mapindipindi na kujinyonga akilia, " Ah ! inauma tena. Shime, watu ! Shime !" Hatta Buddha akamwendea mbio, akamwinua pole-pole, akamweka kitwa magotini, akamtuliza kwa mkonono, akamwambia, " Ee ndugu, unani ? umepatwa na nini ? ee Channa, mbona atweta augua akokota roho akilia ? " Channa akasema, " Ugonjwa, bwana, ndio uliomshika, mwili umechafuka ndani, damu yamruka-ruka mishipini kwa nguvu kama moto, moyo wampi-gapiga, maungo yamelegea, nguvu zimemtoka shingo mgongo miguu pote pia. Uzuri umepotea na furaha hana. Hatta ataka kufa, asiweze mpaka ugonjwa umalize kazi yake, ndio utamtoka ; labuda utamwambukiza mwingine. Acha, bwana, usimshike sana, usishikwe mwenyewe na marathi." Asikubali mtoto kuacha kumwuguza mgonjwa, akauba, " Bassi pana watu wengi wenyi hali hii ? na mimi, naweza patwa hivi mimi ? " " Wengi, bwana, na ginsi zote, jeraha, ugonjwa, upele, mshipa, mtoki, buba, ukoma, vidonda, homa, kuhara, ginsi nyingi sana." " Tena huja, mtu asipothani ? " " Sana, kama nyoka, kama chui, kama umeme." " Bassi watu wote hukaa kwa hofu tu ? " " Naam, kwa hofu." " Asiweze mtu kusema, Mimi leo nalala mtu mzima, na kesho nitaamka vile ? " " Hawezi." " Na mwisho wa maumivu, ndio kuchakaa mwili na akili, ndio uzee ? " " Ndio, akijaliwa kuishi sana." " Lakini wasipoweza kuvumilia, waki-taka mwisho, ao waishi lakini thaifu sana na uzee ukiwazidi, nini tena ? " " Hufa bwana." " Hufa ? Ndio, mwisho kufa, wote mwisho hufa. Tazama huko." Mtoto akainua macho, akaona watu wengi wanakuja wakilia na kupiga maombolezo, mmoja aka-tangulia mwenyi chungu na moto, tena jamaa zake yule marehemu wamejinyoa vitwa wamevaa nguo za kuugulia, wakaimba " Ee Rama, Rama, utusikie !

Ndugu, mwiteni Rama." Tena jeneza, ndio mianzi na miti minne, juu yake mayiti, miguu mbele, imekonda, imekauka, macho yametota ndani, mifupa wazi, imetiwa mavumbi meupe na mekundu. Wakamchukua hatta njia panda wakamgeuza kitwa mbele, wakamleta mtoni, wakaandika kuni chini na mayiti juu, wakatia moto ; moto ukaenda ukaonja nyama ukala, ndimi zake zikacheza, ngozi ikakauka, viungo vikavunjika ; hatta moshi ukashuka, majifu yakatulia chini, na mifupa mmoja mmoja katika majifu, ndio mtu yule, ndio mwisho. Mtoto akasema, " Bassi huu ndio mwisho wa watu wote ? " " Ndio mwisho. Huyule alikuwa mtu wa kula, kunywa, kucheka, kufurahi, kuperenda maisha, hatta siku moja, labuda jiwe njiani, labuba maji mabaya, labuda nyoka, kisu, baridi, mfupa kooni, nyumba ilianguka, bass ! amekwisha, hapana tena. Haoni kitu, wala hataki. Kuliwa na karamu ya wadudu. Hii ndio ajali ya walimwengu, wakubwa kwa wadogo, wema kwa wabaya,—kufa. Hatta wakiishi tena baadaye mwisho vile vile kufa." Mtoto akatazama juu, na macho ya machozi, na sura ya rehema nyingi, tena chini, tena juu, kama akitafuta kitu asione. Akapaliza sauti, moyo wake umejaa upendo usio na kiasi na huruma na matumaini makuu, akilia, " Ee ulimwengu ! ee wenyi mwili wote, na wote ndugu zangu na wote hupatwa na huzuni na ma uti naona nasikia mateso ya ulimwengu yalivyo makuu, na furaha zake hazifai, na uzuri wake si kitu, na ubaya wake mbaya mno ; na mwisho wa anasa maumivu, na ya ujana uzee, na ya heri shari na ya maisha mauti, nami sikujuwa kwanza hatta kidogo. Sasa naona, nimepata macho. Mimi kama watu wangineo, wawaomba miungu wasipate kitu. Lakini wokovu upo, hamna buddi. Hatta miungu wenyewe hawana nguvu. Bassi je ? Muungu akiwa na nguvu awezaje kuumba ulimwengu akauacha uharibike ; asipokuwa na nguvu,

siye Muungu. Channa, twende zetu. "Bassi ! yatosha kutazama haya." Mfalme akasikia habari, akaongeza sana sana walinzi wa mlangoni, akasema, "Mtu asiingie mchana na usiku, wala kutoka."

## 4.

Lakini wakati wake ulipowadia, ndipo Buddha akaondoka nyumbani kwenda kukaa peke yake, jambo la huzuni kuu kwa jamaa, kwa watu wote wokovu wa kuisikia torati na kupata hali bora ya kuwa huru.

Usiku ule mwezi ulikuwa mkubwa uking'aa sana juu ya milima na boonde na mito na mji na nyumba, inchi yote ikatulia kimya, illa walinzi nje wanakesha kwa zamu yao, wakiitana wakipiga ngoma. Ndani wote wamelala, ndio jamii ya vijana waanake walitumika nyumbani mle, wote wamelala chini kwa balamwezi kama maua bustanini, ginsi walivyo wzuri sana wote wala hakuna kuchagua. Na katika kijumba cha ndani ndipo walipolala mwenyewe na mkewe. Lakini mkewe halali, yuna macho, ameamka, anakaa, atoka machozi, alia, ambusu mumewe mkono, amwita, "Amka, bwanangu, unifariji." Naye huibu, "Unani, kipenzi cha moyo ?" Akaugua vile vile, akamwambia, "Ah ! bwanangu, leo hivi furaha bora ikanipata, kwani naona nimepata mimba, ntazaa mtoto, lakini pale nilipolala, nalitokewa na ndoto tatu za hofu na ajabu, ndizo hizi. Kwanza fahali mkubwa mweupe, mwenyi pembe ndefu, apita kati ya mji, achukua pajini mwa uso almasi iliyong'aa kama nyota. Akaendelea pole pole, wala hakuna awezaye kumzuia, sauti ikatoka hekaluni, "Usipomsimamisha, utukufu umekwisha." Asiweze mtu kumzuia. Hatta nami nikajaribia nikamkumbatia kwa mikono, nikashindana

sana nikaamuru wafunge milango na kutia mapingo na komeo. Lakini yule fahali akalia, akainua kitwa akaniondosha mimi akaivunja milango, akakanyaga walinzi akaenda zake. Tena, wawili wa mbinguni wakashuka na jeshi kubwa, wakaingia mjini mwetu, marra bandera juu ya mlango ikaanguka, wakasimikisha ngine nzuri zayidi, kama imeshonwa na nyuzi za fetha, na yenyi kuandikiwa maneno mageni ya habari za furaha kwa viumbe vyote, upepo ukavuma, ikanya kama mvua ya mawe ya rangi isiyo na kifani huku kwetu." Buddha akasema, "Njema sana hii." Akamwambia, "Njema, lakini mwisho sauti ya bofу sana kusema, 'Saa yake karibu ! saa karibu !' Nikaota ya tatu, ndiyo hii. Kitanda hiki chetu nalikiona kitupu, mto tu na matandiko, bass. Mtu hapana. Na mshipi wangu wa lulu ulionipa ukageuka nyoka ya sumu, vikuku vikaanguka, mabanagiri yakavunjika, na maua ya kitwani majifu, kitanda kikaenda chini ya inchi. Nikasikia mbali fahali yule analia, na bandera inapigapiga, na sauti, 'Saa yake karibu !' Nikaamka, nisijue maana, illa labuda nitakufa karibu, ama iliyo mbaya zazidi sana, nifiwe nawe." Mumewe akamwambia, "Usithani, mke wangu, utakosa kuperendwa nami, ikiwa yo yote. Wajua fikara zangu za miezi mingi, ninavyoukumbuka ulimwengu na taabu zake, na kutaka mno kuuokoa, na zayidi wewe, nikupendaye sana. Bassi ikiwa huzuni halafu, labuda kwa huzuni yetu njia ya amani itapatikana kwa watu wote. Si hii faraja ? Bassi ulale sasa, nami naondoka nikeshe."

Akalala kwa machozi akaugua katika usingizi wake, akisema, "Saa yake imekuja," Buddha akatazama juu akaziona nyota kama zikimwonya, "Kweli, saa imekuja. Chagua mawili, mfalme ao maskini, kwa ajili ya ulimwengu." Akasema, "Nitakwenda, saa imekuja. Sitaki ufalme, sitaki fahari za vita, na sifa

kuu. Nataka kupotea katika inchi, kulala chini, kuvaan nguuo mbovu, kula taka, kwani huzuni ya ulimwengu imeniingilia moyoni, na kilio chake masikioni, na huruma imenijaa. Labuda kwa kujinyima yote na kujifisha tamaa na kutiisha mwili, nitapata dawa ya kuponya watu. Miungu yafaa wapi? sadaka zao na mathbahu na sala na wakohani na mahekalu? Yote hayo hayaponyi watu, huzuni, mateso, maumivu, ugonjwa, homa, uzee, mauti. Sisi watu wote kama wa mbegu moja, hatta na nyama na wadudu pia. Bassi akijaliwa mmoja kuondo laana yake, naona wenziwe wote watashariki watabarikiwa. Na zayidi akitokea mtu mwenyi mali na daraja bora na anasa nyingi na ufalme mkuu na enzi bora na afya njema na raha mustarehe, naye kijana bado, asiyechoka wala kukinaika na furaha zake na mapendezi mengi, hana upungufu wala maumivu wala hamu yoyote—akitokea bassi kama mtu huyu, kama mimi hapa, tena akiacha yote, akitupia mbali yote haya mema na mazuri kwa ajili ya kupenda watu tu, akajitoa pia kwa kazi moja ndio kutafuta njia ya kweli, siri ya wokovu—hakosi huyo atapata macho, atapata mwendo, atapata yote kwa kutupa yote, atashinda mauti kwa mauti yake. Bassi! Nakuja! Nitafanya! Naacha yote na mke wangu pia, nipate nuru nikaijue torati. Naondoka nisirudi 'tena, nisijepata kwanza nitafutayo."

“Akamtazama mkewe ya mwisho, akazunguka kitanda marra tatu, akasema, “Silali hapa tena,” akatoka marra tatu akarudi marra tatu, kwani alivutwa sana na upendo, akatoka asirudi; akapita kati ya vijana wakilala bado, asiwaamshe, akafika nje akamlilia mtu wake, “Amka, Channa, kamleta Kantaka.” Akazinduka kidogo, akasema, “Watakani, bwana wangu. Giza bado na njia haziendeki.” Akamwambia, “Kimya! Leta frasi! Saa imekuja, natoka mimi, kwendwa kutafuta njia ya kweli kwa watu wote.” Akasema

## VISA NA HADITHI

“Wala hutaki ufalme na enzi kuu, utakuwa mwo-mbaji ?” Akamwambia, “Ndio ajali yangu. Tena natafuta ufalme upitao zote. Tena yote hubadilibadili. Leta Kantaka.” Akasema, “Ee bwana kumbuka babayo atahuzunika sana, na jamaa pia. Utawazidhia huzuni tu.” Akamwambia, “Upendo wa ku-pendeza tu haufai neno. Nawapenda, ndio maana najitia huzuni na hao pia. Nawaacha nipate ku-wapatia wokovu. Leta Kantaka.” Akasema, “Vema, bwana.” Akaenda akamtandika frasi akamtengeneza vizuri, lijamu na hatamu na matandiko yote, akamleta kwa bwana wake. Frasi akafurahi mwenyewe aki-mwona. Buddha akamwambia frasi, “Kimya, frasi. Nichukue mbali leo, kitu kisikuzuie ; ruka kama moto, kama umeme.” Akampanda, frasi akakanyaga mawe, asimwamshe mtu, kwani usingizi mzito sana umewashika wote ; wakafika mlangoni, mlango uka-funguka peke yake na wa pili na wa tatu, isifanye kishindo, kwani kishindo chao kinasikika mbali sana, na ni kazi ya watu mia kusindua ile milango. Na walini wamelala wote, akatoka, akaenda mbio.

Assubui ulipopambazuka, ndipo akasimamisha frasi, akashuka juu ya frasi, akamwambia Channa, “Kwa maana umenipenda, utapata thawabu kuu. Rudisha frasi na nguo na mshipi na upanga, kampe mfalme baba yangu, kamwombie, afathali anisahau mpaka nirudi mwenyi enzi kupita wafalme kumi, na elimu pia. Natupa ulimwengu, niupate ulimwengu ; ikiwa watu hawaokoki illa kwa mtu, kwa kupenda watu, nawatafutia watu wokovu. Nikiona, upendo wangu utanilikisha ulimwengu.

Buddha akashika njia, hatta akafika palipo milima mitano karibu na mji wa mfalme Bimbisara, na katika milima mmoja Ratnagiri akakuta paango akakaa humo. Siku nyingi zikapita, na juu kali na baridi na mvua alizivumilia zote, amevaa kanzu ya manjano, siku kwa

siku aomba chakula mjini, usiku hulala chini tu. Hivi alitiisha mwili kwa kufunga na kukesha na kufikirifiki. Hatta alipokikaa na fikara zake kimya kabisa kama sanamu kama kifu, komba humpanda gotini, kaanga huleta vifaranga vyake kuja kupekua miguni pake, njiwa huja kula mchele wake mkononi. Tangu aththuri akaketi pale pale hatta magaribi, jua likashuka nyota zikatokea ngoma zikapigwa mjini, asiangalie wala kuondoka mpaka usiku wa manane, ndipo alala saa moja mbili, marra huamka tena, aka-simama juu ya mlima akitaza macho kutazama ulimwengu kwa kufikiri na kutafuta shauri la kuukomboa. Assubui kulipopambazuka, jua likapanda tena, Buddha akalisalimia akanawa akashuka mjini, akapita njiani akiomba nyumba kwa nyumba, akiokota kidogo huko na kidogo huko, watu wakampa kwa furaha, hatta waanake wakamletea watoto awaguse, ginsi walivyomheshimu akienda polepole na uso wa huruma nydingi. Halafu arudi kwake. Ndio desturi yake killa siku.

Bassi pale mlimani lakini chini kidogo palikaa kundi la watu wenyi hali mbaya sana. Wangine mikono imenyoshwa juu mchana na usiku siku nydingi, mikono ikakauka kama matawi makavu ya mtini. Wangine wamefumba mkono, vidole vimekazwa pamoja kwa nguvu, hatta makucha yakapenya kama misomari. Wangine, viatu vimetiwa misomari mikubwa, wangine wamejichanja kifua na paji la uso na pajani kwa jiwe wakajichoma palepale kwa moto. Wangine wamejipenyeza miiba na vibanzi katika nya-ma, ya mwili wao, wakajipaka matope na majifu wakavaa nguo mbovu za watu wafu ; wangine wanakaa penyi mizoga na makaburini ; wangine wakataja marra mia tano killa siku majina ya muungu wao Shiva, wamejifungia nyoka shingoni na pajani. Tena jua likawapiga, ngozi ikakauka, macho ndani, na

nyuso zimekonda ; hatta mmoja kazi yake killa aththuuri kubesabu punje elfu za ntama bassi, akila moja moja ; mmoja akachanganya majani machungu ; mmoja amejiharibu mwote, macho, ulimi, masikio, miguu, yote pia. Bassi hali ya watu hawa mbaya sana, lakini makusudi, wapate kuutiisha mwili, wakasema, "Tutapata furaha baadaye." Bassi Buddha akawaauliza habari, "Ndugu, mbona kuongeza hivi mabaya kwa mabaya katika maisha hii ?" Mmoja akajibu, "Imeandikwa, mtu akitiisha sana mwili, thambi zake zitaondolewa, roho itatakata itaingia raha ya peponi." Akasema Buddha, "Kama maji ya bahari yaendavyo juu yakafanya ya mawingu, yakachukuliwa milimani yakanya tena yakapita mitoni, yarudi baharini, sivyo na maisha ya watu, kwenda na kurudi ? Bassi fayida gani, akienda peponi, na halafu kurudia maisha ya duniani na maumivu yake vile vile ?" "Ah ! Bwana, hatujui vema, lakini mwisho wa usiku mchana, na mwisho wa uthia raha, na mwili huu twauchukia sana. Bassi twajasiria tuwezavyo, labuda miungu watatujalia furaha." Akamwambia, "Lakini furaha yenyewe itapita, bassi kazi burre, isipokuwa pana furaha ngine isiyo ya maisha hiyo, isiyo na mwisho. Hatta miungu yenu, ndugu, hawa-na mwisho ?" Akasema, "Brahma tu hana mwisho. Wangine hukaa tu." Akamwambia, "Bassi akili gani, enyi watawa na wagumu, kujitia athabu hizi mbaya pasipo hakika ya kufanikiwa, msipotumia akili na kuzisitawisha, makusudi mpate vema kutafuta njia ya wokovu ?" Wakasema, "Njia yetu hii tumeichagua. Bassi. Usipojua iliyo bora, pita. wewe." Akapita kwa huzuni yake, akiona watu walivyo wenyi hofu ya kufa wasithubutu kuivumilia hofu, wenyi tamaa ya kuishi wasithubutu kupenda maisha, wikitaka kuirithisha miungu wasipate urathi wenyewe ; akatazama maua, na miti, na ndege, akasema, "Wote

hao wanajifurahia maisha, illa watu tu hujitia huzuni makusudi. Kwa nini?"

Palitokea kijana mwanamke akamsujudu, aka-mwambia, "Huruma, bwana! huruma! Tazama kitoto changu! Leo alikwenda assubui kucheza msituni, akaona nyoka, nyoka akajipinda mkononi mwake, mtoto akacheza, akataka cheza nayo, akamchokosa nyoka. Halafu akalala akaacha kunyonya akazimia. Watu wakasema, "Sumu hiyo," na wangine, "Atakufa." Nikataka dawa, nisipate, wakasema, "Pana mtu pale mlimani, naye sufii. Mwombeakupe dawa." Ndio maana nimekuja. Huruma, bwana! huruma! Buddha akamkazia macho mwanamke, akamtuliza akamfunika mtoto, akasema, "Dawa ipo, dawa yake na dawa yako. Tafuta pilipili nyeusi, tola moja tu, lakini ndio mwiko, usitwae nyumbani kwenyi kufiwa baba ao mama ao mtoto ao mtumwa. Ukipata, leta. Ndio heri sana." Akaenda zake mwanamke, na mtoto amchukua, akiomba pilipili nyumba kwa nyumba, wote wakawa tayari kutoa, nao maskini pia, tena mwanamke huuza habari, "Lakini umefiwa nyumbani, baba, mama, mtoto, mtumwa," wakajibu, "Ee dada, neno gani hilo? wafu wengi, wazima wachache." Akarudisha pilipili, akaendelea akaambiwa vilevile, "Twaa pilipili lakini tumefiwa na mtumwa," "Twaa pilipili, lakini tumefiwa na mwenyeji," "Twaa pilipili, lakini aliyepanda amefariki." Asione hatta nyumba isiyofiwa. Akamwacha mtoto ukingoni mwa-mto akamrudia Buddha, akamwambia, "Mwiko mkubwa. Sipati pilipili. Bassini?" Akamwambia Buddha, "Ndugu, dawa yangu umeipata, kwa kutafuta isiyopatikana. Umefiwa, tena umejua ulimwengu wote hali moja nawe. Ndio faraja yako. Lakini kazi yangu, natafuta njia ya wokovu, laana hii iondolewe pia. Haya! mzike mtoto." Mwanamke akaenda zake.

Buddha akaona mavumbi yanarushwa na kishindo, marra kulitokeo kundi la mbuzi na kondoo wana-pelekwa mjini na mchungaji, na katika kundi koo la kondoo mmoja mwenyi watoto wawili, na mtoto mmoja ameumia mguu, hawezi kwenda, mama aka-sumbuka sana, akienda huko na huko na mtoto mmoja mbele na mmoja nyuma. Marra Buddha akamhurumia yule kondoo, akamshika mtoto yule aliyeumia akamchukua begani, wakaenda wote. Akamwambia mchungaji, "Mbona wapeleka kundi mjini, napo aththuuri sasa, na jioni bado?" Akasema, "Tumetumwa kuleta kondoo mia na mbuzi mia kwa kafara, kwani mfalme atoa thabihu kubwa leo kwa miungu yake." Akamwambia, "Na mimi nakwenda." Mfalme akaambiwa ya kwamba, "Anakuja yule sufii mkaa milimani, afuatana na kundi kuja kwa ibada." Bassi mfalme akasimama, na wakohani wengi wamevaa nyenpe, na mathbahu kati na moto juu ya mathbahu na damu chini inapita inanyewa mchangani, na mbuzi wa madoadoa tayari kuchinjwa, na kisu kooni, na mkokoni atoa sala yake, "Enyi miungu, mpendezewe na kafara na damu na nyama. Thambi za mfalme ziwe juu ya mbuzi huyu, zikaondolewe pamoja naye motoni. Bassi napiga." Asidiriki lakini, kwani Buddha alimzuia, akawambia mfalme, "Ee mfalme mkuu, asimpige mbuzi." Akamfungua mbuzi, mtu asimzuie. Akasema, "Kunrathi sana, ee mfalme, kasikiliza maneno yangu kidogo tu." Akapewa ruhusa akaeleza habari ya uzima, ulivyo kitu bora peke yake, huharibika na wote, haufanyiki na mtu. Wote huupenda, huushindania, huulinda. Watu tu wabaya; waomba huruma, na huruma hawanayo. Lakini viumbe vyenyi uzima kama jamaa moja na ndugu vyote. Tena damu ya mbuzi haitakasi roho. Miungu wakiwa wema, hawataki damu : wakiwa si wema, mbona

kuwaletea sadaka ? kondoo hachukui thambi za watu. Killa mtu atajijibia nafsi yake, atapata thawabu ya matendo yake, mema kwa mema ao mabaya kwa mabaya. Bassi alipokwisha, wakohani walijifunika mikono, mfalme akamkaribia akasikia Buddha akisema, afathali sana wasile nyama wala kumwaga damu, wale nafaka tu ; marra wakohani wakautawanya moto wakatupa visu, mfalme akapiga mbiu kusema, " Machinjo yote yamekwisha ; watu .wote wasile nyama wala kumwaga damu, kwani wenyi huruma ndio watakao hurumiwa." Mfalme akamwomba sana Buddha akae mjini mle, asikubali, akasema, " Nakwenda zangu mwituni, ndipo naona nitapata nuru, kwani nuru iko ; bassi ikipatikana tu, nitarudi kwako na shukrani." Akamwaga, akaenda zake, akakaa na fikara zake.

Mwisho ikaja nuru, mwisho wa miaka minane, karibu na mji Senani, alipokaa Buddha mwituni, akifkiri mateso ya watu na mambo ya ulimwengu na elimu ya vitabu na nyama za mwituni na siri za zamani za kwanza nazo za mwisho na uzima wetu wenyi kukaa katinakati. Hatta akasahau kutafuta chakula, akala matunda tu, mwili wake ukachakaa, uzuri ukapotea, akageuka si kama kwanza. Hatta siku moja alizimia akaanguka chini akalala kama mfu, akapita mtoto mchunga kondoo, akamwona amelala pale, macho yamefumbwa na uso umekunjamana ; akatwaa majani akamfanyizia kibanda, kitwa kisiumie sana na juu kali. Akakama mbuzi akamtia maziwa kitwani, si kwa mkono, kwani mtoto mwe-nyewe cheo chake kinyonge, na desturi ya Wahindi, haramu kabisa mtu mdogo wa chini amguse mtu wa cheo cha juu, ndio kunpasha unajisi. Buddha aka-jirudia akataka maziwa tena, mtoto akasema, " Mimi Sudra tu, siwezi kukupa kwa mkono." Buddha akamwambia, " Ndugu sisi na watu wote wenyi

huruma. Tena damu moja yetu sote, na huzuni moja. Bassi lete maziwa. Nikirudi, utapata fayidi." Akaleta kwa furaha.

Pana siku wakapita kundi la waanake wanakwenda ngomani, kwani siku kuu, killa mtu mwenyi urembo na zezena filimbi na kigoma, na njuga miguuni na viku-ku na banajiri, wakiimba uiinbo wao ; kama kusema.

" Nyosha vizuri nyuzi za zeze,  
Ilie tamu naswi tucheze,  
Ukivuta sana, zitavunjika, hailii tena,  
Ukilegeza, zitakuwa kimya, hailii tena.  
Piga piga nyuzi za zeze,  
Piga piga tuchezecheze."

Buddha akasikia akasema, "Wajinga ndio waalimu. Maisha yangu kama zeze, nimevuta sana nyuzi zake, na uzima wangu unaharibika, na macho yanapofuka, na nguvu sina, lakini nahitaji nisipate kufa, nisijediriki kutafuta njia ya wokovu." Akakaa chini ya mti wake. Waanake wakaenda zao.

Palitokea na mwanamke mwingine, naye mzuri sana, mke wa mwenyi shamba na mkuu wa mji Senani, amekaa sana na mkewe asizae mtoto. Yule mwanamke akaomba sana akatoa sadaka nyingi kwa muungu wa mwituni apate mtoto mume. Akapata, akafurahi mno, akaleta sadaka za shukrani, akaja zake mwituni amtolee Muungu. Akatuma kijakazi kwenda fagia kwanza mbele ya mti na kufunga nyuzi nyekundu. Yule kijakazi akamwona Buddha akathani ndiye, aka-mkimbia bibi yake akampasha habari. Bassi mwanamke akakaribia akamwona akathani ndiye akasujudu akamtolea sala na sadaka, ndio maziwa na marashi, hal waridi. Akala asiseme neno, marra akajiona nguvu zake zamrudia kama kwanza kabla ya siku za kukesha na kufunga, uso wake ukageuka mzuri, mwanamke akastaajabu akasujudu tena, akamwuliza, "Kweli ndiwe muungu ? tena sadaka zangu zimepe-

ndeza?" Buddha akamwambia, "Maziwa gani haya?" Akasema, "Nalitwaa maziwa ya ng'ombe mia, nikalisha ng'ombe hamsini, nikatwaa maziwa yao, nikalisha ng'ombe asharini na tano, nikatwaa maziwa yao, nikalisha ng'ombe thenashara, nikatwaa maziwa yao, nikalisha ng'ombe sita, nikatwaa maziwa yao nikapika na mdalasini na wali vizuri sana, nikaleta. Ndio sadaka yangu na ahsante yangu." Buddha akamwekea mtoto mikono yake kitwani akambariki, akamwambia mamaye, "Si muungu mimi, mimi ndugu yako, mfalme kwanza, sasa maskini aliyepotea miaka sita, nikitafuta nuru nisipate. Lakini nitapata. Hatta sasa iko karibu, inakuja, kwani maziwa haya yamenitia afya njema na uzima si kama kwanza. Lakini sema kweli, maisha yako ndio raha halisi na mstarehe, nini? watosha uzima na kupendana?" Akajibu mwanamke, "Kweli, bwana, maisha yangu yanitosha. Sitaki mengi. Bassi nini? Assubui naamka, naondoka, nasali, natoa chakula gbalani, natengeneza nyumba, naamria wajakazi kazi zao; hatta aththuuri huja bwana wangu, alala, nami namtunza namwimbia nampepea, hatta jioni namwandalia chakula, nasali hekaluni, naongea na rafiki, nalala, bassi. Tena nimezaa mtoto mwanamume, ndio faraja kuu. Tena nathani baadaye itakuwa mema kwa mema, na mema zayidi huko tena. Na huzuni najua labuda itakuja, nikifiwa na mtoto, ah! huzuni kweli! nife naye tu! ao mume wangu, lakini siogopi, navumilia, nitajitoa (ndio desturi yetu) nichomwe mzima pamoja naye, niimpatie furaha zayidi ya baadaye. Bassi si furaha kuishi hivi? wala siwasahau masikini na wagonjwa na wabaya pia, nawakumbuka, nawaombea. Bassi nafanya vema niwezavyo vema, naishika torati, naona ijayo yote itakuwa njema yote." Buddha akamwambia, "Ndiwe mwalimu wa waalimu. Umejua njia ya haki na kazi

ikupasayo usizidi kujuua neno. Umeniabudu. Nakubudu wewe. Tumaini liko kwa waana Adamu. Amani kwako na faraja siku zako zote. Uliyopata, niyapatie mimi. Ndio maneno yangu." Akamwiti-kia, "Ee bwana, upate tu," akaenda zake.

Marra Buddha akaondoka, akashika njia palipo mti mkubwa, mti wa hekima unakwitwa mbodi, akauendea akakaa kitako. Ndipo alipopata nuru, akawa Buddha halisi. Mambo yaliyompata Buddha huko chini ya mbodi, hatujui hakika, lakini yamehadithiwa hivi. Mkuu wa giza, ndio Mara, alipofahamu ya kwamba Buddha sasa atawapatia watu wote wokovu na njia na kweli na uzima, marra akampelekea jeshi lote la pepo zake mbaya, apate kumvuta na kumwogofya kumlegeza moyo. Wakaja wote wakamwendea kwa nguvu, na kwanza thambi kumi zilizo mbaya sana, kama mashetani makuu. Akatangulia mmoja, jina lake Mimi, akaja akamwambia, "Ukiwa Buddha, jiponye nafsi yako, usisumbukie wangine." Akasema, "Nenda kwao wajipendao wenyewe tu." Akaja wa piil, Mashaka, akamwambia, "Ubatili wa ubatili, yote ubatili. Hakuna msaada wa waana Adamu wala wokovu." Akasema, "Huna neno nami. Ondoka." Akaja wa tatu, Uwongo, akamwambia, "Maandiko Matakatifu, miungu na mahekalu yao, wakohani na thabihu zao, angalia usitharau." Akasema, "Natafuta kweli halisi, si kivuli chake." Akaja wa 'nne, ndiye Ngoa, mwenyi nguvu sana na mzuri, upindi wake wa thahabu na mishale mikali, akileta kundi ya waanake makahaba wakiimba wakipiga ngoma zao wakiimba, na mmoja amejifanya mfano wa mkewe Yasodhara, akamvuta sana kwa maneno yake mazuri na yenyi shauko, "Ee bwanangu, nirudie, nipo, nafa, nakutaka. Si mimi mkeo, kipenzi chako?" Akasema, "Mke wangu nampenda. Ndio maana wanivuta burre." Akaja wa tano, Chuki, asiweze

kuvumilia akimtazama tu kwa macho matulivu ; tena Tamaa ya maisha, tena Tamaa ya sifa, tena Kiburi, tena Kujiona, na mwisho Ujinga pamoja na watoto wawili, Hofu na Thulumu. Jeshi kubwa la mashetani na pepo wabaya wakafuatana nao, giza ikazidi, milima ikatetemeka, pepo zikavuma, mvua ikanya, nyota zikaanguka, inchi ikitikisika, hewa ikajaa vioja na vitiisho na mambo ya hofu. Yote burre. Buddha hakuangalia, alikaa tu na mti pia ulikaa mstarehe. Wakamwacha, wakaenda zao. Maana ya majaribu haya, Buddha amepata kujiweza, asishindwe na mabaya, Kwani hayamwezi tena. Bassi alipokwisha kujaribiwa hivyo, ndio mwanzo wa kupata nuru, macho yake yakafumbuka, akajua mambo matatu.

Kwanza akafunuliwa habari ya maisha zake yeye (kwani ndiyo imani ya Wahindi wa kale, killa mtu roho yake imepata kuishi marra nyingi na kuwa na maumbo mengi), akaziona zote taratibu tangu mwanzo hatta mwisho, maisha hamsi mia na hamsini, ndivyo alivyoishi, maisha kwa maisha, tangu maisha ya chini zilizo nyonge, za wadudu na nyama, hatta zile za juu zilizo bora na njema zayidi. Akazitazama zote tháruba moja, tena ginsi zilivyofungamana, killa maisha ilivyo mwanzo wa maisha ya pili yake, kama njema na ile ya pili njema zayidi, kama mbaya na ya pili imezidi, wema wote ukizaa matunda yake mema, na ubaya vile vile. Hatta killa roho ya mtu kwa ustahili wake ama hupanda, huzidi kuwa njema, huingia maisha ngine nzuri, ama hushuka, huwa mbaya zayidi, hupata maisha mbaya, killa roho kwa kadiri ya kutenda kwake.

La pili, akafunuliwa habari za ulimwengu wote na vilivyomo, jua kwa jua, nyota kwa nyota, dunia kwa dunia, vyote vikishika mwendowao, vikizungukazunguka visipotee wala kutulia, vikitiana mwanga na uzuri mwaka kwa mwaka, miaka mia kwa miaka mia, hatta

mwisho wake. Akafahamu ya kwamba iko nguvu ivie-ndeshayo vyote ikiviendeleza vyote vizidi kuwa na uzuri na kufaa, hatta vyote vigeuke vikapate kutengenezwa na kukamilika na kusitawi kwa kuitii na kuifuata kawaida ya nguvu hiyo. Na nguvu hii iko juu, juu ya miungu yote, haibadiliki, hainenekani, na yote chini yake.

La tatu, akafunuliwa siri kuu, ndio asili ya huzuni zote, akafahamu habari zake, ndiyo hii. Huzuni ni kama kivuli cha maisha kikifuatana nayo, kisichondoleka kabisa, isipoondolewa na maisha yenyewe na hali zake, uzazi, kukua, kuchakaa, upendo, machukio, furaha, maumivu, hali zake zote za kuwa, na kutenda pia. Bassi mwanzo wa hekima ndio kujua haya yote ni mitego tu, na kuyataka ni ujinga. Na kazi ya ujinga ni kutia tamaa ya mambo, na tamaa huzaa bidii ya kuyatafuta, na bidii yafanza desturi ya kuya-fuata, na mwisho uzima wa dunia hii uzidio siku zote kuwa na kiu ya mambo yake, ndio yenyi kuonekana tu, kiu ya kutaka anasa, makuu, mali, sifa, enzi, kushinda, kula matamu, kuvaan mazuri, na kuyashindania, kama kiu ya maji ya chumvi. Ukinywa, huzidi. Lakini mwenyi hekima hujikatazia mbali kiu hii ya rohoni, hukaza moyo kuangalia yaliyo kweli, hatafuti, hashindani, hathulumu ; huvumilia yote, hujizuia ; hivi huendelea katika utakatifu na kukamilika ; hatta mwisho hahitaji maisha tena wala mwili (hatta akipata, haithuru ; azidi kutakasika na kuwa kamili vile vile), hufika mwisho wa njia, hadanganyiki na dunia, hashindwi na tamaa, hashikwi na mambo ya kuonekana ; na mwisho wake, ah ! furaha isiyopitika, hataki kuishi tena, na maisha yaisha, yageuka kuwa isiyo maisha, illa kama shwari tupu na utulivu, na raha pasipo thambi, pasipo uthia, hali mbarikiwa, hali ya heri, hali isiyobadilika milele, ndio NIRVANA.

Lakini miaka ile yote sita yule mfalme babaye Suddhodana amekaa na huzuni yake, akimtaka mwana wake pia mkewe yule mzuri Yasodhara amekaa na huzuni yake, asipate furaha ya maisha, kwani ajiona kama amefiwa na mumewe. Pana siku marra nydingi ikaja habari ya wasafiri waliotoka mbali kusema, "Tumemkuta mtu aliyepotea naye mtawa, tukamrudisha kwake ;" lakini siye, wala hawakupata neno moja juu yake, kama amepotea, ao amesahau ao moyo wake umegeuka ao amefariki dunia. Hatta siku moja yule mwanamke alikuwa anatembea bustanini kando la kijito, naye amekonda, nguo zake za kukaa matanga, haendli upesi lama vizito, asiangalie maua na matunda na ndege. Na mkononi ashika mshipi ule ule wa lulu, aliompa Buddha siku alipokimbia, tena kwa mkono wa pili amwongoza mtoto wake mdogo, mzuri sana, naye mwanamume, jina lake Rahula. Na mtotoache ka, achesacheza, atupia samaki wali mtoni, mamaye augua moyoni mwake kwa kumtaka sana mumewe. Marra wakaja vijakazi wakasema, "Ee bibi, kumekuja watu mjini, matajiri, wenyi sifa njema, wametoka mbali baharini, wameleta vitu vizuri vizuri, nguo za thahabu, jambia, vyombo vya shaba, pembe, halua, dawa, ndege, tunu za ajabu sana ; lakini zayidi wasema, yuko, ameonekana, yule yule, mume wako Buddha mwenyewe, wamemwona wazi wazi, na kumasujudia, na kumtolea tunu, kwani amekuwa Mwalimu mkuu, mtakatifu, watu wote wamheshimu ; aleta wokovu kwa maneno mazuri na huruma nydingi. Tena anakuja hapa." Akaondloka bibi akache ka akapiga makofi, akatoka machozi ya furaha, akalia, "Waiteni, waiteni matajiri hao. Nina kiu ya kusikia habari. Waleteni upesi. Wakisema wa kweli, watapata zawadi kubwa, nanyi pia mtapata." Wakaja matajiri, akawaambia, "Ee bwana, mmetoka mbali, tena umemwona bwana

wangu, sasa mwalimu, mtakatifu, watu wote wamheshi-mu, anakuja hapa. Sio?" Mmoja akajibu, "Tumemwonna, bibi mkubwa, tumemsujudia sisi, kwani aliyepotea ameonekana, mkuu kuliko mfalme wa wafalme, penyi mti mbodi. Hajambo, apita mji kwa mji, ahubiri maneno mazuri na njia ya amani avuta watu, wamfuata kikondoo. Tena atafika hapa mbele ya masika." Akamwuliza, "Ginsi gani mambo haya?" Akaeleza habari ya mambo ya mbodini, tena kama kwanza Buddha alilala asithubutu kutanga za habari za furaha, akasikia sauti kama inchi ikilia, "Nime-potea, mimi na viumbe vyangu," na kama upепо ukivuma, "Ee mwalimu mkuu, tangaza torati yako." Marra akaondoka akisema, "Haya! Nahubiri. Mwenyi sikio asikie." Kwanza akafundisha watano, wakasikia kuna mwisho wa kufa na kuzaliwa, hakuna sharti kwa mtu illa matendo yake yeye, wala jehannum asiyofanyiza mwenyewe, wala raha baadaye isiyopatikana, akijiweza tu. Baadaye watu hamsini na nne wakaongoka. Wote settini wakatumwa na Bwana kwenda kueneza mafundisho yake, mwenyewe akaenda mjini kwa Bimbisara, akafundisha siku nyingi, wote wakamwamini, mfalme kwa watumwa; akapewa bustani nzuri, akafanya baraza akatoa hotuba, hatta watu mia kenda walivaa nguo ya uwaanafunzi, nguo ya manjano, wakafundisha wenyewe.

"Wovu huzidisha deni,  
Wema huzilipa pia,  
Acha wovu, shika wema,  
Jizuia. Ndio njia."

Yule mwanamke akasema, "Atakuja lini?" Wakamwambia, "Labuda mwezi mmoja bado."

Marra mfalme akatuma wakubwa wake kenda kwenda upesi kwa frasi, na killa mtu neno lake sawa, "Ee bwana, baba asema, njoo upesi, nisijekufa

kwanza.” Na Yasodhara pia alitura watu kenda kwa frasi kusema, “Bibi, mama Rahula, asema, ataka sana uje, na habari za wokovu pia ataka kuzisikia.” Wajumbe wakaenda upesi, wakafika, wakaingia bustanini, marra waliposikia maneno yake, marra killa mtu amekwisha kusahau neno lake mwenyewe, ni watu wa kusikiliza tu bassi, kama kulambishwa asali. Bassi mfalme alitura waziri wake mkuu, naye mwaminifu sana. Alipokiwasilia pale, akatwaa sufi akaziba masikio akaingia akamtolea Buddha neno la mfalme. Buddha akajibu, “Nakwenda, kwani imenipasa. Mwambie mfalme na bibi pia.”

Marra watu wakapamba mji, wakajenga kibanda kizuri cha miti na maua nje, wakatweka bandera, wakaweka ngoma tayari kupigwa, wakamtazamia sana killa assubui. Akachukuliwa bibi katika machela, akakaa kibandani mle nje ya mlango, akachungulia njia mbele, acauliza watu habari, asipate. Hatta mwisho akaona mtu anakuja pole pole, amenyolewa kitwa, amevaa nguo ya manjano, akashika chungu cha udongo, akaomba chakula nyumba kwa nyumba, watu wawili wakafuatana naye, wamevaa sawa sawa. Bassi yule niwenyi chungu alipopita, killa mtu kama hana buddi kumsujudia, ginsi alivyo na umbo la heshima na macho matakatifu na mwendo kama wa mfalme, wanginge wakaenda hima kutafuta sadaka zingine wampe, wakaulizana, “Nani huyu ?” Lakini alipokifikia kibanda, Yasodhara akamtambua akalia, “Ee ! Ee bwana !” akamwangukia miguuni akalala. Lakini mfalme alipopata habari ya kwamba, “Amekuja, lakini maskini, amenyolewa, amevaa mabovu, aombaoomba,” marra alichukizwa sana. Akatema mate chini marra tatu, akajing’oa ndevu, akatoka kwa haraka na ghathabu, akapanda frasi akamkimbiza, akapita mbio kati ya watu, akafika alipo. Asiweze kushika hasira yake, akatazama macho ya Buddha kama ya mtoto

amheshimiaye sana baba yake, akashuka juu ya frasi, akapiga magotichini, kwani alimwona mwenyi utukufu kupita wafalme, na umbo la kuwavuta watu wote na utisho. Wallakini alimwambia kwa uchungu kidogo, "Ndio mwisho, Buddha arudia ufalme wake kwa umbo la maskini, amevaa mabovu, amenyolewa, aombaomba. Wewe mtoto wangu, mrithi wangu, ungalikuja kwa fahari, na jeshi la asikari. Na sisi tumekutazamia tangu hapo. Kumbe maskini amekuja mbona?" Akajibu, "Babangu, ni desturi ya jamaa yangu." Akamwambia, "Jamaa gani waliofanya hivi?" Akasema, "Mabuddha wote ndio desturi yao, kuja nijavyo mimi, na kutoa nitoavyo mimi, tunu ya thamani nydingi, malimbuko ya hazina, ndio hii." Mfalme akastaajabu akamwambia, "Kitu gani?" Buddha akamshika mkono na Yasodbara, wakapita njiani pole pole wote watatu, akawaelezea habari ya wokovu, na mwisho wake NIRVANA. Wakasikia wakafurahi wakaamini sana. Bassi usiku ule wakaanza kukanayaga njia ya amani. Buddha akakaa miaka arobaini na tano akafariki, kama b.c. 412.

Na mafundisho ya Buddha ni kama haya. Uli-mwengu hauna mwanzo unaojulikana na sisi, wala muumba. Ni kama gurudumu izungukayo tu; na Muungu Mwenyezi hakuna. Haifai sadaka wala sala. Nguvu tu iko iendeshayo yote na maisha ya watu pia. Na maisha ya watu ni hivi. Huzaliwa, hufa; baada ya muda husaliwa tena na hufa; vivi hivi maisha kwa maisha. Na kwa ginsi ya maisha ya kuanza, ndivyo ginsi ya maisha ya pili yake. Maisha ikiwa mbaya na maisha ya pili yazidi; ikiwa njema, yazidi kuwa njema. Juu ya watu wenyewe kute-ngeneza ao kuharibu maisha zao. Asili ya kute-ngeneza ni upendano, na mwisho wake Nirvana, raha na amani na kustarehe milele pasipo maisha pasipo kufa.

Njia ya Nirvana ndio hii.

Jifunze kwanza habari hizi zilizo bora nne.

(1) Huzuni. Yote ni huzuni. Hatta furaha ina huzuni yake.

(2) Asili ya huzuni. Ni tamaa, kwani chanzo ya <sup>\*</sup> mabaya yote.

(3) Kikomo cha huzuni. Ni kujiwezo, kufisha tamaa, kushika njia ya Utakatifu.

(4) Njia, yenyi sehemu nane—

1. Elimu njema.
2. Nia njema.
3. Maneno mema.
4. Mwenendo mwema.
5. Kazi njema.
6. Bidii njema.
7. Utawa mwema.
8. Utulivu mwema.

Tena Njia ina madaraja manne, ndiyo haya—

(1) Wongofu, kama mlango wa kutaka utakatifu.

(2) La watu, wasio na shaka, wajiwao wenye-we, wasioegemea sala na sadaka. Kwao maisha bado moja tu.

(3) La watu, waliotakasika sana, wakahitimia upendano na amani.

(4) La watakatifu, waliokamilika, wakaingia NIRVANA.

Hao ndio waliozishinda thambi kubwa kumi, (1) kusema mimi ndimi, (2) shaka, (3) kuegemea sala na sadaka, (4) ngoa, (5) chuki, (6) tamaa ya maisha ya duniani, (7) tamaa za maisha ya peponi, (8) kiburi, (9) kujitumainia, (10) ujinga.

Amri za torati ndizo hizi tano—

- (1) Usiue.
- (2) Usiibe.
- (3) Usishuhudie kwa uwongo.

(4) Usilewe.

(5) Usizini.

Buddha alipofariki mafundisho yakaenea sana katika Hindi. Wakafanya mukutano, wa kwanza kama \*400 B.C., wa pili kama 300 B.C. na wa tatu kama B.C. 250. Kwani ndipo alipotawala mfalme mkubwa katika Hindi, jina lake Asoka. Hakuwa Mbuddha kwanza akaongoka, akafanya mukutano mkubwa wa Waalimu elfu. Baadaye akapeleka mtoto wake Silon (Ceylon) kumhubiria mfalme wake, B.C. 245; na yeye akawa Mbuddha. Pana tena ajabu hii. Yule mtoto wa Asoka alileta Silon mche wa mbodi, ule inti alipopata nuru Buddha, akaupanda Silon; nao upo, upo hatta leo. Umepata miaka 2137 mti ule, unatunzwa sana na wakohani na mamonaki wa Buddha.

Tena kama siku za Bwana wetu, elimu ya Buddha ikaenea sana Sina, na A.D. 300 ikaingia Korea na A.D. 500 Japan. Lakini dini ya Brama ikapata nguvu tena katika Hindi, Wabuddha wakafukuzwa, hatta kama A.D. 1100 hapana tena katika Hindi, wala leo hapana wengi. Katika Sina, Silon, Japan, ndipo wanapositawi.

## 2. WASINZIAJI.

ZAMANI za kale Wamasihiya walifukuzwa sana kwa ajili ya imani yao ya Kimasihiya. Palikuwa na watu saba vijana katika mji wa Anatolia (Asia Minor), uliokwitwa Efeso, nao Wamasihiya. Walikutana pamoja wakafanya shauri, wafanyeje. Sababu Dekio, mfalme wa Rumi, alikuwa anawaonea sana Wamasihiya, wakatafutwa pote wakachukuliwa wauawe.

Yule wa kwanza akasema, "Angalieni, ndugu, ginsi tunavyofukuzwa sisi Wamasihya. Haya basi

tujitie mikononi mwa liwali, sababu tukifa kwa ajili ya Bwana wetu Isa Masiya marra tutafika kwake mbingumi." Wa pili akasema, "Halifai shauri lako kwani kujitia mikononi mwa liwali ndio kujifisha wenyewe. Muungu hataki watu wajifishe. Amesema, 'Mkifukuzwa katika mji mmoja, kimbieni hatta mwingine.'" Wa tatu akasema, "Hatta na Kanisa takatifu ndivyo lilivyofundisha." Wa 'nne akasema, "Shauri langu ni hili. Twende tujifiche si mbali na mji. Halafu yake mafukuzo haya labuda yatakoma." Wa tano akasema, "Nami najua pazuri pa kufichia, ndipo pango penyi mlima Latmo. Hatta nimelala humo marra nyingi mwenyewe." Wa sita akasema, "Na mimi nina shauri, ndilo kuuza kwanza mali zetu zote tuwape maskini. Hivyo twaziweka mbinguni." Wa saba akasema, "Shauri hilo jema sana." Wote saba wakaenda zao wakauza mali zao, wakampa askofu, awape maskini, wakatoka mjini, wakafika hatta kwa mlima Latmo. Wakaliona pango, lime-funikizwa pia na majani na magugu, upo tena mti mmoja mdogo unakua karibu na mlango. Ikawa jioni wakakaa kidogo wakitazama jua linakuchwa kwa fakhari, wakala chakula, wakanywa maji, wakaweka makombo ya chakula akiba ya assubuhi wakasali wakalala usingizi.

Assubuhi wakaamka, wakamshukuru Muungu, wakataka makombo yale yaliyobaki jioni. Wakatafutatafuta sana wasiyaone. Wakastaajabu, wakasema, "Labuda nyama wameyachukua makombo, au wevi." Wakatoka nje kuyatafuta. Mmoja akasema, "Enyi tazameni mti huo. Jana ulikuwa mdogo, sasa mkubwa sana na mkuukuu, umeoza ndani. Ah ! Ajabu hiyo !" Wenzake wakasema, "Ajabu kweli kweli." Wakasema, "Tupateje chakula basi ? Hatuna buddi kwenda mjini." Mmoja, jina lake Iambeliko, akasema, "Mimi hapa nitakwenda. Niki-

kamatwa nakufa, haidhuru." Wakakubali wenzake, wakamsindikiza njiani mpaka chini ya mlima, wakarudi pangoni, nae akaenda zake peke yake.

Ikawa assubuhi na mapema, akapita njia kuu, asikute watu illa mmoja mmoja tu nao akawadhania kuwa wageni, namna ya nguo zao ilivyo ngeni, nao wakamsangaa yeye vile vile, wasimwambie neno. Akashika njia akakaribia mji akaenda taratibu, asiye akakamatwa. Akautazama mlango wa mji, napo ajabu mno, msalaba mzuri wa mawe umewekwa juu yake. Akafikiri moyoni mwake, "Ah! jana hapanam salaba, leo upo. Naona hila hiyo ya kuwadanganya Wamasihiya." Akaingia mjini. Akasema, "Mji umejaa wageni leo. Simtambui hatta mtu. Tena wote wamevaa sawa sawa. Wako wapi watu wa mjini? Kwani hunikazia macho?" Wakamtazama sana kweli kweli, wakasemana, "Mtu gani huyu? Tazama nguo za kishenzi. Mgeni na mjinga huyu." Akaendelea punde, akaona jumba refu na zuri la mawe ya marmár, lenyi mnara, na juu ya mnara msalaba mkubwa wa shaba. Akasema kimoyo, "Ee Muungu, unirehemu. Uchawi huo. Sifahamu hatta njia, hatta nyumba. Basi nini? Akili zimenipotea?" Akakuta na kijana akamwambia, "Ee rafiki, njia hii imekwitwa nini? njia ya Artemi, siyo?" Yule kijana akamchekelea, akasema, "Ee bwana, wewe mgeni. Njia ya Kiyama hii." Akasema, "Ya Kiyama? Jana njia ya Artemi, leo ya Kiyama. Ah! uchawi huu." (Na Artemi ndio jina la muungu wa uwongo, Waefeso waliomwabudu sana.) Akaona duka la mwokaji, akamjia, akataka mikate sita. Mwokaji akampa. Akatoa fetha, akataka kuivunja sarafu ya fedha. Mwenyi duka akatazama fedha ile akasema, "Fedha hii ya zamani sana. Umeipatapi?" Akamwambia, "Sijui. Nimepewa tu." Yule mtu akamwita mwenziwe aliyekuwa ana-

keti hapo karibu, akamwonyesha fedha. Wote wawili wakaiangalia sana, wakamjia kijana, wakamwambia, "Hatuna buddi kutafuta khabari za fetha ile. Unazo zingine kama hiyo?" Kijana akafadhaika sana, akawambia, "T'waeni zote basi. Uniache tu." Akatoa kifuko chake cha fetha. Yule mwokaji akasema, "Bado kwanza wee." Akafunga mlango, akazitazama fetha, akamwambia, "Ee rafiki, umeokota fedha hizo, fedha za watu." Kijana akatoka haraka, akakimbia. Watu wakamfuata mbio wakamkamata, wakamfunga wakamchukua kwa kadhi. Nae akichukuliwa akauangalia mji umegeuka pia. Hapana mahekalu ya miungu ya uwongo, hapana njia za kwanza, illakini misalaba ipo pote. Wakafika hatta kwa kadhi, mwokaji aka-mshtaki ya kuwa ana fetha zisizotumika wala kutambulikana siku hizi. Labuda ameokota, labuda ameiba. Kadhi akasema, "Huyu asema Kiyunani au Kirumi?" Mwokaji akamwambia, "Asema Kiyunani, bwana, lakini si vema."

"Jina lako nani?"

"Jina langu Iambeliko."

"Wakaa wapi?"

"Katika njia ya Ares."

"Katika mji upi?"

"Mumo humo, katika Efeso."

"Njia ya Ares! Ah! Siijui mimi."

"Ee bwana, waijua njia ile iendayo toka hekalu la Ares mpaka amfiteatro?"

"Una wazimu wee. Hakuna njia ile." Hatta mzee mmoja aliyekuwako akamwambia kadhi, "Ee bwana, nimesikia babu yangu akisema, ilikuwako njia ya Ares, zamani sana, sasa imegeuka." Kadhi akasema, "Mambo haya hayanielei. Basi wewe Mmasihiya?" Kijana akaona sasa atakuwa marra, akaungama, "Ndio, mimi Mmasihiya." Kadhi akamwambia, "Vema. Nalikudhania u kafiri." Kijana

akazidi kusangaa, akamwuliza kadhi, "Na Dekio je ? Dekio, mfalme wa Rumi ?" Akajibu, "Una wazimu kweli kweli wewe. Dekio amekwisha kufa zamani, yapata miaka miteen." Akasema, "Muungu ajuae, jana alikuwa mzima." Wakaita mtabibu wakamwambia, "Angalia huyu, hawezi kitwa, ana wazimu, nini ?" Mtabibu akasema, "Naona mzima huyu, lakini amefadhaika sana roho yake." Saa ile ile askofu wa mji akaingia katika chumba cha hukumu. Wote wakamwondokea wakamsalimu. Kadhi aka-mweleza khabari za kijana. Basi askofu akamwuza kijana, "Ee mwanangu, nipe kisa chako." Yule kijana akamwambia, "Baba wangu, kisa changu si chingi. Jana nalitoka mjini, sababu Dekio anafukuza sana Wamasihiya, nikalala usiku katika mlima Latmo, mimi na wenzangu watu sita. Leo nikaja mjini kutafuta chakula, kumbe mji wote umegeuka pia, hatta nimeambiwa ya kwamba Dekio amekwisha kufa yapata miaka miteen." Askofu akasangaa akafikiri, khalafu yake akamwuliza kwa werevu, "Sikilize, mwanangu. Wajua maneno haya ?" Askofu akanena maneno ya imani ya Nikaya, ndiyo ianzayo kwa, "Naamini kwa Muungu mmoja." Na maneno ya imani hiyo hayajaandikwa bado wakati wa Dekio, alipolala pangoni kijana yule. Baadae yamejulika sana na Wamasihiya wote. Basi askofu alipokwisha kunena maneno yale, kijana akasema, "Maneno mazuri hayo, lakini mimi sijayasikia." Akamwambia, "Nani aliye kuwa askofu wa mji siku zako ?" Akamwambia, "Aithala, ndilo jina lake." Wakafuliza kumwuza maswali mengi. Hatta pole-pole jambo lote likatokea wazi, kama kijana yule amelala usingizi muda wa miaka miteen. Wote wakafurahi, wakimwuliza khabari za siku zake, wakimwonyesha mji ulivyogeuka kuwa wa kimasihya. Wakaenda kwitwa wenzake wale sita, nao wakasangaa

sana. Khalafu yake Muungu akawatwaa, wakalala wasiamke tena.

---

### 3. KRISTOFER.

HADITHI ya Kristoferi ndio hii. Palikuwa na mtu katika inchi ya Sham, nae mtu hodari, mrefu sana kimo chake. Akaondoka akaenda zake kwa mfalme mmoja akamtumikia. Hatta siku moja akaja mtu mwenyi kazi yake kuimba nyimbo, akaimba mbele ya mfalme na wakuu wake. Na katika uimbo alimtaja Shetani, nae mfalme aliposikia jina lile baya, akajipigia alama ya msalaba. Yule mkubwa aka-mwambia, "Kwa nini kufanya hivi?" Mfalme akajibu, "Illi nilindwe na nguvu zake Shetani, kwani namwogopa." Akamwambia, "Kwamba wa-mwogopa Shetani, ye ye mkubwa kuliko wewe. Bassi naenda kumtafuta nimtumikie." Akaenda zake, aka-safiri mbali huko na huko, hatta katika nyika kuu akakuta njiani jeshi la watu wenyi silakha za vita, na mkuu wao uso wake mbaya na ukali kama haramia, akamwambia, "Ee mwana Adamu, wendapi?" Akaitikia, "Nakwenda tafuta mfalme Shetani, nataka kumtumikia." Yule mkuu akamwambia, "Kaa basi, ndiye mimi." Akamsujudia, akawa mtumishi wake, akafuatana naye.

Wakafika penyi njia panda, napo msalaba wa mti umewekwa. Na Shetani akikaribia akashikwa na khofu, akatetemeka. Yule mrefu akamwuliza sababu yake, akasema, "Sababu Isa Masiya akafa msalabani, mbele yake natetemeka kwa khofu." Akamwambia, "Huyo Isa Masiya mwenyi enzi kuliko wewe. Basi ndiye nitakaemtumikia."

Akaenda zake kumtafuta Isa, akawasili katika

pango, ndipo alipokaa peke yake mtu mmoja mzee nae mcha Muungu sana, akamtaka mzee amwonye-she Masiya. Akamwambia, "Masiya ndiye mfalme wa mbingu na inchi. Ukitaka kumtumikia Yeye, huna buddi kufunga na kuomba." Akajibu, "Kufunga siwezi, kuomba sijui." Akamwambia, "Basi, nenda mtoni mle, uwasaidie wavukao. Maji yanapita kasi." Jambo lile likampendeza sana yule mtu, akang'oa mnazi mzima, ndio fimbo yake, akakaa kule mchana na usiku, tayari siku zote kuwachukua wasafiri begani kuwavukisha mto.

Akakaa siku nyingi. Hatta siku mmoja akamtokea mtoto mchanga anasimama ukingoni mwa mto, akiilia, "Ewe mshujaa, nivukishe." Nae aka-mpandisha juu ya bega lake, akaitwaa fimbo, akaingia mtoni. Maji yakazidi yakajaa sana, ikawa dhóruba, na mawimbi makubwa, kitoto yule akazidi kuwa mzito sana hatta kumlemea, mshujaa akaogopa atashindwa na maji. Akapepapepa, akalevyalevy, khatima kwa shidda na juhudhi akafika ng'ambu. Akamwambia mtoto, "Nani wewe, mtoto? kama ningalitiwa ulimwengu pia begaui, singalikuwa na mzigo mzito kupita wewe." Mtoto akajibu, "Ewe shujaa, ume-chukua begani Aliyeumba ulimwengu pia na wewe. Walitaka kunitumikia katika kazi hii njema, basi tazama nimekukubali." Akaenda zake asionekane tena. Nae yule shujaa alijua kama amekubaliwa, akamsujudia Masiya. Kwa hiyo amekwitwa Kristo-fer, maana yake, mwenyi kumchukua Masiya.

#### 4. MAKARIO MTAKATIFU NA KITWA.

SIKU moja Makario, alikitembea mahali penyi maka-buri ya kale ya Wamisri, ndipo alipokaa mwenyewe,

akaona kitwa cha maiti, akakipindua kwa mko-ngojo wake, akakiuliza, "Cha nani hiki?" Kikajibu, "Cha mshenzi." "Na roho yake iko wapi?" "Iko katika jehannum." Makario akauliza, "Kwapataje kwenda kwake chini?" Kikajibu, "Kwapita mwe-ndo wa tokea mbingu mpaka inchi." Akauliza tena, "Wako watu tena chini yao?" Kitwa kikajibu, "Wako Wayahudi chini bado." Akauliza, "Hatta na chini yao tena wako?" Kikanena, "Wamasihiya Isa Masiya aliyewakomboa, nao wamejionyesha kwa matendo yao kama. wamemsahau kabisa, ndio walio-ko chini sana."

## 5. VITALI,

MTU ASIYEKUWANA SHUKRANI.

SIKU moja aliondokea mtu tajiri wa Venezia, mji wa Italia, akaenda kusaka nyama pamoja na rafiki zake na watumishi wengi. Jina lake yule mtu, Vitali. Na katika kusaka kule yee alipotea peke yake mwituni, akatumbukia katika shimo lililochimbia makusudi ya kukamata wanyama. Akaskinda humo siku nzima, mchana na usiku, kwa hofu nyingi na juhudhi, kwani shimo lenyi giza sana ; akakimbia huko na huko, akitafuta shina, au gugu, la kujikwe-zea juu na kutoka mle shimonii ; akasikia sauti ngeni na mbaya, vilio na ngurumo na uvumi, hatta aka-taka kufa kwa khofu zake nyingi, akajikunyata chini kimya, hana shauri la kuokoka illa kufa tu.

Hatta assubuhi yake alisikia mtu anapita karibu ya shimo, akapaliza sauti, akalia, "Ee mama wee ! mama wee ! njoo, njoo, unitoe humo shimonii, nakufa." Na yule mtu anaepita nimaskini, akamsi-

kia akilia, kwanza akaogopa, akakaa kitambo, akapata moyo, akakaribia shimo, akamwuliza, "Nani wewe uliomo ?" Akajibu Vitali, "Mimi hapa maskini mwindaji, nimeshinda humu siku nzima, mchana na usiku. Niopoe, nakusihi ; ukinitoa utapata thawabu nydingi sana." Na jina lake yule maskini, Massachio, akamwambia, "Ntafanya kadri niwezavyo." Aka-twaa mundu akakata tawi kubwa kidogo, akanena, "Ewe mwindaji, sikiliza maneno yangu. Nitaku-shushia tawi hili shimonii, ntalikaza sana mbavuni mwa shimo, na kulishika kwa mikono, nawe ulikamate sana ujivute kupanda juu, nwenda utapata kutoka." Vitali akamwambia, "Vema. Unitakalo lote utape-wa." Akamwambia, "Mimi sitaki kitu, illa nakwenda kuoa karibu, bassi umpe bibi arusi upendalo mwenyewe." Akalishusha tawi, marra akalionaa zito kidogo, kumbe nyani akatoka shimonii akiruka kwenda zake kwa furaha. Na huyo nyani nae ametumbukia mle mle shimonii, akalishika tawi akaruka juu. Aka-shtuka sana Massachio akakimbia mbali akasema, "Aliyesema nami humo shimonii hakosi shetani, ndiye shetani kwelikweli." Vitali akamlilia sana, "Ewe rafiki, umeniacha ? nakuomba, nakusihi, unitoe tu ; bibi arusi nitampa thawabu nydingi, ntakupasha utajiri. Mimi ni Vitali, mtu mkubwa mwenyi mali ; usinishindishe kwa njaa hatta kufa hapo shimonii." Bassi Massachio, akamwonea huruma, akarudi pale pale, akashusha tawi la pili, akalionaa zito sana, kumbe simba akaruka kutoka shimonii, akaenda zake mwituni akipiga ngurumo za furaha. Na Massachio amekimbia tena, akisema, "Hakika yake ndiye shetani aliyeeniiitikia, nimejua sasa." Marra akasikiliza Vitali analia kwa uchungu mwingi, "Kufa basi ntakufa kwa njaa. Hapana mtu anitoae. Uwae yote, rudi, nakusihi, unihifadhi, uniopoe kwani waweza. Nami ntakufadhili. Ntakupa jumba, na ng'ombe, na thahabu, killa uta-

kalo; niopoe tu." Akasimama, hana buddi kurudi, ashusha tawi, kumbe nyoka akatokea akipiga kelele ya furaha, akaenda zake. Massachio akapiga magoti, karibu kuzimia kwa khofu nyingi mno, akasali sala zote alizokumbuka, apate kumfukuzia mbali yule shetani. Na Vitali alia vilevile, nae karibu kukata tamaa pia, akasema, "Hakuna mtu wa kunisaidia. Basi tena, na nife tu." Akalia sana kwa machozi mengi na kuugua. Hatta Massachio akajirudia, akasema moyoni mwake, "Lakini sauti ya bin Adamu." Na Vitali akilia, "Upo hatta sasa? niponye, nipate kufa kwangu, wala sio hapo pabaya shimonii. Basi sasa. Sauti yangu imekwisha. Nikupe nini? jumba langu la mjini? mali zote? heshima? Twaa basi. Kana hukupata, niue. Uzima! uzima tu! ndio nitakao." Asiweze Massachio kukataa, alivyoomba na ahadi bora, akashusha tawi vilevile, akamwona anapanda, "Ah! umekuja basi?" Akaitikia, "Nimekuja." Akalia marra moja kwa furaha akazimia pale pale. Basi Massachio akamwuguza, akimtunza sana, khalafu akafufuka, aka-mshika mkono, akamwambia, "Twende zetu tutoke mwituni." Asiweze Vitali kwenda kwanza, kwani njaa imemshika sana. Massachio akatoa mkate katika mkoba, akampa. Akala, akapata nguvu kidogo, akamwambia, "Ewe mfathili wangu! Ewe mwokozi wangu! Ewe malaika wangu! niweze wapi kukulipa ulivyostahili?" Akamwambia, "Umeniahidia mchumba wangu mahari kubwa, na mimi jumba lako la mjini." Nae Vitali amezidi kupata nguvu akasema, "Kweli ntampa mali mchumba wako, na wewe ntakupasha utajiri mwingi huko unapokaa. Ukaapo wapi?" "Nakaa Kapalatta mwituni, lakini nataka kuuacha mji wangu na kukaa katika Venezia jumbani mle ulioniahidia." Akasema Vitali, "Sasa tumetoka mwituni. Najua kwa kwenda sasa. Ahsante sana." Massachio akamwambia, "Nije inini nilitwae jumba na mali hiso?" Akamwambia,

"Upendapo." Wakaagana. Vitali akaenda zake mjini, nae Massachio nyumbani kwake, akamwarifu mchumba wake khabari ya mambo yote yaliyompata, na mahari nzuri atakayopewa, na jumba atakamokaa.

Siku ya pili assububi na mapema aliondoka Massachio kwenda Venezia. Alipofika, akawauliza watu, "Wapi akaapo Vitali?" Wakamwambia, "Kule mbele. kidogo." Akaenda akafika, marra akaingia akawambia watu waliomo, "Karibu ntakuja mimi na mke wangu kwa gari, nitwae jumba nililopewa na Vitali." Wakasema, "Una wazimu." Wakaenda kumwarifu bwana ya kwamba yuko maskini amekuja, ataka mahari kwake, asema jumba hili ni mali yangu. Vitali akawaambia, "Mwondosheni marra moja, simjui." Wale watu wakaja wakamfukuza kwa mashutumu mengi, Massachio akarudi kwake mwenyi uchungu rohoni, asithubutu kumwamkia mchumba wake.

Alipoingia nyumbani, kumbe nyani amekaa jikoni upande huu, na simba upande huu, na nyoka amejikunja katikati. Akashikwa na khofu, akasema moyoni, "Yule mtu amenifukuza mlangoni kwake, sasa simba atanitafuna, nyoka ataniuina, nyani atanicheka. Basi ndiyo thawabu niliyoipata kwa kuwao-ko shimonii." Lakini sivyo, kwani nyani alimcheke-lea kwa upole, simba akatikisa mkia akaja akamlamba mkono, kama akimbembeleza, nyoka akajikunjua, akacheza miguuni kama akitaka kumshukuru. Massachio akapata moyo tena, akasema, "Enyi wanyama maskini! Bora hao kuliko Bwana Vitali. Yeye alinifukuza tu. Nataka sana kumtumbukiza mlemlle shimonii. Na mchumba wangu, ah! nalionna ntafanya harusi nzurinzuri. Nami sina hatta ukuni, sina chakula, sina fedha. Mbaya yule, hana hatta shukrani, na mali zile na jumba, ah!" Ndiyo maneno ya Massachio, akaona uchungu sana. Marra nyani amtazamisha kama akitaka kumwita, na simba azidi kutikisatikisa

mkia sana, na nyoka kunyonganyonga upesi upesi. Tena nyani alimwendea Massachio akampungia mkono amfuate, akampeleka kipenuni, kumbe zimo kuni nyangi sana zimewekwa kipenuni, kuni za kutosha kwa mwaka. Nae nyani ndiye aliyeokota kuni mwituni, akazileta nyumbani kwa Massachio. Akafurahiwa sana, yule nyani alivyokuwa na shukrani. Tena simba akatoa ngurumo lakini si ya nguvu kama ya kumwita tu, akampeleka pembeni mwa chumba akaona nyama tele ajabu, kondoo mbili, wana mbuzi watatu, sungura wengi, nguruwe wa mwituni, yote imewekwa taratibu, imefunikizwa na majani isioze. Nae simba ndiye aliywemwindia mfadhili wake. Massachio akapendezewa sana. Tena akamwambia nyoka, "Na wewe je ? Hukuniletea kitu ?" kama huyo nyani, kama simba ?" Marra nyoka akapenya chini ya majani makavu, akatokea tena, akajisimikisha kitwa juu, Massachio akaona kwa ushangao mwingi iko almasi nzuri sana kanwani. Akalia, "Loo masalale ! Almasi hiyo !" akanyosha mkono kuitwaa, na kumpapasa nyoka.

Marra Massachio akaenda mjini, kwenda kuiuza almasi apate mali yake. Akaenda kwa duka, mwenyi duka akaitwaa almasi akaitazamisha sana, akaona kama kubwa na nzuri. Akamwambia, "Kem ? wauzaje ?" Akamwambia "Reale miteen." Akidhani ndio nyangi, kwani hakujua thamani yake haswa ndiyo elfeen. Mwenyi duka akamchungulia, akasema, "Ukiuza hivyo, umeiba. Utafungwa." Akamwambia, "Ee Bwana, haidhuru. Labda miteen ndiyo nyangi. Lete mia basi. Nyoka aliyenipa." Wakaja asikari wakamchukua kwa kadhi.

Basi pale penyi kadhi alisumulia habari zote za mambo yaliyompata. Hakumsadiki. Lakini kwa saba-bu Vitali yumo katika jambo lile, kadhi aliwaita watu wakubwa, wakafanya baraza. Massachio akawekwa

mbele ya baraza. Mkubwa mmoja akamwambia, "Toa khabari zako. Uki sema uwongo, utatupwa mtoni." Akazitoa pia. Mkubwa akasema, "Basi ukamwokoa Vitali?" "Ee wallah! bwana." "Akakufukuza vibaya mlangoni kwake?" "Ee wallah! bwana." "Mwite Vitali." Akaenda kuitwa akaja. Mkuu wa baraza akamwambia, "Vitali, wamjua mtu huyu?" Akajibu, "Simjui mtu huyu." Watu wa baraza waka-fanya pamoja, wakasema, "Mtu huyu Massachio ni ayari mkuu. Afungwe gerezani basi. Vitali, nenda zako." Wakamwita asikari, wakasema, "Mchukue huyu gerezani." Massachio akapiga magoti pale barazani, akalia, "Ee bwana wangu! bwana wangu! labda mtu aliiba almasi. Labda nyoka aliyenipa alitaka kunitanganya. Labda yule nyoka, na simba, na nyani, ni mashetani tu. Lakini nalimwokoa Vitali, ndiyo kweli. Ewe bwana Vitali, sikutakii mahari, wala jumba, illa neno moja tu. Usiniache nifungwe gerezani, usiniache. Sikukuacha wewe mle shimon." Vitali akawambia watu wa baraza, "Sina neno mimi, illa nililolinena tu. Simjui mtu huyu. Aweza wapi kuleta shahidi hatta mmoja?" Ghafula hiyo watu wote waliopo walitiwa khofu na ushangao mwangi, kwani simba, na nyani, na nyoka, wakatokea pale penyi baraza. Na nyani amepanda juu ya simba, na nyoka amejikunja mkononi mwa nyani. Wakiingia, simba akanguruma, nyani akacheke, nyoka akatoa kilio. Marra Massachio akanena, "Hao ndiyo wanayama wa shimon." Watu wakatulia tena, mkuu wa baraza akamwambia Vitali, "Umesema, wa wapi mashabidi yake Massachio? Basi Muungu amewa-tokeza sawa sawa mbele ya baraza. Muungu ndiye shahidi juu yako. Basi na sisi hatuna buddi kukua-dhibisha kwa sababu huna shukrani. Jumba lako na mali zote umetwaliwa, utafungwa gerezani maisha yako pia. Na wewe, Massachio, kwani umeahidiwa

na mkuu wa Venezia jumba la marmar, na mahari ya mchumba, serkali itakufikilizia ahadi hiyo. Jumba la Vitali na mali zake ni zako. Na wewe, karani, uandike khabari za mambo haya yote, watu wa Venezia wapate kujua siku zote kama kwetu sisi watu wa baraza kuu killa mtu hakosi kupata haki yake aliyostahili.” Basi Massachio na mkewe wakaingia jumbani pamoja; na simba, na nyani, na nyoka, wa-kakaa raha mustarehe maisha pia.

---

## 6. YOVINIANO,

### KAISARI ALIYEJISIFU.

ZAMANI za kale aliyetawala ulimwengu wote ndiye mfalme wa Rumi, akaitwa kaisari. Palikuwa na kaisari, jina lake Yoviniano, akajinyosha kitandani, akafikiri enzi yake kuu na mali nyingi nyingi, moyo wake ukajivuna mno kupita kiasi, hatta akasema, “Hakika yangu, hakuna Muungu mwingine illa mimi.”

Bassi siku moja assubuhi kaisari akaondoka akawaita wawindaji wake na rafiki, akaenda kuwinda paa mwituni. Wakawinda wakawinda, jua likapanda juu, Yoviniano akasimamisha frasi ukingoni pa kijito kilichokipita katika inchi yake, nacho kijito chenyi maji mazuri meupe sana. Alipoona maji yale, aka-taka kuoga, akawambia watumishi, “Kaeni hapo, mimi nakwenda kule kwenyi miti mingi kando la maji, nioge peke yangu kwa faragha.” Marra akaenda kuoga, akavua nguo, akaingia majini, akachezacheza kwa baridi. Alipokioga pale, mtu aliyefanana nae umbo, na sura ya uso, na sauti, pia sawasawa akakaribia mtoni, asionekane nae, akavaa nguo za kaisari,

akapanda frasi wake, akaenda kukutana na wawindaji, nao hawakumtambua, kwani uso na nguo sawasawa, wakadhani kama ndiye kaisari niwenyewe, wakamtii wakamfuata huyo kaisari mgeni hatta jumbani kwake. Khalafu Yoviniano akatoka majini, akatafutatafuta nguo na frasi, asipate. Akawaita watumishi kwa sauti kuu, wala hawakumsikia, kwani wamefuatana nae kaisari mgeni. Basi Yoviniapo akajiona uchi akasema, "Ole wangu maskini ! Hali hiyo mbaya kama ipi ? Niende wapi ? nani atakaenikaribisha nikiwa hali hiyo ? Lakini kuna mtu mmoja tajiri akaa karibu, atanihifadhi, nami nitamzidishia daraja bora sana. Haya niende kwake, nipate kwa msaada wake kurejea kwangu na kumrudi yule aliyenidhulu-mu." Akaenda vile alivyo, mwenyi uchi na haya nyingi, akawasili hatta jumbani kwa tajiri, akagongonga mlangoni. Akaja mngoje mlango, hakumfungulia, akasema, "Nani wee ? watakani ?" Yule kaisari akizidi kugonga sana, "Fungua, fungua, mbaya wee !" Akamfungulia mzee mlinzi akamwona mwenyi hali ngeni sana, akamwambia, "Lo-o-o-o rafiki ! mtu gani nawe ?" "Mtu gani nami ? simi kaisari ? mwambie bwana wako, Yoviniano yupo amekuja, anilettee frasi, na nguo, kwani nimeibiwa." Akajibu mlinzi, "Kaisari gani wee ? siye kaisari amepita sasa hivi, akaja hapa, na watumishi wengi, akamwamkia bwana wangu, akala nae meza ni. Wee kaisari ? ah ! mzuri peke yako kweli ! ah ! ntamwambia bwana. Yeye atajua kama mwenyi kichaa, au umelewa, au mwizi labda." Mzee akachukizwa sana, akaingia kwa bwana wake, akasema, "Yuko mtu chini amesimama, hana nguo hatta kidogo, ajiita kaisari, ataka nguo na frazi mzuri." Tajiri akasema, "Mlete hapa." Wakamleta, akasimama mbele ya tajiri, akasema kwa nguvu, "Mimi Yoviniano." Wakamcheka sana. "We-we kaisari ? una wazimu, somo. Haya mpe kaniki

bovu kuzuia imbu usiku." Akasema, "Ndimi kaisari, bwana wako Nalikupasha utajiri mwingi, na heshima. Khalafu ntakuadhibisha kwa matendo haya." Yule tajiri akaghadhhabika mno, "Mbwa! mjinga! nawe kaisari? mwenyi kutawala ng'ombe na mbuzi, naona. Bassi bwana wangu hakula nami sasi hivi, na kuzungumza? hakuniambia nimshindikize kidogo njiani, nikarudi sasa hivi? nalikudhani kwanza kuwa mjinga, sasa nakujuua u mwerevu. Haya mtupeni huyo, kampigeni mijeledi tangu hapa hatta kule mtoni." Wakampiga hatta wakaisha. Yule kaisari akakaa kitako akajifungia nguo, akafikiri ulimwengu ulivyomsonga, akasema "Ee Muungu," (kwani sasa amkumbuka Muungu, wala si nafsi yake tu), "hali gani mbaya na maskini niliyopata, kwa maana yule niliyemfadhilia sana hana shukrani!" Wala haku-jiangalia nafsi yake asivyomshukuru Muungu, mwenyi kutweza na kuwatukuza wafalme wote. Ataka kuji-lipiza kisasi tu, kwani mwili wote unauma kwa kupoigwa kwa mijeledi. Akasema, "Ntampiga, ntamtubisha, hatta anijue nna nguvu ya kupa na ya kuondoa. Haya, niende zangu kwa mwingine, mkubwa na diwani. Yeye atanijuua, atanionea huruma katika msiba wangu."

Akaenda kule, akabisha mlangoni, mngoje mlango akamfungulia; akamwona, akamwuliza, "Wewe u nani? kwani kubisha?" Akajibu, "Mimi Yoviniano, rafiki. Nimeibiwa nguo nikioga, sasa sina nguo illa kaniki bovu bovu, wala frasi sina. Umwambie bwana wako, kaisari yuko." Mngoje mlango akazidi kushangaa, akaenda kwa bwana wake, akamwambia maneno yake Yoviniano. Bwana akasema, "Mlete basi. Labuda mwenyi wazimu huyo." Wakamleta ndani, akamtazamisha sana uso, asimtambue. Yoviniano akampasha khabari zake akafanya ukali tena, hatta yule diwani akamsikitikia, akasema, "Ewe maskini,

mimi nimerudi sasa hivi katika jumba la kaisari, nikamwacha pale pale. Basi ndiwe yee? Haya, mchukue gerezani. Labuda atapoa, apate akili tena. Nenda basi, nakusikitikia sana." Watumishi wakamchukua wakamlisha mkate na maji, baada ya siku wakamwondoa, kwani alifulia kusema, "Ndimi kaisari." Basi alipofukuzwa vile, alitoka machozi mengi ya uchungu na huzuni, kwani hali yake mbaya sana, akalia, "Ole wangu! Niende wapi?" Hatta yule diwani mwema hakunitambua, alinidhani kuwa mweenyi wazimu. Haya, nitakwenda nikajitambulische kwa mke wangu. Hakosi ye ye atanifahamu.

Akafika mlangoni kwa jumba lake, akataka kuingia. Mngoje mlango akamwambia, "Ewe maskini unani wewe?" Akajibu, "Umenitumikia yapata, miaka khamstashara. Basi hunitambui?" "Ee mbuzi, kutumikia gani huko? namtumikia kaisari mimi, lakini wewe? ah! hasha!" "Ndimi kaisari. Hunifahamu? Ee rafiki, nenda kwa malkia, kaseme; Mwenyi mawaa matatu kifuani amekuja, —ndiyo ishara kama ndimi. Basi anilettee nguo za kifaume, nilizoibwa." "Ee-e-e, akili zinatembea kweli! Kaisari yuko anakula na mkewe. Haidhuru, nakwenda, nipate kukurudi khalafu kwa bakora nyingi. 'Mawaa matatu kifuani!' Hakika utapigwa sana." Akaenda kwa malkiya akamwarifu maneno yake mwenyi wazimu, malkia akainama kitwa, akamwambia bwana wake, "Ee bwana wangu, yuko mtu mlangoni ameniita, ameonya zile dalili zisizojulika na mtu illa mimi na wewe, asema, lete nguo za kifaume, ukankaribishe, kwani mimi mume na bwana wako." Kaisari mgeni aliposikia haya, akatuma watu kwenda kumwita Yoviniano. Akaingia mbele yake, wala mtu hakumtambua, wala mbwa wake aliyemzolea sana zamani akiwinda nae, wala ndege yake aliyemfuga, wote hawakumtambua,

kwa ginsi alivyogeuka kuwa kama mtu mwingine. Kaisari akawambia wakubwa wake, "Sikilizeni ntakayomwuliza huyu." Wakasikiliza. Akamwuliza khabari, "Jina lako nani? wataka nini kwa malkia?" Akajibu Yoviniano, "Jina langu nani? kwani nimekuja? simi kaisari, mwenyewe wa nyumba hii na ufalme pia?" Akamwambia, "Basi hao wataka-oamua. Semeni nyie, yupi aliye kaisari, mimi ama huyu?" Wote wakamjibu, "Ah! bwana, maneno gani hayo? Hapana shaka, wewe kaisari, tumekujua tangu utoto. Huyo maskini mnyonge hatumjui yu nani." Watu wote wakataka sana aadhibishwe. Tena kaisari mgeni alimwuliza malkia, "Sema kweli, wamkumbuka mtu huyu ajitaja mfalme wa inchi?" Akamwambia, "Ee bwana wangu, siyo miaka thelatini niliyojulikana nawe nikakuzalia watoto? mbona umeniuiliza? illa hiyo tu ndiyo naajabisha, amepataje kuijua ile siri yetu, ile dalili." Basi yule mgeni akamwita Yoviniano, akamtolea ukali sana kwa ufidhuli wake, akaamuru asikari wamfungie frasi miguu, apasuliwe mbali mwili wote. Amri hiyo alitoa wazi, khalafu akatuma mtu kwenda kwa asikari kusema, wampige mijeledi, na kumwacha. Yoviniano akataka sana kufa. "Mbona niishi basi? rafiki, watumishi, hatta mke wangu wanichukia, nao nilio-wafadhili sana wanitupa. Haya niende kwa kasisi, kuae nimeungama dhambi zangu na makosa marra nyingi. Labda yeye atanitambua." Na yule kasisi akaa kijumbani karibu kidogo na jumba la mfalme. Yoviniano akabisha hodi, na yule kasisi akisoma ndani, akaitikia, "Nani huyo? Mbona wanisumbua?" Akamwambia, "Mimi kaisari Yoviniano, fungua dirisha, niseme nawe." Kasisi akafungua dirisha dogo, akatazama nje, akaona hapana mtu illa maskini amevaa nguo mbovu mbovu. Akasema, "Ondokelee mbali, ewe kilaanifu. Siwe kaisari wetu, illa shetani na

mjaribu." Yoviniano akalia sana, "Ole wangu ! ole wangu ! nitakuwaje bassi ? nikiondoshwa na kasisi mwema. Ah ! nakumbuka sasa. Kwa kiburi changu nalijitaja Muungu. Dhambi hiyo inanilemea sana. Ee baba, baba yangu, sikia khabari za dhambi za mtu maskini mwenyi kutubu." Kasisi akasikia furaha. Alipokwisha kuungama, akamfariji, akamwambia, "Ukitubu kwa moyo, dhambi zako zitasameheka." Marra yule kasisi kama wingu likamwangukia machoni, akaona vema, akamtazamisha sana Yoviniano, akamtambua kama ndiye, akamsikitikia akamvika nguo awezavyo, akafuatana nae hatta mlangoni kwa jumba.

Mnganje mlango amesimama pale. Alipomwona Yoviniano na kasisi, alisujudu, akamfungulia mlango kaisari. Kaisari akamwuliza "Wanifahamu ?" Akajibu, "Kwani nisikufahamu ? Nataka tu hungalitoka nyumbani." Yoviniano akaingia ndani. Alipokipita, wakubwa wote wakamsujudia. Kwani mgeni yule yupo pengine, wakamtambua uso Yoviniano. Basi na mkubwa mmoja akaenda kwa kaisari mgeni, akamwambia, "Ee bwana wangu, pana mtu chumbani pa kulia, wote wanamsujudia, kwani amefanana sana na wewe, hatta hatujui yupi aliye ndiye." Yule mgeni akamwambia malkia, "Nenda wewe, kamtazame huyo." Akaenenda, akarudi akasema, "Bwana wangu, nisemeje ?" Yoviniano mmoja ama watu wawili ?" Akamwambia, "Nitakwenda mwenyewe kuamua." Akamshika mkono, akampeleka chumbani kwa kulia, akamkalisha kitini, akawambia waliopo, "Enyi wakubwa, sikieni. Mmeapa kumtii kaisari. Chagueni basi, mimi ama huyo ?" Malkia akajibu, "Mimi niseme kwanza. Ndio haki. Basi sijui yupi aliye mume na bwana wangu." Wote wakasema vilevile. Basi pale yule mgeni akaondoka akatoa maneno, "Enyi wakubwa, sikilizeni. Huyu

ndiye kaisari na bwana wenu. Msikieni. Alijitukusa mno kuliko haki, akajifanya sawa na Muungu. Na thawabu yake ameipata, ndiyo aibu tele na kudhulumiwa sana, wala hamkuweza kumtambua. Sasa ametubu, akapata masamaha. Amemridhia Bwana, awezavyo. Msikieni, mkumbukeni, mtiini." Akisema haya, akafanya ajabu kuu sana, mavazi ya kifaume yanamwangukia, akaonekana mbele yao wote malaika wa Muungu, amevaa nyeupe. Alipokwisha, akainama kitwa, akatoweka pia. Yoviniano akaingia tena enzini, akawatawala watu kwa huruma na haki miaka mitatu. Ilipokwisha, malaika yuleyule aka-mtokea, akamwonya atakufa karibu. Yoviniano akamwitia karani akamwandikisha khabari zote za maisha yake na taabu yake pia, wote wajue ginsi makuu yasivyofaa, illa kuushika utawa haswa. Alipokwisha akamshukuru Muungu, akalala usingizi, ndio mauti.

---

## 7. GUIDO,

MTUMISHI MWAMINIFU.

PALIKUWA na mfalme mkubwa wa Rumi, jina lake Valerio, nae alitaka killa mtu awae yote amtumikie apendavyo. Basi akatoa amri, mtu ye yote apenda kumtumikia, apige hodi marra tatu mlangoni pa jumba. Palikuwa na maskini katika milki ya mfalme, akasikia khabari ya amri hiyo, akasema moyoni mwake, "Mimi hapa maskini, sitambulikani. Basi ipi heri, kuishi utumwani, ama kufa ungwanani ?" Akaenenda kwa mlango wa mfalme, akapiga hodi marra tatu, akafunguliwa, akaletwa ndani kwa mfalme, akamsujudia. Valerio akamwuliza, "Ee rafiki, wataka nini ?" Akajibu, "Kukutumikia wewe,

ee mfalme." Mfalme akamwambia, "Matumishi gani utakayoyafanya?" Akasema, "Matumishi masita nayaweza. Ya kwanza, kuwa mlinzi, kutengeneza kitanda, kupika chakula, na kungoja chumbani. Ya pili, kukesha watu walalapo, kulala wakeshapo. Ya tatu, kuonja mvinyo na kuchagua ulio mzuri. Ya 'nne, kuita wageni karamuni watakaomfaa mfalme. Ya tano, kuwasha moto ulio moto sana, nao hautoi moshi. Ya sita, kuonyesha njia ya kwenda Yerusalem, waiendeao watafaidi." Mfalme akasema, "Makuu hayo. Bassi uyatende, killa kazi mwaka mmoja. Kwanza, uwe mlinzi."

Guido akawa radhi kumtii mfalme, akafanya kazi ya mlinzi. Killaa siku hutengeneza kitanda, huweka mavazi tayari. Killaa siku hulala mlangoni pa chumba, mwenyi selaha, na mbwa wake mbavuni aliyekesha sana. Killaa jambo humtumikia vema mfalme, hatta mwaka ukaisha. Mfalme akapendezewa sana, akamfanya mkuu wa nyumba na wakili.

Bassi Guido akaingia katika kazi ya pili. Wakati wa neema tele alikusanya vitu vingi, vyote vilivyo-hitajiwa na mfalme, akanunua rahisi, akajaza ghali, akatenda kazi sana. Lakini watu wakamcheka, wakisema, "Neema sana siku hizi. Kazi hiyo yafaa wapi? tujinyoshe tu." Bassi khalafu ikawa njaa, wale watu wakaamka, wakashika kazi, lakini chakula shidda sana, nae Guido hana kazi, raha na mustarehe. Mwaka wa pili ukamwishia, akasifiwa sana.

Tena mwaka wa tatu. Mfalme akamwita mwandikaji akamwambia, "Twae kikombe utie mvinyo mzuri, na siki, na tembo; kamnyweshe Guido, tupate kujua, aonjavyo kinywa ji kitamu, na kuyapambanua yaliyo-changanyika." Mwandikaji akatwaa mvinyo, na siki, na tembo; akazichanganya, akampa Guido, akaonja akasema, "Hakika yake kizuri kilivyokuwa, na kilivyo, na kitakavyokuwa." Mfalme akamwambia,

“ Unitafsirie maneno yako.” Akasema, “ Siki ilikuwa nzuri kwanza, na mvinyo mzuri, na tembo itakuwa nzuri khalafu.” Akajua mfalme kama amechagua vema machanganyiko, asiyoyafahamu kwanza.

Akamwambia, “ Basi nenda kawaite rafiki zangu waje karamuni, kwani siku kuu ya kuzaliwa Bwana ni karibu.” Asiwaite rafiki Guido, kwani hakuenda kuita rafiki illa adui. Mfalme akashukia chumba cha kulia, moyo wake ukafadhaika, akiona adui watupu wako, wala hapana rafiki. Akamwita Guido akamkaripia vikali, “ Ewe mbaya, hukusema, wajua kuchagua wageni wangu ?” Akajibu, “ Nimesema.” “ Sikugiza, uwaite rafiki, kumbe umewaita adui ?” Guido akamwambia, “ Nina neno moja, bwana.” Akamwambia, “ Nena bass.” Mtumishi akasema, “ Ee bwana wangu, hapana wakati rafiki zako wasioweza kuja kukuamkia, na kukaribishwa vizuri na kwa heshima, lakini adui sivyo. Nikasema rohoni mwangu, “ Hatta adui wakitendewa mema na mazuri watageuka kuwa rafiki.”

Ndivyo ilivyokuwa. Karamu ikasitawi ikaisha, nae mfalme amepatana na adui, wakafanya urafiki kwa maisha pia. Basi mfalme akamwita Guido, akamwambia, “ Kwa msaada wa Muungu Mwenyezezi, shauri lako limefanikiwa. Haya basi utuwashie mimi na adui zangu walio rafiki moto usio na moshi. Akajibu Guido, “ Kama ulivyoamuru, ndivyo itakavyofanyika.” Akatuma watu, akakusanya kuni tele mbichi, akaanika juani, hatta zikaisha kukauka pia, akafanya moto, na ule moto moto sana, lakini moshi hamna. Wakafurahiwa sana mfalme na wageni.

Bassi mfalme alipoona ya kwamba kazi tano zime-mtimilia vizuri Guido, alimwamuru atimize nayo ya sita, apate heshima bora sana katika milki yake. Guido akamwambia, “ Ee bwana wangu, atakae jua njia ya kwenda Yerusalem, aje kwangu pwani.”

Mfalme akapiga mbiu, watu wakaja wengi wengi, waume kwa wake, wakajaa sana pwani. Basi walipokusanyika, Guido akawambia, "Enyi jamaa, mwaona kule baharini niyaonayo niimi?" Wakajibu, "Hatujui." "Bassi mwaona mwamba mwembamba umesimama mawimbini?" Watu wakamwambia, "Uko. Basi nini?" Guido akasema, "Jueni nyote, ya kwamba juu ya mwamba ule akaa ndege, akaae dayima tunduni mwake, namo humo tunduni mayai saba. Killa akaapo ndege, bahari ni shwari tupu, watu huenda huko na huko katika vilindi salama. Killa aondokapo, pepo zavuma, mawimbi yachafuka, wengi hutoswa majini." Watu wakasema, "Tujue wapi, ndege aondokapo tunduni?" Akajibu Guido, "Huyo akaa siku zote, isipokuwa jambo baya lime-mpata. Aondokapo, marra huja ndege mwingine mkubwa na hodari, hutia uchafu tunduni mwake, huvunja mayai yake saba. Basi yule ndege akiona akimbia mbali, pepo na dhoruba zacheza. Ndipo wana maji hawana buddi kukaa bandarini." Watu wakamwambia, "Bwana, tufanyeni, mambo haya yasiwe, tukamlinde ndege na tundu katika adui?" Akasema Guido, "Damu yake mwana kondoo ndiyo imchukizayo sana adui, wala hawezi kuja ilipo. Basi twaeni hiyo damu, mwinyunyize tunduni ndani na nje. Hatta tone moja likiwapo, yule ndege mzuri atakaa raha, wala mawimbi hayachafuki, pote salama tu baharini." Wakafanya. Wakatwaa damu ya mwana kondoo, wakainyunyiza juu ya tundu na mwamba pia.

Mfalme na watu wake wakapita kwenda Yerusalem, wakawasili, wakarudi kwao salama salimini. Mfalme akamfanyia Guido, alivyomwahidia, akampasha mtumishi mwaminifu utajiri mwingi, akamtu-kuza kwa heshima kuu juu ya watu.

## 8. MFALME NA MLAIFI.

PALIKUWA na mfalme wa Rumi, nae huwaonea huruma sana walio vipofu, hatta akatoa amri, killa mtu wake aliye kipofu apewe reale asharini katika hazina ya mfalme. Bassi pale Rumi kulikuwa chama ya watu walioharibika akili, kazi yao kukaa anasani, kula kunywa kufanya jeuri tu bass. Nao wamekaa siku saba katika nyumba wakinywa wakilewa, hatta mwenyewe nyumba akataka kulipwa fedha yake. Killi mtu akatafuta mapesa aliyofutika, mapesa hayatosh. Mwenyewe akawambia, "Bado reale ashari-ni." Wakasema, "Tufanyeni?" Fedha nyingi hiyo. Hatta mmoja alikumbuka amri ya mfalme, akasema, "Sikilizeni. Mfalme hatoi reale asharini kwa killa kipofu?" Akamwambia, "Hutoa kweli. Basi nini? sisi vipofu?" Kijana akawambia, "Basi nini? Tuchague kwa kura, nani atakaetiwa upofu, tumng'oe macho, tukampeleke kwa mfalme, tutapata reale asharini." Wakasema, "Vema." Wakapiga kura, kura ikampata yule aliyetoa shauri. Wenziwe wakamtwa, wakamng'oa macho, wakampeleka jumbani kwa mfalme. Wakabisha hodi, mngoje mlango aka-fungua, akawauliza, "Mwataka nini?" Wakamwambia, "Huna macho? tazama, si huyu mwenzetu kipofu? ataka ada ya mfalme." Nae mngoje mlango alimjua kijana zamani, akasema, "Amekuwaje kipofu gháfula hiyo? Haidhuru, ntamwita karani." Akaja karani mlangoni, akamtazamisha kijana, akamwambia, "Watakani?" Kijana akajibu, "Nataka reale asharini wapewazo vipofu na mfalme." Karani akasema, "Ginsi gani kuwa kipofu marra hiyo? Ilikuwaje? Nalikuona mwenyi macho mazima jana mjini katika duka la mvinyo." Kipofu akasema, "Ah!"

bwana, pale pale dukani usiku leo nimekuwa kipofu." Karani akamwambia, "Kamleteni mwenyewe, tupate kujua khabari." Wakamleta, akamwuliza khabari akasikia yote yalivyokuwa, akamwambia kijana, "Hakika yako huijui amri illa nussu tu, nayo si vema. Vipofu wa Muungu ndio hupewa ada na mfalme. Lakini wewe ulipataje kuwa kipofu? Umekubali kung'olewa macho, upate fedha ya kulipa deni ya ulafi na asharati. Basi umestahili kupewa kitu? Ondoka, ee mjinga! choyo tu kilichokupovusha." Wakawafukuza vijana, wakaenda zao wakajuta majuto makuu.

---

## 9. MTAWA NA MALAIKA.

PALIKUWA mtu nae mtawa sana. Akaondoka aka-sema, "Mimi hapa sitaki neno illa moja tu, ndilo kumwabudu Muungu Mwenyezezi. Basi niwezeje hapa mjini nikizungumza na watu walio wabaya? Nitakwenda kukaa peke yangu mbali." Akaenda akaona mahali palipo ukiwa, watu hapana, akachimba shimo, akakaa.

Akaja mchungaji masikini, akichunga kondoo wa bwana wake pale nyikani, kwani pana majani tele. Siku moja yule mchungaji akalala usingizi, kwani amechoka sana kazi, akaja mwivi akamnyang'anya kondoo. Alipoamka aliona kondoo hapana, akasema, "Mwivi aliywachukua." Akaenda kwa bwana, aka-mwambia, "Mwivi amewanyang'anya kondoo zako." Bwana akasema, "Sivyo, umewapoteza wee." Aka-amuru asikari wamwue mchungaji, wakamwua. Yule mtawa akalijua jambo, akasema rohoni mwake, "Ee Muungu Mwenyi rehema, umeyaona haya? aliyekosa mtu mgine, aliyeuawa mtu mgine, nawe huangalii

mbona ? Basi bora kufanya mabaya. Niende nilipo-kuwa kwanza, nikafanye wafanyakyo wana Adamu wote." Akaliacha shimo akafanya safari kurudi mjini, malaika akamkuta njiani, umbo lake kama mtu msafiri, akamsalimu, akamwuliza khabari, "Waendapi rafiki ?" Akajibu, "Nakwenda kule mjini." Akamwambia, "Na mimi nakwenda. Mimi malaika, Muungu amenituma kufuatana nawe."

Wakaenda wote pamoja, wakafika mjini, wakaenda nyumbani kwa akida mmoja, wakamsihi awakaribishe wakae usiku. Akakubali kwa furaha, akawaheshimu sana wale wageni, akawapa chakula kizuri. Yule akida ana mtoto mmoja mchanga, aliyempenda sana. Wakala wakaisha, akida akawapa pazuri pa kulala, wakalala wote wawili, malaika na mtawa. Hatta usiku wa manane mtawa akaamka, akamwona malai-ka aliondoka kitandani akaingia chumbani alipolala mtoto, akamsonga. Yule mtawa akasema kwa moyo wake, "Siye malaika huyo. Akida ametukaribisha vizuri vizuri awezavyo, nae mgeni wake amemwulia mtoto wake pekee." Hakuthubutu lakini kumshtaki malaika.

Wakaondoka assubuhi, wakaenda hatta mji wa pili, tajiri mmoja akawakaribisha nyumbani. Tajiri akawa na kikombe cha dhahabu cha thamani nyingi sana. Basi usiku malaika akakiiba kikombe. Mtawa asithubutu kumkemea, kwani aliogopa.

Wakaondoka assubuhi, wakashika njia, wakafika kwenyi mto, na juu ya mto daraja ya kuvukia watu. Wakapita juu ya daraja, wakamkuta masikini mzee. Malaika akamwambia mzee, "Ee baba, tuonyeshe njia ya kwenda mjini kule." Mzee akageuka kumwonyesha njia, marra malaika akamkamata mzee kwa nguvu, akamtupa mtoni, akazama majini. Mtawa akashtuka sana, akasema moyoni, "Ole wangu ! ole wangu ! siye huyo shetani ? mzee alikosa

nini? hakuwa na hatia, wala hakustahili." Asitoe neno lakini, kwani hofu imemwingia.

Basi jioni wakafika mji mwingine, wakatafuta mahali pa kulala usiku. Wasipate, kwani mwenyewe nyumba aliwafukuza vikali. Nae malaika akimsihi sana, "Usitutupe nje, mbwa wa mwitu na wanyama wakali watatukamata." Akamwambia, "Basi pale tundu la nguruwe. Laleni humo. Hapana pengine." Malaika akasema, "Ah bwana, tutalala. Basi je? hatuna buddi." Kesho assubuhi malaika akamwita mwenyewe, akamwambia, "Rafiki, nakupa kikombe hiki, ndio ada." Akamtolea kile kikombe alichokiiba kwanza. Mtawa akasema, "Sasa nimemjua yakini siye malaika. Hulipa mabaya kwa mema, na mema, kwa mabaya. Basi siwezi kusafiri pamoja nawe. Tuagane. Kuaheri." Akataka kwenda zake. Malaika akamwambia, "Ee rafiki yangu, nisikilize kwanza. Ulipokikaa kule nyikani, bwana wa shamba alimwua mtumishi wake, aliye amini, si kwa haki. Nae mtumishi asiyekosa amestahili kuingia peponi. Angaliishi, angalitenda dhambi ya kufa asitubu. Nae aliyewaiba kondoo atapata adhabu ya milele. Nae bwana wa kondoo hakujuua vema. Basi atubu akafanye iliyo haki. Tena, asikari aliyetukaribisha vizuri; akampendelea mno mtoto wake, akaacha kutoa sadaka na kuwahurumia masikini, kwani? apate kumwekea mtoto akiba kubwa. Hivyo akafanya choyo sana. Sasa amefiwa, atakuwa mwema na mtawa na mtoa sadaka. Na mwenye nyumba niliywiblia kikombe; alikuwa kwanza mtu wa kiasi sana, akakipata kikombe, marra tamaa ikamwingia ya kunywa mno kulewa. Nikakitwaa, amekuwa mwenyi kiasi tena. Tena, mzee niliyemtumbukiza mtoni; nae pia mcha Muungu sana. Kama angalindelea, angalitenda dhambi kuu. Sasa ameokoka, ametukuka peponi. Wala sikumpa yule mkorofi

aliyetufukuza kikombe billa sababu ; kwani mbaya sana, alitulaza penyi nguruwe. Na thawabu yake ameipata, kile kikombe, kwani kitamvuta kwa mabaya, ndio anasa na ulevi. Basi, rafiki, jilinde midomo, wala usimnenee vibaya Muungu Mwenyeze, kwani ndiye ajuae yote." Mtawa akamsujudia malaika, akataka samehewa. Akapata, akarudi pale shimoni akakaa.

---

## 10. FULJENTIO.

PALIKUWA mfalme wa Rumi, jina lake Martini, na mjomba wake ndiye mkuu wa jumba, jina lake Malitio. Tena kijana aliye mwana wa ndugu yake mfalme, alifiwa na wazazi wake, yeze alimngojea mfalme siku zote, na kumwandikia mezani, na kute-ngeneza kitanda. Kwani Martini alimpenda sana yule kijana, akamtendea mema, kama mtoto wake mwenyewe, kwani mfalme hakuwa na mtoto. Na Malitio alimchukia sana huyo Fuljentio, ndilo jina lake kijana ; sababu yeze akipata kuurithi ufalme, mtoto wake Malitio haupati, haki yake itampotea. Basi Malitio kazi yake siku zote, mchana na usiku, kutafuta shauri la kumtia hatiani kijana, mfalme aliyempendelea.

Basi siku moja akaondoka akamjia mfalme, kama mwenyi uchungu mwingi na huzuni ; akamwambia, "Ee bwana wangu, sipendi mimi katta kidogo kuchongea watu, wallakini sina buddi kumwonya mfalme neno limpunguzialo mfalme heshima yake." Mfalme akamwambia, "Nena bass." Malitio akajifanya anasitasita kwanza, akamwambia, "Neno hili ndilo siri. Bwana wangu asilitoe wazi, tulijue wawili, wewe na mimi tu bass." Mfalme akamwa-

mbia, "Upendavyo." Basi yule akaanza maneno yake, "Ee bwana wangu, ulimwengu huu hauna shukrani kabisa." Mfalme akasema, "Labuda ndivyo. Usinikawilishe tu. Toa siri yako, juu linachomoza, nataka kwenda kuwinda." "Yule kijana, Fuljentio!" "Fuljentio? ana nini?" "Ee bwana, kijana yule mbaya sana, kazi yake kukunenea vibaya kwa wenzake, asema dasturi zako si njema, na pumuzi yako ina harufu ya kumfisha mtu, hatta hawezi kukungojea tena." Mfalme akamwambia, "Maneno hayo ya kweli?" Akamwambia, "Ee bwana, angalia tu. Yule kijana akikuletea kikombe, akikengeua uso akaribiapo, ndio maana, ataka kukusingizia na kuwasadikisha wengine kama ndivyo asemavyo." Mfalme akajibu, "Vema; nenda, rafiki, nimesikia inaneno yako." Marra yule Malitio alimwendea kijana, akamtolea maneno mazuri ya kwamba anampenda sana, tena kwa upendo wake kuwa mwingi ataka kumwonya neno moja, asipate kumchukiza mfalme na kuupoteza urithi wake. Akamchekelea kwa upole akamwambia, "Ee ndugu, pumuzi yako yamtia chuki sana mfalme, hatta amesema ataka kukutoa katika kumngoea." Kijana akasema, "Ee bwana, ndiyo kweli?" "Hapana shaka ndiyo. Hatta mimi nalikuwa hali hiyo hiyo zamani, lakini ugonjwa, haikukaa sana, itakwenda zake." "Lakini hatta siku moja yatosha kumtia mfalme machukizo. Nifanyeje basi?" Akajibu Malitio, "Nadhani hili ndilo shauri jema. Ukimletea mfalme kikombe, pindua uso kidogo. Hatasumbuka na pumuzi yako, tena ataangalia umefanya bidii ya kumpendeza." "Ahsante sana, Malitio, shauri lako limenifurahisha mno." Malitio akaenda zake, akisema, "Potelea mbali na furaha yako."

Siku ile ile Fuljentio alimletea mfalme kikombe mezani; alipokimletea kikombe alinyosha sana mko-

no, akajizungua kitwa, asipate kumsumbuia mfalme. Mfalme akaona ghathabu akampiga konde la kifua, akamwambia, "Ewe mbaya! najua sasa ndiyo kweli niliyosikia khabari yako. Ondoka, nenda mbali. Nalidbani nitakufanya mfalme. Sasa tusionane tena siku zote." Yule kijana akilia sana, akitoka mezani akichekwa na kushutumiwa na wote waliopo. Kwani ametupwa, basi hatambulikani tena. Mfalme aka-mwambia Malitio, "Mtoto wako aingie katika kazi ya huyo, asiye na shukrani. Haya unishauri tena njia ya kumwondolea kijana, aliyenitia aibu mbele ya watu wote." Akamwambia, "Hili ndilo shauri langu. Kuna watumwa wako wanachoma chokaa mwituni kule katika tanuu kubwa kubwa. Utume intu leo usiku kuwaamuru, mtu wa kwanza atakaewajia kesho assubuhi, akiwambia: Mmefanya alivyoamuru bwana? marra wamtupe motoni ndani ya tanuu. Tena mwite Fuljentio, kamwambie aende zake mapema assubuhi kwao wachoma chokaa na kuwambia: Mniefanya alivyoamuru bwana? Marra watamtupa motoni, ndio mwisho wa mazungumzo yake mabaya."

Mfalme akafurahi, akamwita Fuljentio akamwamu afikie tanuuni jua likichomoza. Tena akatuma mtu kwa frasi kuwambia wachoma chokaa, mtu wa kwanza atakaewauliza kesho khabari, kama wamefanya walivyoamriwa, wamchome motoni.

Basi usiku ule Fuljentio hakulala, akaondoka na mapema, haijacha assubuhi, akaenda kufanya amri ya mfalme upesi, akadhani labuda akitenda mema atakubalika, atapata kupendelewa vile vile. Alipokiwasili hatta mwitu walimokaa wachoma chokaa, akasikia kengele inalia, akajua ndiyo kengele ya kikanisa inakwita watu kuja kusali. Kengele ile ikamkuliza roho, kwani ameona huzuni nydingi, marra akaingia kanisani akamtolea Muungu sala na mashu-

kuru. Kisha kusali, akijiona amechoka sana akataka kupumzika kidogo, akakaa ukumbini mwa kanisa kidogo, khalafu akalala. Kasisi akatokea ukumbini, akamrehemia akisema, "Ee mwanangu naona umechoka na huzuni." Lala tu, hapana atakaekuamsha." Akalala hatta mshuko wa alasiri, akaamka.

Sasa tumrudie Malitio kidogo. Nae hakulala usiku ule, moyo wake unakesha sana kwa kumfikiria kijana atakuwaje, kufa au kuishi. Akafadhaika sana kwa fikara zake. Hatta adhdhuhuri hawezi kustahamili tena, akaondoka akaenda mbio hatta mwituni ; alipofika akawauliza wachoma chokaa, "Mmefanya bwana alivyoamuru ?" Wakamtolea ukali wakasema, "Bado, bwana, bado. Lakini haidhuru. Marra tutafanya." Wakamkamata, wakamkokota tanuuni. Malitio akalamika sana, "Haifai, bwana, mniache. Mimi siye, illa Fuljentio. Acha basi ! acha !" Wakanmcheka sana, "Sisi hatukutambui wala wewe wala Fuljentio. Ndiwe wa kwanza aliyetufikia leo hivi, na kuuliza : Mmefanya bwana alivyoamuru ? Basi tena, basi ! haya, jamani ! Tupeni." Wakamtupa motoni, akafa.

Ikawa alasiri, ndipo Fuljentio akaamka, na juu likishuka. Akasema, "Ah ! nimechelewa sana kuttenda bwana alivyoamuru." Akaenda mbio mwituni, akawasili hatta tanuu. Msimamizi wao wachoma chokaa akamwambia, "Ewe mtoto, wataka nini ?" Akamsihi sana, "Ee bwana, mmefanya bwana alivyoamuru ?" "Tumefanya sana tena. Haya njoo, tupa jicho mle tanuuni, kamwone, mifupa yake inaungua hatta sasa." Fuljentio akastuka akatemeka kwa khofu, "Mifupa yake ? mifupa gani ?" Wakampasha khabari za zote walizoamuriwa, na kama aliyetangulia kuja ndiye Malitio, akachomwa. Hatta Fuljentio akapiga magoti palepale akamshukuru Muungu, kwa sababu ameo'oka i a kufa kubaya

sana. Akaagana nao wachoma chokaa, akarudi kwa jumba la mfalme. Akaingia akainama mbele ya kitu chake akasujudu. Mfalme akamwambia, "Ee mtoto, umejia nini ? hukuwaendea wachoma chokaa ?" Akamwambia, "Nimekwenda, nikafanya ulivyoamuru, lakini kabla sijafika mimi, amri yako imekwisha kutimia." Mfalme akasema, "Kutimia imetimiaje nawe ? Malitio yuko wapi ?" "Ah ! bwana wangu, amechomwa tanuuni, alifika wa kwanza, wachoma chokaa wakafanya ulivyoamuru, amekufa, nami ni meokoka. Ee bwana, kwa nini ultaka kuniua mimi vile vibaya, mimi mtoto wako masikini ?" Wakazungumza, hatta hila ya Malitio ikafahamika. Mfalme akamwinua mtoto, akamfanya mtoto wake na mrithi milki, akamshukuru Muungu, kwani ameokoa maisha yake asiye na hatia, akamwua aliye mbaya.

---

## 11. SEMIRAMISI.

SULTANI Nino akamwambia Semiramisi, "Katika wanawake wote nilio nao ndiwe nikupendae sana. Hapana mwenyi neema na uzuri mwingi kama wewe, kwa ajili yako napenda kuwaacha wengineo wote pia." Akajibu, "Sultani ayaangalie vema maneno yake. Labda mimi nkipenda kujuu kama ndiyo kweli, je ?" Akamwambia, "Haidhuru. Nikipendwa na wewe, sitaki wengine hatta mmoja." Akamwambia, "Basi kama nikitaka mimi, utawaondolea mbali wanawake wengine ulio nao, na kunipenda mimi peke yangu ? na kunisharikisha katika enzi na ufalme, hatta kuwa malkia wa Ashur ?" Sultani akamwambia, "Lakini hatta sasa si wewe malkia wa Ashur ? kwani mimi sultani wake, na wewe unitawalee mimi, kwa maana ya uzuri wako." "Sivyo,

Bwana, sivyo. Mimi kijakazi tu unaempenda. Sita-wali, napendeza tu. Nikitoa amri, kwako shauri la kuifkiliza ama kuitangua.” “Basi waona kutawala ndio kitu bora?” “Naona, lakini sijajaribia.” “Wataka tena kujaribia? Wapenda kutawala siku mbili tatu mahali pangu?” “Angalia, ee mfalme! Usikarimie nyingi mno.” “Haidhuru. Nasema, wataka kutawala siku moja nzima mchana kutwa peke yako? kama ukipenda nakubali mimi.” “Basi na amri zangu zo zote zitatimizwa?” “Zitatimizwa, nakutolea siku moja, mchana kutwa, mamlaka yangu, na fimbo ya dhahabu, ndio ishara ya enzi kuu.” “Itakuwa lini basi?” “Ukipenda, kesho.” “Napenda.” Semiramisi akainama kitwa begani kwa sultani, kama akitaka masameha ya haja yake ali-yomtaka.

Assubuhi ya pili, Semiramisi akawaita wajakazi wake, wakamvika vizurivizuri mno. Alivaa kitwani taji ya vito vya tunu, kisha akamtokea Nino. Nae akashangilia alivyo mzuri na sura na mavazi, aka-waamuru wakubwa wote wa jumbani kukutanika pamoja penyi baraza, na fimbo ya dhahabu iletwe. Akaingia barazani, akimshika mkono Semiramisi. Wakasujudu wote mbele ya sultani, akampeleka Semiramisi kitini kwake akamketisha huko. Akawambia wote walioko, “Simameni.” Wakasimama. Tena akawaamuru wote siku ile mchana kutwa wamtii Semiramisi kama sultani mwenyewe. Tena akaitwaa fimbo ya dhahabu, akaiweka mkononi mwa Semiramisi, akasema, “Ewe malkiya, nakuwekea mkononi iliyo ishara ya enzi kuu. Uipokee, uwe na uwezo juu ya ufalme wote. Hao wote waliopo watumwa wako, na mimi pia mtumwa wako wa leo hivi mchana kutwa. Asiyekutii kwa bidii, aadhibishwe vilevile kama kwamba amwasi mfalme.” Ali-pokwisha kunena, sultani akamsujudia Semiramisi,

nae akamchekelea akatoa mkono aubusu. Tena wakubwa wote wakapita taratibu, killa mtu akatoa kiapo ya kuwa atamtii Semiramisi kwa yote aamu ruyo. Wakaisha, sultani akamsalimu malkiya, akamwambia, "Ndiyo ajabu, ulivyo kama malkiya thabiti halisi, na sura, na umbo, na mwenendo pia." Semiramisi akajibu, "Kwani nalikuwa nikifikiri, amri gani za leo nitakazowaamrisha watu wangu. Sina illa siku moja tu ya kutawala. Sharti niitumie vema." Sultani akacheka, akazidi kupendezewa nae; akamwambia, "Haya, endelea. Amri zipi uzitoazo?" Semiramisi akasema kwa sauti kuu, "Mwite karani wa sultani." Akaja karani, watumwa wawili wakaleta meza ya kuandikia akaiweka mbele yake. Semiramisi akasema, "Mwandikie barua mkuu wa ngome ya Babel: Hii ndiyo amri ya malkia: Mtu akuleteae barua hii, umtolee marra moja ukuu wako wote na kazi. Asipotoa, auawe. Twaa khati, kunja, tia muhuri yake sultani, unipe. Tena mwandikie barua mkuu wa utumwa wote wa jumbani: Hii ndiyo amri ya malkia: Mtu akuleteae barua hii, umtolee marra moja ukuu wako wote na kazi pia. Asipotoa, auawe. Twaa khati, kunja, tia muhuri, unipe." Wakubwa wote wakashtuka kwa khofu nydingi, hatta na sultani mwenyewe aka shangaa. Semiramisi akasema, "Sikilizeni. Saa a tatu wakubwa wote waje kuniletea zawadi, kwa dasturi ya masultani wakianza kumiliki. Tena jioni fanyeni karamu ya siku kuu. Basi ondokeni, illa mtumwa wangu amini Nino tu, akae. Nataka kumshauri kwa mambo ya ufalme." Wote wakaondoka, Semiramisi akamwambia mfalme, "Basi waonaje?"

Nimejua kuwa malkia ama siyo?" Akamwambia, "Hakika yako umejua, hatta kunistaajabisha tena. Lakini neno moja, kunradhi ukamwambie mtumwa wako, sababu ya zile khati je? wafanyaje nazo?" Akamwambia, "Nikiwa malkia, mbona wanitakia sababu? Lakini haidhuru. Kusudi langu, ndio nataka kuwalipiza kisasi wale wakuu watatu, juu yao nimetoa amri." "Kisasi gani tena?" "Yule wa kwanza, mkuu wa ngome; mwenyi chongo, killa nimkutapo hunitia khofu. Wa pili, mkuu wa utumwa; namchukia, huniambia: Ntaleta wanawake wengine wa kumpendeza sultani. Wa tatu, mkuu wa jeshi; hukushughulisha sana huko kwake kituoni pa asikari, nami napenda ukae hapa kwangu. Namwonea vivu." Jibu hilo jerevu sana na lenyi kumsifu likamchekesha sana sultani, akasema, "Vema sana. Sababu njema hizo za kuwaondosha walio wakubwa katika ufalme."

Khalafu wakaja wakubwa **kumletea** zawadi malkiya, wengine johari, na vitu vya tunu; walio wadogo maua, na matunda; nao watumwa hawana kitu, wamsujudia tu. Katika wale watumwa palikuwa na ndugu watatu, waliotoka katika inchi Kaukaso pamoja na Semiramisi alipochukuliwa utumwani, ikawa khatari njiani, ndio chui, wale ndugu wakamwokoa. Basi walipopita mbele yake Semiramisi akawambia, "Hamna zawadi za kumletea malkiya?" Wa kwanza, jina lake Zopire, akajibu, "Sina kitu, illa maisha yangu, nimlinde nayo." Nae wa pili, jina lake Artabani, "Sina kitu illa upanga juu ya adui zake." Wa tatu, jina lake Assar, "Sina kitu, illa kumheshimu alivyestahili." Semiramisi akawambia, "Enyi watumwa, ndinyi mlioniletea zawadi zilizo bora, nami nawaonea shukrani nyingi. Wewe mwenyi upanga, twaa khati hii, kumpelekee mkuu wa jeshi la asikari wa sultani, kampe. Utapata

faida nayo. Mwenyi kutoa maisha yako kwa ajili yangu, twaa khati hii, umpelekee mkuu wa ngome. Utapata faida nayo. Mwenyi kunireshimu nistahilivyo, twaa khati hii, umpe mkuu wa utumwa wa jumbani. Utapata faida nayo." Na kwa sababu alikuwa mzuri mno yule mwanamke, akafanya yote kwa kicheko na taratibu, Nino hakukasirika, alifurahiwa tu. Khalafu malkia akaamuru akatwe kitwa mtumwa mmoja aliyesita kidogo akitenda kazi yake, Nino akazidi kucheka akazungumza sana na Semiramisi, hatta jioni. Basi jioni wakafanya karamu, malkia akaingia chumbani kwa kulia, marra akaletewa kitwa cha mtumwa aliyekatwa kitwa, akakitazamisha akasema, "Ndio njema. Basi kiweke wazi katika behewa ya jumba, wote wapate kukiona, nawe ukae pale ukatangaze; Mtu mwenyi kitwa hiki alikuwa mzima saa tissa, tena hakumtii malkia, akaondolewa kitwa. Ndiyo khabari."

Karamu ikawa nzuri mno, vyakula vingi vitamu na vya thamani, wote wakamsujudia malkiya aka-wakaribisha kwa heshima sana, marra kwa marra azungumza na Nino, akamfanya heshima nyngi sana kupita wote, akasema, "Wewe mgeni wangu, Sultani, basi sina buddi kukupendeza niwezavyo." Wakala wote. Walipoanza kula, Semiramisi aliwachanganya sana wageni akawabadilishia mahali. Na Nino alimweka chini yao wageni wote. Nae kucheklea tu, wote wakakubali kukaa apendapo mwe nyewe malkia, wakisema, "Sultani amekubali, basi sisi tukatae?" Semiramisi akawaita wale ndugu watatu, watumwa waliotoka Kaukaso, akawaketisha. mbavuni pake, akawauliza, "Mmefanya nilivyoamuru?" Wakajibu, "Tumefanya." Karamu ikasitawi sana. Palikuwa na mtumwa, nae kwa dasturi ya siku zote alimpakulia sultani kwanza, kwani ndiyo heshima yake. Marra Semiramisi akaamuru

apigwe bakora. Akalia sana, wageni wakamcheka. Killa mtu akawa na furaha. Wakala wakaisha, wakaletewa kahawa, wakaisha. Ndipo malkiya akao-ndoka, akawambia, "Enyi wakubwa, karani amenipa hesabu ya watu wote walioniletea zawadi leo assubuhi kwa siku kuu yangu ya kuanza kutawala. Mkubwa mmoja tu asiyeniletea hatta kitu." Marra Nino akalia, "Nani huyo? Mwathibishe sana." Aka-sema, "Wewe ndiye, bwana wangu. Umemletea malkiya nini leo?" Nino akaondoka, akaja kwa kicheko, akanena neno moja masikioni kwa mal-kiya. Marra malkiya akapaliza sauti akinena, "Nimeaibishwa nae mtumwa wangu." Sultani aka-piga magoti akinena, "Nakuomba unisamehe, malkia wangu, kunradhi ukonisamehe." Akasema, "Na-taka karamu hii iishe." Semiramisi akamwambia, "Wataka nitoke katika kutawala? usiwe haraka lakini, saa mbili zipo tena za kutawala." Mfalme akambusu mkono, nae hakubali, akamsukumia mbali, akasena, "Ameniaibisha, nae mtumwa, sikubali. Ee mtumwa! bado kidogo tu, utakufa." Nae Nino yuko amepiga magoti, akamwambia malkia, "Ee bibi! mapumbavu hayo; haidhuru, uwezo wako utakwisha marra." Malkia akainama kidogo, akamwambia kwa faragha, "Usikasirike, basi, kama mimi nikitoa amri moja." Akaseina, "Sikasiriki." Semiramisi akasema kwa sauti kuu, "Enyi watumwa, mkamateni huyo, mka-mateni Nino." Nae akicheka tu, akafungwa na watumwa. "Mtoeni nje, mpelekeni behewani mwa jumba, fanyeni tayari kumwua, mkangojeni." Wa-kamchukua nje, nae akicheka vile vile, hatta behewani, napo kitwa kipo cha mtumwa aliyeasi. Semiramisi akatokea darini juu. Nae Nino amefungwa mikono nyuma. Malkia akawambia wale ndugu watatu, "Nenda upesi, wewe Zopire, ngomeni; na wewe, Artabani, kituoni kwa asikari; na wewe Assar, fu-

ngeni sana malango ya jumba yote." Wakasikia, wakafanya alivyosema. Nino akamwambia Semiramisi, " Mchezo huo mzuri mno, neno moja nataka, uishe upesi." Semiramisi akamwambia, " Basi, ume-kwisha. Enyi watumwa, mkumbukeni aliyeasi. Pigeni." Wakapiga. Nino asidiriki kutoa hatta kilio kimoja, kitwa kikaanguka chini, chenyi kucheklelea vilevile. Semiramisi akasema, " Basi mimi hapa nitawalae, malkiya wa Asshur. Mtu asiyenitii, auawe kama yule mtumwa, kama Nino."

---

## 12. SANAMU TATU.

**PALIKUWA** mfalme wa Rumi, jina lake Leo, nae hupenda sana kutazamatazama nyuso za watu wazuri, ndio furaha yake. Hatta akafanya sanamu tatu za mawe zenyi nyuso zilizo nzuri inno, akaziweka hekaluni, watu wote wapate kuzitazamisha na kubudu. Na sanamu hizo, moja imesimama yenyi mkono umenyoka mbele, na katika kidole pete ya dhahabu ilioandikiwa, " Kidole changu ki karimu." Ya pili ikawa na ndevu ya dhahabu iliyofuliwa, na juu ya paji la uso imeandikwa, " Nina ndevu mimi. Asiye na ndevu aje kwangu, nitampa." Nayya tatu imevaliwa joho la dhahabu na kisibao chekundu, ika-andikwa kifuani, " Siogopi hatta mtu." Tena zisipate kuibiwa mali, mfalme akatoa amri, mtu aibae pete, ama ndevu, ama joho, auawe.

Marra akaja mwivi akaziiba. Na huyo mwivi, alikuwa mwalimu kwanza, akili zake nyingi zikampotea, hatta akafanya mambo mengi ya asharati ; killa alicho nacho kikampotea, akakaa mtu wa kuomba tu. Akaondoka, akaziiba zile mali, watu wakamgundua, wakamkamata wakamchukua kwa mfalme ; waka-

mwambia mfalme, "Huyu aliyeunja amri yako." Nae mwizi akamwambia, "Ee bwana wangu, nataka ruksha ya kunena maneno yangu." Mfalme aka-mwambia, "Nena bass." Akamwambia, "Nilipoingia hekaluni, kumbe sanamu imeninyoshea kidole, kama ikitaka kusema ; Twaa pete. Nami nikasita kidogo, hatta nikasoma ilivyoandikwa ; Kidole changu ki karimu. Basi nikajua kama ndiyo itakayo kidole chenyewe, kunipa pete. Basi je? nisitwae? nalitwaa. Nikaenda penyi sanamu ya pili, nikasema moyoni mwangu ; Fundi aliye fanyiza ndevu hizi hakika hana ndevu. Basi kiumbe kimshinde : aliye wumba ? hasha ! Nikaona haya lakini kwanza, hatta nikasoma ; Asiye na ndevu, aje kwangu, nitampa. Basi kukataa wapi, nikipewa na sanamu ? Tena joho la dhahabu, kulitwaa ndio rehema tu, kwani mawe yana baridi, na dhahabu ni baridi, na sanamu ndiyo ya mawe, nalo joho dhahabu. Bassi siku za baridi ndio kuzidisha baridi, na siku za juu kali, joho zito litafaa wapi ? hatta hivi ningeona mashaka, kama nisingetazama maneno yake ; Siogopi hatta mtu. Kiburi gani hicho ? Nay o sanamu tu. Nikasema : Heri niirudi kidogo yenyi kujisifu mno, nikalichukua joho." Asifaidie mwizi kwa maneno yake mengi. Mfalme aka-mwambia, "Ee rafiki ! husikii amri ikitsema ; Aibae auawe ? Nawe umeiba. Basi uuawe." Akauawa. Ndio mwisho.

### 13. EUSTASIO.

ZAMANI za Trajano, mfalme wa Rumi, aliondokea mtu, jina lake Plakido, nae shujaa na hodari kwa vita, na mkuu wa majeshi yote ya Warumi. Tena nwema sana, mwenyi rehema na haki, lakini kafiri, alitweza Wamasihiya. Na mkewe pia mwema, mzuri,

nae kafiri. Na watoto wake wawili wote waume, wamelelewa vema sana, nao makafiri. Siku moja katika siku Plakido akataka kuwinda, akawaita rafiki na wafuasi, wakaenda wote na mbwa pia, wa-kaona kundi la paa wengi, wakawinda sana. Na paa mmoja mrefu sana na mwenyi pembe kubwakubwa, akawaacha wenzake, akakimbia vichakani mwa mwitu peke yake. Basi wale wengine wakawafuata paa wale wengi, illa Plakido akashika kumwinda paa huyo mmoja. Akaenda akaenda, mwitu na nyika, akamkaribia sana paa, asiweze kumpatia kwa mkuki. Akafika penyi kilima, paa akachoka sana, akasimama akazunguka uso, naye Plakido ataka kumpiga, marra akaona kati ya pembe zake paa, msalaba unang'aa sana mweupe mno, hawezi kumpiga, asimama kwa ushangao, sauti ikamwambia kama ikitoka katika paa, "Ee Plakido, mbona wanifukuza ? Kwa ajili yako nimejigeuza hivi. Ndimi Masiya, unaemwabudu kwa moyo usipotambua. Sadaka zako na sala zimenipandia juu, ndio maana nimekuja. Wewe umemwinda paa, basi sasa mimi nakuwinda wewe." Akazimia Plakido akaanguka juu ya frasi. Khalafu akili zikamrudia, akalia kwa uchungu, "Wanitakia nini, Bwana, nipate kukuamini na kufanya upendalo ?" Akaambiwa, "Ndimi Masiya, Mwana wa Muungu, niliyeviumba mbingu na inchi, na nuru nikaitenga na giza, nikaagiza siku, na miezi, na miaka. Nika-fanyiza Adamu kwa mavumbi ya inchi, kwa ajili yake nikalitwaa umbo la mwana Adamu. Nikasulibiwa, nikafa, nikazikwa, siku ya tatu nikafufuka." Plakido akamwambia, "Hayo yote nayaamini, Bwana. Nawe ndiwe mwenyi kumwongoza vema aliyepotea." Sauti ikamjilia tena, "Kama ukiamini, nenda mjini uka-batizwe." Akajibu, "Niwafunulie haya mke wangu na watoto, wapate kuamini nao ?" Akaambiwa, "Wafunulie ; kesho assubuhi rudi papa hapa, utasikia

khabari za maisha yako iliyosalia." Bassi Plakido akaenda zake nyumbani, akamwarifu mkewe yote yaliyompata, wakaamini, wakabatizwa, na watoto wote wawili. Plakido akatajwa jina lake Eustasio, na mkewe Theosbuta, na watoto Theosbuto na Agapeto.

Siku ya pili akarudi pale pale alipoiona njozi, akaomba, "Ee Bwana, nakusihi, ujifunue kwangu, kama ulivyosema." Ndipo sauti ikasikiwa, "Umebarikiwa, Eustasio, kwani umeoshwa kwa neema yangu, ukamshinda Shetani, umemkanyaga chini aliye кудангanya, nae atakutolea ghathabu nyingi kwa ajili yangu. Utakuwa kama Ayub. Usiogope, dumu tu. Neema yangu yakutosha. Khatima utashinda. Chagua tu. Majaribu hayo yakushike sasa hivi, au katika uzee ?" Akasema, "Upendavyo, Bwana. Illa, kama ukipenda, nijaribiwe sasa, unihifadhi nikiningia majaribuni." Sauti ikamwambia, "Fanya kiime, neema yangu itakuwezesha." Ikanyamaza, isisikiwe tena. Eustasio akaomba, akamsifu Muungu, akaondoka akaenda zake nyumbani.

Siku zikapita si nyingi, marra mateso ya Ayub yakamjia Eustasio na jamaa zake. Ng'ombe zote, na kondoo, na mbuzi wakafa kwa maradhi mabaya sana ; watumwa wengine wakakimbia, wengine wakafa palepale ; maharamia wakaiteka nyumba, wakamfukiza yeye, na mkewe, na watoto, wenyi umasikini na uchi. Mfalme akantafuta sana shujaa, asipate hatta dalili yake moja. Wale maskini wakapotea siku nyingi, na nguo mbovu, na njaa inauma ; wakafika pwani, wakakuta chombo kinasafiri, wakamwomba nakhodha awavukishe ng'ambu ya pili. Akakubali, kwani alimwona Theosbuta ndiye mwanamke mzuri sana, akamtamani kuwa mkewe. Wakavuka, wakafika ng'ambu ya pili, wakashuka. Yule nakhodha akiwatoza nauli, Eustasio akamwambia, "Ee Bwana,

mimi maskini fukara, sina hatta pesa." Akajibu nakhodha, "Basi, haiduru. Ntamtwaa mke wako. Ndiyo nauli." Mwanamke akalia akaambatana na mumewe, Eustasio akasema, "Simwachi mimi, illa nikifa." Nakhodha akasema, "Upendavyo. Haya nyie, mkamateni huyo mwanamke, mpeleke chomboni. Na mtu na watoto, watupeni majini." Hatta mwanamke akamsihi Eustasio, "Ee mume wangu, uniache, ujiponye nafsi na watoto. Kufa ndio kwa marra moja tu." Akamsihi sana, akakubali, akawashika watoto mikono, wakaenda zao, wakilia, "Ee Mama ! Ee watoto maskini ! Ee Mama, umepotea, umepata utumwa mzito katika inchi ngeni, utalia sana." Wakaenda hatta wakafika palipo mto mkubwa na mpana, na maji mengi yapita kassi, Eustasio akakhofu kuavukisha watoto wawili wote pamoja. Akamwacha ukingoni mmoja chini ya kijiti, akamchukua wa pili akaingia mtoni. Shidda saña kuvuka, maji karibu yakamshinda, akajitahidi sana, akafika akampeleka mtoto ukingoni ; akaingia mtoni tena kwenda kumtwaa mtoto wa pili. Alipofika katikati ya mto, aliona chui anamnyemelea yule mtoto aliye kwisha kuvuka. Eustasio akamlilia mtoto akimbie, akafanya bidii kurudi pale, asiwahi kabisa. Chui akamkamata mtoto akamchukua. Marra simba akinguruma, baba akashtuka, akatupa jicho ng'ambu, akaona simba yule akimchukua mtoto aliyesazwa nyuma. Shujaa akalia sana, "Ole wangu ! kama mti mzuri nalisitawi, sasa nimekauka. Watu wengi wengi walionizunguka, sasa nipo peke yangu. Mkewe amekuwa mtumwa, na watoto wanawe wamekuwa. Ee Muungu ! si hayo ya kumshinda Ayub ? Yeye alikuna kitanda, mimi sina. Yeye alikuna mke, mimi sina. Yeye alikuna rafiki, mimi sina. Ee Muungu ! unilinde midomo, nisitoe mapumbavu na makuu." Khalafu akashukuru Muungu, akashika njia, akawasili hatta mji, akajiajirisha kwa

mtu mwenyi shamba, akamtumikia vema na amini miaka khamstashara. Hatta yule mtu akafa, Eustasio akairithi nyumba na shamba pia. Akakaa.

Na mfalme wa Rumi akikaa vile vile, lakini hafanikiwi. Adui wakazidi kumsonga, wala hana mtu shujaa wa kuwashinda, kama Plakido, akamkumbuka. Akamtafuta pote kwa bidii. Hatta akatuma wapelelezi wawili kwenda inchi mbali, na bahati yao wakamkuta Eustasio analima shamba, wasimtambue kwanza kama ndiye, wakamsalimu, wakamwuliza, "Ee rafiki, wajua mtu mwenyi jina lake Plakido, na watoto wake wawili?" Nae akawatambua wao, akasema moyoni mwake, "Nifanyeje? Nirudi huko, nisirudi? Illa mimi mtu mmoja tu peke yangu, sina mke, sina mtoto. Bora kukaa papa hapa." Akawambia, "Sikumwona mtu jina lake Plakido." Wakanwambia, "Basi, tumekuja burre. Twatafuta jemadari wetu aliyetupotea, hatumpati." "Tangu lini amepotea?" "Mwaka huu wa khamstashara, naona. Basi kuaheri, tunakwenda." Akawambia, "Ee wangwana! karibuni kwangu; kubaya tu, lakini mkipenda, karibuni." Wakaingia kwake, wakala, Eustasio akawaandikia. Tena akafikiri ulimwengu wake wa zamani kwao, fikira zake zikamshinda moyo, akalia, akatoka chumbani kwenda kunawa uso. Mmoja wao akawambia mwenzake, "Sijui vema, naona lakini huyo mwenyewe, ndiye tunayemtafuta. Uliangalia alivyosita tulipomkuta kwanza?" Akawambia, "Ndio, tena sasa hivi ametoka machozi." "Basi, tutazamishe sana kitwa kama kina kovu alilolipata katika vita ya zamani." Aliporudi Eustasio, wakatazamisha, wakaona liko, wakamtambua, wakafanya furaha sana, tena wakamtambulisha na matendo yake makuu kwa watu wa mji na ujirani wote.

Wakashika njia wakasafiri siku khamstashara hatta walifika Rumi. Mfalme akatoka kumlaki,

Eustasio ataka kumsujudia, ye ye hakubali, wakaingia mjini pamoja, mfalme na shujaa. Watu wakafurahi wengi wakaja kuandikwa majina kuwa asikari, aka-fanya jeshi kubwa juu ya adui. Wakaja vijana wawili wazuri na warefu sana, nao hirimu moja na nyuso zao sawasawa, wenzo wakawachagua kuwa wakubwa. Nae Eustasio akawapenda akawaweka mahali pa mbele katika jeshi, wakaenda kufanya vita pale alipofukuzwa chomboni na yule nakhodha. Walipofika, walitua, wale vijana wakakaribishwa nyumbani mwa mjane mmoja, wakala wakaisha. Tena wakazungumza khabari zao za zamani. Mmoja akasema, "Nilipokuwa mtoto mimi, babangu alinivukisha mto begani mwake, akaniweka ukingoni akarudi kuchukua na ndugu yangu, simba akaja akanichukua. Nilipokichukuliwa, nikaona chui amekamata ndugu yangu. Watu wakaja wakamfukuza simba akaniacha, nikao-koka. Na mamangu alifungwa na nakhodha wa chombo pwani ya bahari hii." Marra kijana wa pili akalia, "Ewe ndugu yangu ! ndugu yangu ! ndimi niliyechukuliwa na chui, nikaokoka vile vile." Waka-furahiana mno. Nae mjane alistaajabu akisikiaye khabari hizo, kesho akaenda kwa Eustasio, akamkuta amezungukwa na jeshi la wakubwa, nao vijana wawili wako. Akamwomba rukhsa ya kurudi kwake, akasema, "Ee Bwana, mimi hapa mgeni. Mwaka huu wa khamstashara tangu nilipotoka na mume wangu, nae kwanza tajiri, tukawa maskini, tukafika pwani, tukavuka chomboni, marra nakhodha alitutoza fedha ya nauli, na sisi hatuna fedha. Akanifunga nikakaa kwake miaka mengi, Muungu akamzuia asinitende mabaya. Alipokufa, nikapata uhuru, nikakaa. Sasa nataka kwenda Rumi kumtafuta mume na watoto." Marra Eustasio akamwambia, "Ndiwe mke wangu, Theosbuta." Akaitikia, "Ndiwe, mume wangu, Eustasio," kwani walitambulikana. Eustasio aka-

mwambia, "Lakini watoto wetu hatuwaoni tena. Walichukuliwa na chui na simba. Nalionna mimi." Nao vijana wakampigia magoti, wakasema, "Ndiwe baba yetu." Mamao akasema, "Ndinyi watoto wetu, kwani nimesikia khabari mlivyozungumza." Ikawa furaha kuu kwa watu wote, wakapiga vigelegele vingi, na ngoma, na panda nyingi. Wakapigana na adui, wakawashinda sana, wakarudi kwao. Walipofika, wakamkuta mfalme Trajano amekwisha kufa.

Paliondokea na mfalme mwingine, akamkaribisha Eustasio kwa heshima nyingi, akafanya karamu kubwa ya vyakula namna zote zilizo tamu, na za thamani. Wakala wote. Khala fu mfalme akamwambia, "Kesho tutawatolea dhabihu miungu wa vita, na kushukuru kwa ajili ya kushinda adui." Eustasio akamwambia, "Bwana wangu mfalme afanye apendalo, lakini kama mimi nisipokuwamo, usiseme nimekudharau. Hasha!" Mfalme akaona hasira, kwani ni kafiri, achukia sana Wamasihiya, akamwamuru, "Nakuamuru, uwepo wewe na jamaa zako madhbahuni pa Mars kesho adhdhuhuri. Utatoa dhabihu kwa mkono wako." Eustasio akamjibu, "Mkono mwenyi kutoa dhabihu vile ntaukatia mbali." "Basi Mmasihya wee? chagua, kutoa dhabihu ama kufa." "Nife basi, Bwana. Namwabudu Masiya wala si sanamu." "Basi Masiya akuokoe na simba. Haya, asikari, mchukueni huyu kwa tundu la wanyama. Twende zetu, wageni wangu, kwenda amfiteatro." Theosbuta akasema, "Na miye nataka kwenda." "Haya, simba watashiba leo." Wakaenda amfiteatro. Watu wakajaa wengi wengi hatta kusongana, kwani wamesikia yule jemadari mkuu ataliwa leo na simba. Wengine wakamsikitikia, "Ujinga gani kufa burre! kutia uvumba kidogo motoni tu, ndiyo kuokoka." Wengine wakafurahi, kwani waliwachukia Wamasihiya. Wengine wachache wakamwomba Muungu, amhifadhi

ndugu yao, kwani nao Wamasihiya. Basi Eustasio alisimama katikati, na mkewe na watoto wawili. Mfalme akapungia mkono wafunguliwe simba. Wakafungua mlango wa tundu, simba akaruka nje kwa ngurumo. Alipowaona vijana, akainama kitwa, aka-wanyemelea polepole akawalamba miguu. Simba mwengine akatokea, na mwengine, yule mzee simba wa kwanza aliwafukuza wenzake, akapigana nao, wakarudi tunduni. Mfalme akaghadhabika sana, akasema, "Basi, huyo mganga, amefanyiza dawa juu ya simba. Labuda hana dawa juu ya moto. Fanyeni tayari ng'ombe wa shaba." Na ng'ombe ya shaba ndiyo mfano mkubwa wa ng'ombe, wazi ndani, na mlango mbavuni wa kuingilia ndani tumboni mwa ng'ombe. Wakawasha moto mkubwa chini, ng'ombe akapata moto sana. Wakafungua mlango, asikari wakataka kuwatupa ndani. Asikubali Eustasio, aka-sema, "Tutaingia kwa miguu." Wakalaeta ngazi, akapanda Eustasio, na mkewe na watoto wawili wali-fuata nyuma, wote wakaingia taratibu na pasipo hofu, wakafunga mlango. Moto ukawaka siku tatu, siku ya tatu jioni wakafungua mlango, wakawakuta Eustasio na mkewe na watoto wawili, wamelala kama kwa usingizi. Hatta unyele mmoja haukuharibika, wala harufu ya moto hapana juu yao. Wakamzika kwa heshima nyingi wakampigia maombolezo mengi, kwa ginsi shujaa alivyokufa kikondoo kwa ajili ya Masiya.

---

#### 14. GUIDO SHUJAA.

ZAMANI za kale paliondokea watu wawili katika Uingereza, majina yao Guido na Turi, nao mashujaa sana wote wawili. Wakakaa na mfalme wa Uingereza,

wakampigania vita nyingi wakatenda makuu, wakawa mashujaa thabiti halisi. Hatta Guido akaoa mke wakapendana sana, yeye na mke wake. Katika usiku Guido akatokewa na njozi, kama malaika wa Muungu akisema naye, akaogopa. Malaika akamwambia, "Ee Guido, mbona umelala? Amka, vaa selaha, kaenenda kuupigania msalaba mtakatifu." Akamwambia, "Bwana, nimepigana sana marra nyingi." Malaika akamwambia, "Kweli umepigania waana Adamu maara nyingi kwa bidii. Sasa umpiganie Muungu na msalaba wake Masiya. Fanya vita juu ya adui zake Muungu." Malaika akatoweka, na Guido akafahamu amekwitwa kwenda Yerusalem kipigana na makafiri. Akamwamsha mkewe akamwambia, "Ee Felikia, hatuna buddi kutakana buriani, kwani nimekwitwa kwenda Yerusalem kufanya vita juu ya makafiri." Akamwambia, "Ee Bwana wangu, utaniacha? bora mauti. Haya, nife tu." Akatwaa kisu akataka kujifisha pale pale; akazuiliwa kwa nguvu na Guido. Akamwambia, "Ee Felikia? usijisumbue mno. Sina buddi kwenda Yerusalem. Subiri bassi, mke wangu, kwa muda kitambo." Akasema, "Muungu apendalo lifanyike. Twae pete hii; killa uitazamapo, ukiwa na hali ya furaha ao huzuni, unikumbuke mimi Felikia mke wako." Bassi Guido akakusanya watu wake, na rafiki yake Turi naye akaenda pia, wakashika njia ya kwenda Yerusalem.

Wakaenda wakaenda hatta wakafikia inchi iliyokwitwa Dakia, nayo inchi imeviziwa sana na makafiri. Bassi Guido akamwambia rafiki yake, "Ee Ndugu, nenda kwa mfalme wa inchi na upanga wako, ukamponye katika mikono ya adui. Nami nakwenda Yerusalem; adui za Muungu wakiisha kushindwa ntarudi papa hapa tuonane, tukarudi wawili hatta kwetu." Akamwambia. "Vema, upendavyo wewe. Ntakaa mpaka tuonane." Wakaagana. Guido akae-

nda Yerusalem, akapigana sana na Waaslimu, aka-washinda marra nyangi sana, hashindwi hatta marra moja. Killa mtu maneno yake mamoa yote, kumsifu Guido, matendo yake, wema wake, huruma zake. Wakampangia tenzi na mashairi, sifa zake zikaenea ulimwenguni mwote. Naye Turi pia akafanikiwa sana, akampatia mfalme milki yake, akawafukuza pia makafiri. Mfalme akamwonea shukrani sana, aka-mpasha daraja bora sana na utajiri mwingi sana. Ndio mwanzo wa kusumbuka kwake. Kwani mtu mmoja, jina lake Plebeo, aliondoka, naye kabla hajaja Turi, ndiye mwenyi kusifiwa sana kwa shujaa na maarifa ya vita. Turi akampitia mbali, bassi aka-mwonea uwivu, tena kumchukia, tena kumsingizia, hatta akamfanyizia uwongo mkubwa, kama huyo Turi ana shauri baya sana la kumwasi mfalme na kumtwalia milki yake. Mfalme akamsadikisha akamwita Turi, akamshutumu sana ya kuwa mwasi, wala hana shukrani. Akamwambia, "Ondoka kwangu. Nime-kuheshimu sana, hatta nikataka kuongeza tena. Sasa kwani umenipigania sana, nakuachia maisha. Enenda mzima, lakini maskini." Akafukuzwa akapotea kwa umasikini wake, na huzuni, hatta akachoka akakaa kitako njiani, akamshukuru Muungu. Akaja mtu mrefu sana, akamwambia, "Ee Rafiki, umetokapi ?" Akamwambia, "Ee Baba, mimi nimetoka Rumi, miaka mingi nimekaa hapo, sasa nakwenda pangine. Tena nikawa na rafiki, akaagana nami, akaenenda Yerusalem, sasa yu hayi sijui, ama amekufa." Yule mtu mrefu akasema, "Rafiki, nimechoka mimi. Kwa ajili ya rafiki yako yule, niache nikulazie kitwa kifuanini, nipate usingizi kidogo." Akasema, "Haya !" Na yule mrefu uso wake hautambulikani veina kwani ? kwa sababu amefunikiza kwa kitambaa. Bassi alipolala, mchiro mdogo mweupe akamtoka kanwani, akaenda mbio hatta mbavuni kwa kilima, akaingia

tunduni. Halafu akarudi akaingia tena kanwani mwake akilala. Marra akaamka, akamwambia Turi, "Katika ndoto yangu, nalionna mchiro mdogo naye mweupe akitoka kanwani kwangu akienda mbio tunduni kule kwenyi kilima, akarudi, akiniingga tena kanwani." Turi akasema, "Sivyo ndoto, Baba. Nalionna na mimi hapa nikikesha. Lakini mchiro alifanyani buko kilimani, sijui." Akamwambia, "Ondoka bassi, twende kutazama, labuda tutapata kitu cha tunu." Wakaenda, wakafika tunduni wakiona paango kubwa, mtu mrefu akasema, "Kumbe ndivyo, yuko joka amekufa, amejaaa thahabu ndani, mali zake sisi tumezipata, na tena upanga. Ah ! maneno gani hayo umeandikwa ?" "Kwa mimi Guido atawashinda adui zake Turi." Akasema Turi, "Ee Guido wee ? Guido wee ! u wapi tena, rafiki yangu ?" Yule akamwambia, "Haya, tuzigawanye mali. Twaa wee thahabu ile nydingi na johari, kwangu upanga tu." Marra Turi akalia, "Upanga wa Guido kwako wee ? Haifai." Yule mrefu akamatizia, akisema, "Naam, kwangu mimi upanga wake Guido, kwangu mimi, Ee Turi." Akavua kile kitambaa kitwani, Turi akamtazamisha uso akisema, "Ndiwe Guido, rafiki, ndugu ! Tu-meonana tena. Bassi, ndugu." "Haya, Turi, usilie. Mimi ntapigana na adui yako kwa upanga huo ntawatiisha. Wewe nenda kwako tu." Wakaagana, Turi akaenda zake kwao na mali nydingi sana, Guido akaenda jumbani kwa mfalme.

Akabisha, akaja mnganje mlango akamwambia, "Nani huyo ? umetoka wapi ?" "Mimi msafiri mgeni, nimetoka Yerusalem, narudi kwetu." Marra mnganje akampigia magote akisema, "Karibu Baba, unibarikie." "Umebarikiwa, Mwanangu, Amani kwako na nyumbani huku. Namtafuta mfalme." Naye mfalme amekaa chakulani, akamjia, mfalme akamkaribisha, "Salama sana, habari gani za Yeru-

salemi ?” “Amani kule, bwana wangu, Tumelitwaa kaburi la Bwana, tukawafukuza Waaslimu.” “Haya, mwondokeleeni huyo ; starehe, Baba ; leteni mkate na kahawa. Ee Baba, umesikia habari za shujaa mmoja, jina lake Guido ?” “Nimesikia, tena nime-mwona, twalikuwa tukila pamoja, tukalala kitanda kimoja.” “Na huko Yerusalem wamepata habari zetu wafalme Wamasihya ?” “Twalisikia mfalme wa Dakia amerudishiwa milki yake kwa msaada wa shujaa aliyetoka Rumi, akamzidishia heshima nyingi na mali pia.” Mfalme akakunja uso akasema, “Ndivyo ilivyo.” “Tena imesikiwa, ya kwamba uli-mfukuza yule shujaa mwema, kwani amesingiziwa na mtu mbaya sana, Plebeo ; hatta wewe ukamsadiki.” Naye Plebeo yuko amesimama mbavuni pa mfalme akasema, “Mwongo wewe, umetoa uwongo mkubwa. Ukiuawa, utajua. Yule Turi mwasi, alitaka kumsukumia mbali nfalme, na kuitwaa milki.” Guido akamwambia, “Nimesema kweli mimi, Bwana. Ukiwa Plebeo, bassi wewe Plebeo uliye mwongo. Mfalme akinipa rukhsa, nitathubutisha maneno kwa kupigana nawe.” Mfalme akakubali, akasema, “Ashindaye ndiye aliyesema kweli, kwa rehema yake Muungu,” Guido akamjibu, “Ndiyo nitakayo, illa sina selaha, upanga huo tu bassi. Lete selaha, ntapigana.” Akasema, “Vema. Kesko aththuuri mtapigana. Sasa enenda nyumbani.”

Kesho saa a aththuuri watu wote wa mji wakaja kutazama pale penyi kupigana, wakamhimiza Guido wakisema, “Adui yako yuko amesimama, akuita, asema, wee mwoga, mbona umekawia ?” Marra Guido akatwaa selaha, na upanga, akatokea, mfalme akaketi kitini, wakapigana sana. Hatta Guido akafanya bidii akamchosha adui kwa mapigo mengi, yule adui kiu kikamshika hatta karibu hufa. Akamwambia Guido, “Ee Bwana, niachilie kidogo, ninywe maji marra

moja tu. Nawe ukitaka halafu, utapata." Akasema, "Vema." Plebeo akanywa, akaburudika, wakapigana tena sana. Hatta na Guido akiona kiu akasema, "Bassi nataka ulivyoahidi." Akasema, "Ewe Mjinga, ukitaka maji, enenda katwaa illa kwa nguvu." Akasema, "Haya ntakwenda." Akaenda kwenyi ziwa, akimkinga adui kwa ngao, akarukia majini, akanywa sana, akamrukia adui akamfukuza sana. Marra mfalme akasema, "Bassi, mpaka kesho." Binti mfalme akamtwa Guido, akamganga jeraha, akamwuguza akampikia, akalala, kwani amechoka usingizi ukamshika sana. Plebeo akawaita watu saba hodari, ndio watoto wake, akawaambia, "Enyi watoto, yule mgeni akitokea kupigana tena kesho, nimekwisha. Sijakuta shujaa kama huyu." Wote wakasema, "Haithuru, Baba, sisi tutamwuguza sana." Naye Guido amelala ndani. Usiku wa manane wakaja wale saba watoto wa Plebeo, wakafungua mlango, wakaingia chumbani. Mkubwa wao akasema, "Usingizi umemshika sana. Shauri gani bassi ? Tukimwulia mbali papa hapa, tutakufa sisi kesho." Mmoja akasema, "Siyo bahari chini karibu ?" Wakasema, "Iko, lakini tukimtumbukiza, akiamka je ?" Akasema, "Tutupe na kitanda pia." Naye Guido kulala tu, wakamtupa. Hapo chini palikuwa mvuvi, anavua kwa wavu katika mtumbwi, akasikia kishindo, akasema moyoni mwake, "Kishindo gani hicho ? Ah ! Ah ! kitanda kiko kinalea majini, kumbe na mtu juu yake." Guido akaamka, "Ni wapi mimi ? Ee Rafiki, njoo, nishike, nazama. Mimi yule aliypigana jana. Ahsante sana." Akaingia mtumbwini, "Nini iliyonipata ?" Akasema, "Sijui. Naliskia kishindo, nikachungulia kwa balamwezi nikaona wewe na kitanda kinalea. Hila hiyo ya adui." Akasema, "Haithuru. Hawakuifkiliza vema. Kesho ntawafathaisha sana kwa maana ya jeuri." Ulipo-

kuwa assubuhi, watu wengi wakaja vile vile wakajaa sana penyi kupigani. Mfalme akaketi, vyote tayari, Plebeo akatokea akamwambia mfalme, "Mimi nipo, nataka kupigana na adui yangu." Akamwambia, "Vema." Akatuma asikari kwenda kumwita Guido. Marra akaja binti mfalme, na uso wake huzuni sana ; mfalme akamwambia, "Ee Mwanangu, yu wapi yule shujaa, rafiki yake Turi ? Tunangoja sote." Akamwambia, "Sijui mimi, alipo. Nalimwacha usiku ameshikwa sana na usingizi. Sasa haonekani, wala kitanda hakipo." Plebeo akasema, "Mwoga huyo, mjivunaji mtupu, hathubutu kupigana tena. Amekimbia. Mwoga sana." Mtu maskini akaondoka akasema, "Hapana, Bwana, hakukimbia." "Wase-maje wee ?" "Yuko amelala kijumbani kwangu. Nalimwokota usiku akielea majini na kitanda chake, karibu na jumba la mfalme. Nikamtwa nikamponya." "Vema. Umwite. Bassi, Plebeo, usisumbukie sana adui yako. Anakuja. Umpe selaha tu." Plebeo akaingiwa na hofu akatetemeka, akasema, "Ee Mfalme, usimharakishe, haraka haina baraka, hajapata nguvu naona, ataka jiburudisha." Marra hiyo akaja Guido akamwambia vikali, "Hatta dakika moja sitaki. Kupigana marra moja, ndio nataka. Kumbuke usiku leo." Wakashika kupigana, wakachapana marra mbili tu. Ya tatu, Plebeo akakatwa kitwa, akaanguka chini, akafa. Mfalme akamwambia Guido, "Muungu ameamua kwa haki. Hatta sasa hivi nimesikia habari za huyo alivyondanganya, na watoto wamekufanyia jeuri. Watapata thawabu, ndiyo kuuawa. Bassi, Bwana, kwa ajili yako namrudishia Turi mali yake yote na heshima kama kwanza, na zayidi pia. Na wewe, nataka neno moja. Jina lako nani ? tupate kujua nani aliyemshinda mwovu akampigania vema rafiki yake aliyetuokoa." Akamwambia, "Jina langu limekwisha kujulikana nawe.

Mimi yule shujaa wa Yerusalem, Guido." Watu wote wakamjia wakampigia vigelegele vingi vya furaha na kumsalimia, mfalme akamkumbatia, akampenda kama ndugu yake.

Miaka saba ikaisha tangu alipotoka Guido kwake akasafiri kwenda Yerusalem. Na mkewe alikaa pale, kazi yake siku kwa siku kuwatunza maskini, na kumpa sadaka killa atakaye. Bassi killa ampaye, yule bibi humwomba neno moja tu, ndio amwombee mume wake apate kurudi. Ndio moyo wake utafurahiwa sana akirudi mumewe. Bassi katika siku yule bibi yuko barazani, baraza likajaa masikini wengi, akawauliza habari, akatoa sadaka. Na mtoto wake yupo pamoja na mama, akamsikia mama anawaagiza watu wamwombee Guido, akasema, "Ee Mama, siye baba yangu uliyewaagiza wamwombee." Akamwambia, "Ndiyo, Mwanangu. Yapata sasa miaka saba tangu alipotoka. Alinioa akakaa siku si nyangi akaitwa na Muungu kwenda Yerusalem, akaenda kumpigania Muungu huko." Marra alipokisema, akamkaribia mtu mrefu amesimama mbali kidogo akampa sadaka akamwagiza vile vile. Yule mrefu akainama kitwa, hatoi neno, bibi akapita, na mtoto wake. Yule mtu akainamatena akamkumbatia mtoto, akamwambia, "Muungu akubariki, Mwanangu, upate kumtumikia vema." Bibi akamwambia, "Ahsante sana, Baba. Wataka nikufathili neno ?" Akamwambia, "Ee Bibi, nataka unipe pango lile dogo, chini ya mwamba wa tai, nikae humo hatta nikafe." Bibi akashtuka akasema, "Bassi umejuu sana mahali penyewe. Wewe ntu wa hapa ?" "Zamani sana, Bibi, nimekaa hapa, nikasafiri. Sasa maskini wa Muungu." "Bassi upendavyo. Nenda kamwombee mwenyeji nyumba hii." Akaenda akaakaa paangoni. Killi siku huja jumbani, huzungumza na mtoto wa bibi, humsumulia habari za vita katika Yerusalem na mashujaa walivyopigana wakafanya

makuu sana, wangine wakarudi kwao salama. Hati-ma akapatikana na farathi, akalala akamwambia mtoto, "Ee Mwanangu, twae pete hii, kampelekee mama yako, kamwombie, akitaka kunitazama kabla sijafa, aje upesi." Mtoto akaenda kwa mama, aka-mwambia, "Ee Mama yangu, yule maskini hawez sana, amekupelekea pete hii, ataka uje upesi kumta-zama kabla hajafa." Akaitazama pete hiyo, akasema, "Upesi, Mwanangu ! upesi ! ndiyo pete ya bwana wangu, baba yako. Twende, twende paangoni." Akaenda mbio akafika, akamkuta mume amekwisha kufa. Akajitupa juu yake akilia, "Ole wangu ! ole wangu ! zi wapi sadaka ? mume wangu akaomba sada-ka, nami sikumtambua. Ndiye baba yako, mwana-nangu, aliyezungumza nawe akakukumbatia wewe, wala hukumtambua. Ee Guido wee ! ulimtzamisha mkeo, ukambariki mtoto wako, wala hukutambulikana. Ee mume wangu ! mume wangu !" Akakaa katika huzuni yake.

## 15. VIBWETA.

PALIONDOKA mfalme wa Rumi, jina lake Anselmo, na mkewe binti wa mfalme wa Yerusalem, mwana-mke mzuri sana na mwema, wakakaa siku nyingi, ha-wakuzaa mtoto. Mfalme akatembea bustanini aka-mkumbuka mfalme wa Amplui, aliyemfanyia vita nyingi akamsumbuwa sana siku zote, kwani hana mtoto wa kuilinda milki yake. Alipokitembea vile akitaza-ma mwezi, kama akazimia roho yake, akaona ndoto, na katika ndoto yake ussubuhi ulipambazuka vizuri sana, na mwezi ukaonekana nuss mweupe nuss mweusi kidogo. Akaja ndege mdogo wa rangi mbili aka-mrukia, tena wanyama wawili mbavuni wa kindege

wakintia moto kwa miili yao. Wakaja tena wanya-ma wangine, wakasujudu mbele ya ndege wakaenda zao, tena ndege wengi wangine wenyi mabawa mazuri na sauti pia, wakiimbaimba nyimbo zao hatta kumwamsha mfalme. Anselmo akafathaika kwa ndoto yake akawaita waalimu, na wakubwa, na madiwani, akawasumulia ndoto, akataka kujuu tafsiri yake. Waalimu, na wakubwa, na madiwani wakafanya shauri ya mambو haya, wakamwambia mfalme kwa furaha, "Ee Bwana, ndoto hiyo njema sana, kwani milki yako itazidi kusitawi. Tena mwezi ukipungukiwa kidogo weupe wake, ndio maana, malkiya kidogo atathoofika kwa kuzaa mtoto. Na yule kindege ndio mtoto atakayezaliwa. Nao nyama waliomtia moto, ndio walio wema na walio wakubwa wa milki hii, watamtolea mtoto asili zao za kumlinda na kumhifathi. Tena mataifa makuu na hodari watamsujudia, na watu wetu watafurahiwa mno, kama wale ndege wenyi kuimba vizuri vizuri katika ndoto yako. Hiyo ndiyo tafsiri, Ee Mfalme." Mfalme akafurahi sana mno, akazaliwa mtoto mume, akazidi kufurahi.

Bassi mfalme wa Amplui aliposikia ya kwamba Anselmo amezaliwa mtoto mume, aliona hofu kwa sababu alivyomsumbaa sana Anselmo kwa vita, akasema, "Sasa mimi ntalipizwa kisasi na mtoto huyo." Akatubu akampelekea Anselmo waraka aka-taka amani. Anselmo akausoma waraka, akamletea jibu la kusema, "Ukitoa amana na kodi kidogo, nitakusamehe." Mfalme wa Amplui akawaita wakubwa barazani akawasomea barua, akataka shauri kwao. Wakasema, "Maneno yake Anselmo mazuri sana. Na amana yake, huna binti mzuri? na yeze ana mtoto huyo mume. Bassi waonane. Ndio amana ya amani." Akawasikia, akamwandikia barua Anselmo, naye akapendezewa sana.

Bassi watoto wale walipokua, mfalme wa Amplui

akamsafirisha binti wake kwenda Rumi kwa merikebu nzuri sana na kubwa, yenyi milingote mirefu na baharia wengi, na jamii ya watu wakubwa na watumishi wakafuatana naye kwenda kufanya arusi kubwa ya binti mfalme, na mwana wa Anselmo. Wakaenda baharini, ikaja tufanu kuu, ikaipiga merikebu, ikachukuliwa huko na huko kwa mawimbi, ikavunjika penyi mwamba, ikazama. Wote wakafa illa yule binti mfalme tu, naye akamwaminia Muungu akaokoka. Kwani tufanu ikiisha, merikebu ikapanda katika vilindi, ikaelea, lakini haiwezi kwenda kwa ginsi ilivyovunjika. Akaja nyamgumi mkubwa aka-taka kuimeza merikebu na kijana pia. Bassi kijana aliwasha moto, nyamgumi akaogopa asithubutu kuikaribia aimeze merikebu, kwani moto ulimtia hofu. Halafu kijana alichoka kwa kukesha sana, usingizi ukamshika alfajiri ; aliposinzia, moto uka-zimika, nyamgumi akaja akammeza. Bassi kijana alipoamka, giza pote, kwani yumo tumboni mwa nyamgumi. Hakuogopa, atwaa jiwe na kisu, aka-gonga jiwe, moto ukatoka, ukamchoma nyamgumi mbavuni, hatta nyamgumi akajiona hawezo sana, ataka kufika pwani upesi. Pale pwani palikuwa mtu anatembea naye mkubwa na tajiri, akamwona nyamgumi anakuja pwani akawaita watumwa, wote wakaja pwani wakampigapiga nyangumi, wakamtia jeraha nyingi na karibu kumfisha. Walipokipiga, wakasikia kijana analia ndani, "Ee Rafiki, acheni, acheni ! Nimo mimi hapa binti mfalme." Waka-shangaa mno, wakamkokota nyamgumi pwani, wakamtumbua, kijana akatokea. Wakamwuliza habari, wakamsikitikia sana, wakampeleka nyumbani wakamtunza.

Bassi Anselmo alipojua kama kijana amepona, akaona furaha sana, akaja kumtwaa, akamhurumia, akasema, "Umeteswa sana kwa ajili ya mtoto wangu,

illakini usipojaribiwa tena vingine, hustahili kuwa mkewe." Akanena, "Vileteni vibweta vitatu." Watumishi wa mfalme wakaleta vibweta vitatu. Kimoja ndicho thahabu safi, chenyi vito vingi na johari; ndani kimejazwa mifupa ya watu; kuka-andikiwa, "Anichaguaye, atapata astahiliyo." Cha pili, cha fetha nzuri, kimetiwa ndani udongo na mafunza; nacho chenyi andiko, "Anichaguaye, atapata asili yake vitamaniyo." Cha tatu risasi tupu, haking'ai wala kupendeza, kikajaa ndani almasi, yakuti, feruzi, killa kito cha tunu; kika-andikiwa, "Anichaguaye, atapata Muungu aliymwekeea." Mfalme akamwambia kijana, "Ee kijana, tazamisha vibweta hivi, vyote vizuri na vya thamani; ukichagua kitakachokufaa wewe na wenzio, utaolewa na mtoto wangu. Usipochagua, urudi kwenu kwa baba." Yule binti akainua mikono akamwomba Muungu, amsayidie katika jaribu. Kwanza akakitazamisha kile cha thahabu, akasoma maneno yake, akasema, "Kizuri wewe na cha kutamanika, lakini yaliyomo siyatambui. Ee bwana wangu, sikichagui hicho." Akakitazama cha pili cha fetha, akasoma maneno, "Atapata asili yake itamaniyo." Akasema, "Asili ya waana adamu ndiye uovu, bassi ndivyo yaliyomo. Wala hicho sikichagui." Mwisho akatupa jicho kwa kile cha risasi, akasema, "Ewe kibweta, kinyonge wewe, lakini chenyi maneno mazuri, 'Muungu amwekeayo.' Bassi Muungu hawawekei watu yaliyo mabaya, illa yaliyo mema. Bassi nakuchagua wewe." Marra mfalme akamwambia, "Ee kijana mwema na bora, funue kibweta, kwani kimejaa vitu vizuri na vya tunu. Umechagua vema." Akaamuru siku ya arusi, arusi ikasitawi sana, wakakaa raha mwana wa mfalme na mkewe mpaka maisha.

## 16. MANENO MATATU.

**PALIKUWA** mfalme wa Rumi, naye mwema na mwe-nyi haki, hawaachilii waovu. Siku kuu ya kuzaliwa Bwana akafanya karamu akawaita wakubwa kuja kula naye jioni. Bassi karamu ikasitawi sana ndani ya jumba, lakini nje giza, na baridi, na mvua ikinya. Mngoje mlango akasikia mtu akimbishia, akaitika, "Nani huyo? wataka nini, Rafiki?" Akamwona mtu mrefu, amevaa nguo nene sana, ngozi ya dubu yenyi nyele nydingi sana, kama baridi ikimshika. Akamwambia, "Mimi mfanyi biashara. Nimetoka mbali sana, naleta bithaa nydingi sana, vitu vya tunu kwa mfalme, kama akipenda kununua." Akamwambia, "Karibu bassi, karibu. Mfalme anakula, lakini kwa karamu ya siku kuu hii akaribisha watu wo wote. Wataka chakula?" Akasema, "Mimi siku zote sioni njaa, wala kiu, wala baridi." Mgoje mlango akamwambia, "Na miye ninazo zote tatu. Haya, ingie."

Akaingia mbele ya mfalme. Mfalme akamwuliza habari. Akamjibu, "Njema. Nimeleta vitu vingi katika inchi zilizo mbali. Wataka nunua?" "Nionyeshe kwanza." "Nina maneno matatu ya kufaa sana." "Uyanene bassi." "Lakini, Bwana, naya-za. Nikiyatoa wewe usipoyapenda, yamenipotea na mali yake pia." "Na mimi je? Nikitoa fetha nisijeyasikiliza kwanza, kama yafaa ama hayafai, nisipotolewe na wakati na fetha pia? Kiasi gani?" "Reale elfu, bwana wangu." "Bassi nitoe reale elfu, nisipojua za nini?" "Maneno haya yasipokufaa, ntarudisha fetha." "Vema. Lete maneno yako." "La kwanza; usifanye mwanzo, usijefikiri mwisho." "Limenipendeza mno. Liandikwe pote katika nyu-

mba, kutani, na milangoni, na tena katika vitambaa na nguo za meza.” “La pili; usitoke njia kuu kwenda njia ndogo.” “Halinelei vema hilo. Haya.” “La tatu; usilale nyumbani alimo mwenyeji mzee na mkewe kijana.” Mfalme akasema, “Ngoje kwanza mwaka mmoja kwa killa neno. Ndipo utalipwa.” “Vema, nitakuwapo sawa sawa.” Yule mfanyi biashara akaenda zake.

Yule mfalme akakaa katika milki yake, akihukumu killa jambo kwa haki wala hawaachilii waovu. Hatta wangine walio wabaya wakamfanyia hila nydingi wamwue, wasiweze, kwani alizifahamu kwa akili. Akaondoka mtu mmoja akawaambia, “Mimi kinyozi wa mfalme, killa siku namnyoa. Toeni ahadi ya kwamba mimi ntakuwa mfalme, ntamchinja thoruba moja.” Wote wakakubali. “Kinyozi ndiyе atakayekuwa mfalme.” Siku ya pili kinyozi akaingia chumbani kwa mfalme, kwa desturi ya killa siku, akatwaa wembe akamfungia shingoni kitambaa. Na kitambaa kile kimeandikiwa kwa amri ya mfalme, “Usifanye mwanzo, usipofikiri mwisho.” Yule kinyozi akayaona maneno, akasema moyoni mwake, “Natenda nini mimi? Kumchinja mfalme nipate kutawala? Nitatawala wapi? Sio kuuawa tu kwa athabu nydingi, nao waliopatana nami watanitupa.” Mfalme akamwambia, “Ee kinyozi, ume-sinzia leo?” Kwa sauti ya mfalme, kinyozi akatemeka mno, wembe ukamponyokea, akaanguka magoteni mbele ya mfalme. Akamwambia, “Unani bassi?” Akamwambia, “Ee Mfalme, leo nalitaka kukuua, nikayaangalia maneno katika kitambaa nikafikiri ulimwengu na mwisho wake, sasa nimetubu sana. Unisamehe, bwana wangu!” Akaiambiwa, “Ukiwa amini, hakuna hofu.” Marra akaja mtumishi, akasema, “Yule mfanyi biashara yupo.” Mfalme akamwambia, “Umediriki, Bwana, kwa siku

yake sawasawa. Nalo neno la kwanza limethubutika, likaniponya uzima wangu." "Ndivyo niliyonena. Nakwenda zangu, Bwana, kiisha mwaka nitarudi."

Wale wabaya wakaona uchungu sana, wakasema, "Mtu mmoja hafai, tujaribie sisi sote. Mfalme huenda Napoli killa mwaka siku yapili yake kuzaliwa Bwana. Tumwotee njiani ; si njia kuu, njia ndogo, hakosi ndiyo atakayopitia." Wakasema, "Twende." Na mfalme siku ile alishika njia ya kwenda Napoli, wengi wakafuatana naye, wakubwa, na asikari, na watumishi, na makarani, wakafika karibu. Waka-mwambia mfalme, "Jua linashuka. Njia hii ndogo ndiyo ya kufika upesi kuliko njia kuu. Tuiendee." Mfalme akakataa akisema, "Nakumbuka lile neno, 'Usitoke njia kuu kwenda njia ndogo.' Na mwaka karibu kwisha. Nitalifahamu kama kweli. Bassi ninyi nussu mtangulie kwa njia ndogo, nussu wafuatane na mimi katika njia kuu." Waliokwenda njia ndogo wakafika penyi walipomwotea mfalme, marra wakatokewa na watu wengi wenyi selaha, wakauawa wote illa mmoja naye mtoto. Mfalme mwenyewe akafika mjini salama salimini. Kule mlangoni mtu akamkuta, ndiye yule mfanyi biashara, akamwambia, "Ee Mfalme, simama. Neno la pili limekwi-sha kuthubutika." Mfalme akamwambia, "Kwa-je ?" Akasema, "Wameuawa wote waliotangulia kwa njia ndogo, illa huyo mtoto mdogo peke yake." Mfalme akamwuliza mtoto habari akajua kama ndivyo. Akasema, "Bassi hiyo marra ya pili ni-meokoka. Neno lako limefaa sana." Akamwambia, "Ee Mfalme, kua heri. Kiisha mwaka nita-kuja."

Wakafanya hasira sana wale wabaya, wakasema, "Mashauri yote hayafai. Kazi burre tu. Bassi tushindwe, tusishindwe ?" Mtu mmoja akawa-

ambia, "Nina shaari mimi. Killa mwaka mfalme aenda kwa mji mmoja kumwamkia mlezi wake, nao mji mwenyewe mdogo, hamna nyumba illa moja ya kumkaribishia mfalme. Na mwenyeji nyumba mzee. Tumshawishi amchinje mfalme usiku." Wote wakasema "Haya." Mwenyeji nyumba akakubali. Mfalme akaja akataka kulala nyumbani mwake, akaona mlangoni kijana mwanamke amesimama, akamwuliza mzee, "Ni nani huyo? ni binti yako?" Akamwambia, "Hakuna, Bwana. Mke wangu huyo." Marra mfalme akasema, "Silali hapa mimi. Twende kuingine." Wakasema, "Upendavyo, Bwana, lakini nyumba ngine nzuri hamna mijini humu, labuda mbovu." Mfalme akasema, "Haithuru. Silali hapa mimi. Lakini ninyi kaeni." Wakakaa wakalala. Mtu mmoja akalalia kitanda cha mfalme. Bassi usiku usiku akaja yule mzee akamchoma kisu yule aliyelalia kitanda cha mfalme, akasema, "Nimemwua mwenyewe." Kwani hakujua ya kwamba mfalme hapo. Mfalme akaamka assubuhi akaja mtumishi akasema, "Mfanyi biashara yule amekuja. Tena habari za mijini njema, lakini mbaya sana." Aka-sema, "Mwite." Wakamwita. Akaja mwenyi furaha sana. Marra mfalme akasikia ya kuwa mtu wake ameuawa kitandani mahali pake. Akamwambia mfanyi biashara, "Neno la tatu limethubutika pia. Nitakuzidishia heshima nyingi na fetha yako marra tatu."

---

## 17. KUNGURU.

HAPO kale paliondoka ndugu wawili, mmoja ana mke, mmoja hana, wakakaa. Yule asiye na mke, akamwambia mwenziwe, "Nimejua, hapana mke

awezaye kusetiri neno. Kama hujui, mjaribie mke wako." Akamwambia, "Njema." Bassi katika usiku walikuwako wawili, yeye na mkewe, peke yao, akamwambia yule mwanamke, na uso wake kama akifathaika sana, "Ee bibi wangu, mpenzi wangu, jambo kubwa la kustirika limenipata; nataka kukupasha habari nisithubutu. Hakika yako utafunua. Ukitunua, nimeharibika." Akamwambia, "Hapana hofu. Siswi mwili mmoja na roho mmoja? Fayida yako fayida kwangu, hasara yako hasara kwangu." Akamwambia, "Haya, sikilize tu. Nilipotoka chumbani leo assubuhi, hashikwa sana na ugonjwa, hataka kutapika, hakakamuka-kakamuka, kumbe hatoka kunguru mkubwa mkubwa kanwani, akaruka kwenda zake, nami ni hofu na kutetemeka." "Ee Bwana, ajabu hiyo kweli. Lakini hofu hapana. Shukrani tu, kwani kitu kibaya sana kimekwisha kukutoka."

Ilipokuwa assubuhi, wakaamka, marra yule mwana-mke fikara zake zote kunguru tu, akamkimbilia jirani, akamwambia, "Ee Rafiki, nimesikia neno la kustirika sana, lakini wee, ah! sijui, niküwekee utatoa, hutoi?" "Nitoe wapi? hapana hofu. Sema bass." "Neno kubwa sana limempata mume wangu." "Neno gani hilo? Haya sema." "Usiku leo, aliugua sana, aka-shikwa na maumivu mengi, kumbe kunguru wawili wakubwa wakamtoka kanwani wakaruka dirishani wakaenda zao." Alipokwisha kutoa maneno yake, yule mwanamke roho yake kama haijambo kidogo, akarudi nyumbani.

Marra hiyo yule jirani amemkimbilia mwenziwe wa tatu, akamsumulia vilevile, illa hii tu, alimwongezea kunguru watatu. Hadithi ikaenea sana. Killaa iliposumuliwa, hutia kunguru mmoja juu. Hatimaye ujurani wote wamesikia yule maskini ametokwa na kunguru hamsini tumboni, hatta pana watu wamewaona kundi zima la ndege wakubwa weusi

wakiruka dirishani. Wote wakasema, "Mtu huyo mbaya sana, mchawi mkubwa. Tumfukuze kabisa." Wakaanza kumsumbuwa sana. Hana buddi kuwaita wote na kueleza asili ya hadithi. Mkewe akapata aibu sana na kuchekwa, watu wa mjini wakafahamu kama, "Mwanamke hasetiri hatta neno."

---

### 18. ISKANDER NA HARAMIA.

ISKANDER, mfalme wa Wayonani, alitiisha inchi mataifa, falme zote alizopigana nazo, akautawala ulimwengu, akawa mwenyi enzi kuu. Palikuwa na haramia mmoja, mwenyi mtepe, kazi yake kuvizia baharini, kuotea watu, kukamata, kuteka, kuua, ndio kazi yake. Iskander akasikia habari zake, akatumia watu kumkamata; wakamkamata wakamleta. Iskander akamwambia, "Wathubutuje nawe kuvizia baharini na mtepe wako?" Asihofu yule haramia, akajibu, "Wathubutuje na wewe kuivizia inchi pia? Mimi mwenyi mtepe mmoja tu, watu husema, 'Haramia mbaya sana huyu.' Wewe mwenyi majeshi mengi sana, husema, 'Iskander ndiye jemadari na mshindaji mkuu.' Labuda hali yangu ikibadilika, ningetulia. Bahati yako heri sana, bassi umekuwa mbaya zayidi." Iskander akamwambia, "Vema. Nitakubadilishia bahati yako, usipate nafasi kuinenea bahati yangu." Akampasha utajiri mwingu. Haramia akatubu akawa shekhi mkubwa na mwenyi haki.

---

### 19. ISKANDER NA NYOKA.

ISKANDER, mfalme wa Wayonani, alimiliki inchi zote. Akafanya jeshi, akazunguka mji mmoja, aki-

taka kuutwaa. Asiweze, kwani mashujaa wengi na asikari waliuawa pale, wasitiwe jeraha yo yote. Aka-waita madiwani na waalimu, akawaambia, "Imeku-waje hiyo? watu hufa, wala jeraha hakuna." Wakamwambia, "Kuna nyoka huko bomani, hatta akimtupia mtu jicho atakuфа. Ndio maana." Aka-wauliza. "Na dawa hapana?" Wakasema, "Iko. Twa kiyoo, kakikaze juu kidogo kati yao asikari na yule nyoka. Nyoka atatazamisha kiyoo, ataona jicho lake yeye, sumu itamrudia mwenyewe, atakuфа." Akafanya hivyo, asikari wakapona, wakautwaa mji.

---

## 20. MFALME MKARIMU.

MFALME mmoja akapiga mbiu, "Mtu akiniomba atapata lo lote atakalo." Wakaja wengi, kwanza wakubwa na matajiri wakataka falme, mashamba, mali; wakapata. Baadaye maskini na wajinga, wakataka vilevile. Mfalme akawaambia, "Mbona mmechelewa? Nimeishiwa mali." Wakafathaika mno. Hatta mfalme akawasikitikia, akasema, "Bado kitu kimoja ninacho. Mali zimekwisha, enzi tu imebaki. Hapana aliyetaka. Twaeni, kawatawaleni wale wakubwa." Wakubwa wakasikia habari, nao wakafathaika ajabu mno, wakamwambia mfalme, "Tutawaliwe na hao? Bora kufa." Akawaambia, "Mmepata iliyo haki. Bassi sikelizeni shauri yangu. Toeni sadaka kawatendeeni hao mema, ndio mtawatuliza sana ua kutia urathi. Hawatapenda kusumbukia enzi na kutawala, itanirudia mimi. Nanyi mmetoka utumwani." Wakafanya. Wote wakakaa raha.

## 21. RAFIKI.

**PALIONDOKA** mfalme, akazaa mtoto wa pekee, aka-mpenda sana. Mtoto akakua akasafiri akakaa miaka saba akarudi, akamwambia baba, "Nimepata rafiki watatu. Mmoja nampenda kupita nafsi yangu ; wa pili nampenda sawasawa ; wa tatu, si mno, kidogo tu." Babaye akasema, "Bassi tuwajaribie. Chinja nguruwe, kamtie fukoni, nenda usiku kwake umpendaye sana sana, kamwambie, "Ee Rafiki, nimeua mtu kwa bahati. Nikikamatwa, sina buddi kufa. Nakusihii, uniponye."

Akaenda ; rafiki yule akajibu, "Ukiua mtu, uta-sulibiwa ; ndiyo haki. Lakini kwa urafiki nakutolea pima moja la nguo ya kuzikiwa. Bassi."

Kijana akaona uchungu, akamwendea wa pili, aka-mwambia vile vile. Akajibu, "Kukuponya, ndiye hatari kwangu mimi. Lakini kwa urafiki ntakuja kukusindikiza hatta msalabani."

Kijana asikubali, akaenda kwa yule wa tatu, aka-mwambia vile vile. Akajibu, "Sisi wawili mmoja tu. Ukihukumiwa kufa, nami nife badala yako ; kama sivyo, nife pale, pamoja nawe." Akamtambua huyo ndiye rafiki.

---

## 22. NA TENA ?

**PALIKUWA** na kijana, ametiwa chuoni, amesoma sana, amehitimu ilmu pia. Akaondoka akienda mjini kutafata kazi, akakuta njiani mtu mzee akasema naye. Yule mzee akamwambia, "Waenda mjini ?" Akanena, "Nakwenda." Akamwambia, "Kwa nini ?" Akajibu, "Kutafuta kazi." Akamwambia, "Na tena ?"

“Tena naona nitapata mshaara mkubwa.” “Na tena ?” “Tena nitaweka akiba, nitafanya mali nyingi.” “Na tena ?” “Tena nitakuwa tajiri na mngwana.” “Na tena ?” “Tena nitaoa, nitazaa watoto, nitakuwa na jamaa bora.” “Na tena ?” “Tena watu wote wataniheshimu, labuda nitakuwa mfalme.” “Na tena ?” “Tena nitakaa raha na mustarehe, ntakuwa mzee.” “Na tena ?” “Tena, tena naona ntakufa.” “Na tena ?” “Na tena, na tena, na tena, Ah !” Akanyamaza yule kijana akaenda zake akafikiri mambo ya Muungu rohoni mwake.

---

### 23. JUMBE KATIKA BARRA.

PALIKUWA na jumbe katika barra, hodari na mwe-nyi mali, na Mzungu akikaa pale pale, naye Mmasihiya mpelekwa. Bassi yule jumbe ameonekana amefanya thambi, hatta akayakinia kwa nafusi yake kama amekosa sana kweli kweli. Akaingia mashaka akaenda kwa yule Mmasihiya akamtolea mshipi wake, na ngozi ndizo mateka yake ya ktwindwa, apate kupona katika hofu zake. Mmasihiya aka-mwambia, “Hakuna, Muungu hakubali sadaka kama hii.” Jumbe akaenda zake, marra akarejea, akamtolea bunduki nzuri. Akajibiwa vile vile, “Muungu hazikubali sadaka hizo.” Akaenda zake tena, asikae sana. Hana buddi kurudi marra ya tatu, akamtolea na kibaanda chake, mkewe, mtoto, killa alicho nacho, kwa amani na samehe. Akaambiwa, “Hakuna, Muungu harathi sadaka kama hizo.” Jumbe yule akalemewa na shangao na huzuni kwa kitambo, hatima akamwinulia Mmasihiya macho yenyi machozi, akamlilia kwa moyo, “Ee Bwana tazama, kanitwae mimi hapa maskini tena.”

## 24. DAWA YA UGOMVI.

PALIKUWA na mwanamke amegombana na mumees amepigwa naye. Mtu akamjia akamwambia, "Usipopenda pigwa, ntakupa dawa ya ugomvi." Akamwambia, "Haya." Akampa dawa, ndio maji matupu, katika chupa, akanena, "Tia kinwani tu, usiyameze, mumeo hatakukaripia. Naye marra ya kumwona mumee na uchungu akaitia kinwani mwake. Hasira yake ikapoa upesi, akamwacha amani. Baadaye mwanamke akamwuliza mtu yule aliyempa maji, "Dawa yako imefaa sana ajabu. Inapatikana wapi?" Akajibu, "Kisimani mo mote."

## 25. KUNGU.

PALIKUWA na nokoa, aliyeleta mjini kungu tano nzuri kuliko awezazo kupata. Ndio awali hii, watoto wake kuyaona matunda kama haya, nao wakachekelea sana kwa matunda yale kuwa mekundu na laini kama machavu yao. Na babao aliwapa watoto wa'gne moja moja, na ya tano mama yao.

Usiku wakati wa kulala baba yule alisema, "Niambieni mmetakaje matunda yale mazuri." Mtoto aliye mkubwa wao akamwambia, "Sana, baba, ina maji tele na tena tamu. Nimeweka kokwa yake nitaipanda nioteshe mti." "Heri sana," alisema baba, "Una akili na busara." Kitinda mimba aka-jibu, "Yangu naliila pale pale, nikatupia mbali kokwa. Mamangu akanipa nussu. Ah! tamu sana, imeyeyuka kinwani mwangu pia." "Bassi," alisema baba, "hukufanya busara, lakini kwa utoto wako, kama tuwaonavyo watoto." Yule wa pili

akaanza, "Nikaiokota kokwa ile aliyoitupa ndugu yangu, nikaivunja. Ulikuwa mbegu ndani, utamu wake kama njugu, lakini nikauza kungu yangu nikaapata pesa nyingi, hatta nikienda mjini nitaweza kununua sita kwa mali yake." Baba akatikisa kitwa akasema, "Ndio busara halisi, lakini si ya utoto hiyo busara. Hasha usikue na choyo kama bakhili." Akamwuliza mtoto wa tatu, "Na wewe je?" Alijibu, "Naliichukua kungu yangu kwa yule kijana maskini, mtoto wa jirani yetu, hawezo, ana homa. Naye akakataa, bassi nikaiweka kitandani pake nikatoka." "Je, enyi watoto?" akasema baba yao, "Nani kati yenu aliyetumia vema kungu yake?" Wakasema wote watatu, "Huyu ndugu yetu." Yule akanyamaza kimya. Mamaye akambusu sana na machozi machoni pake.

---

## 26. SULTANI HAKKUM.

PALIKUWA na Sultani, jina lake Hakkum, akatwaa kwa nguvu shamba dogo la mjaani mmoja maskini, sababu alitaka kuiongeza bustani yake. Na yule maskini akaenda zake kwa kathi, apate kuhukumiwa haki yake. Naye kathi akamtandika punda yake, akaweka kapo kubwa juu yake, akapanda akaenda zake kwa Sultani, na ye ye aliakuwa anatembea katika shamba lile ndilo bustani yake mpya. Akamwambia, "Nataka ruksa nijaze kapo hili udongo wa shamba hili." Sultani akampa ruksa, tena yule kathi akajaza kapo udongo, akamtaka Sultani amsayidie kuliweka juu ya punda. Likawa zito sana. Akasema Sultani, "Lanishinda, haiwezekani kabisa." Kathi akamwambia, "Tazama, kapo hilo laweka kipande kidogo tu cha shamba, ulilomtwalia mjaani

yule maskini. Bassi utawezaje kuchukua begani shamba lote pia, ndio mzigo utakaowekwa na Mwamuzi Mkuu siku ya mwisho?" Sultani akasangaa, akatubu, akamrudishia mjaani urithi wake.

---

### 27. SULTANI ORUNGZEBI.

Uko katika Hindi mji mdogo, unaokwitwa Tolapur, maana yake pa kupima. Umehadithiwa hivi, ya kwamba palikuwa na Sultani, jina lake Orungzebi, akawa anapita katika inchi yake na asikari wake, akafika mjini mle, napo na mto na mashua ya kuvukisha watu. Akangoja pale penyi kivuko, wakivuka asikari wake, akaongea na mwenyi mashua. Mtu yule akawa na sifa nyingi kwa kuwa mwerevu sana. Akamwambia Sultani, "Hatta hapana nyama yo yote nisiyoweza kuipima uzito wake barabba." Sultani akasema, "Bassi unipimie tembo huyo niliompanda." Akamwambia, "Kwanza mweke katika mashua yangu." Wakamweka. Mashua ikazama sana kwa uzito wake, mtu yule akapiga mstari katika mbavu za mashua sawa sawa na maji yalipofika juu. Wakashusha tembo pwani, akapakia mawe mengi makubwa, hatta mashua ikazama tena mpaka mstari ule ule. Tena akayapima mawe yale moja moja, akahesabu jumla la uzito wao, akamwambia Sultani, "Hiyo ndiyo apatayo tembo wako kwa uzito wake." Sultani yule akapendezewa sana na werevu wake akampa mji ule Tolapur.

---

### 28. SULTANI MAHMOUD.

PALIKUWA na Sultani mmoja wa Ajjemi, jina lake Mahmoud. Akafanya vita nyingi akaoneea rayia

zake, hatta inchi ya Ajjemi imekuwa kama jangwa, haina miji illa haba tu, ukiwa pote na maanguko matupu, na watu wachache.

Na waziri wake akajisanya anasikia lugha ya ndege, hatta ndege yo yote akilia, yule waziri hujua kufasiri maneno yake. Hatta siku moja jioni anatembea na Sultani, wakaona bundi wawili wametua mtini penyi kuta zilizovunjika. Sultani akamwambia waziri, "Nataka jua wanazumgumza nini wale." Waziri akakaribia mtini, akawasikiliza bundi, aka-rudi, akasema. "Nimewasikia kidogo, lakini kufasiri, Ah! hatta sithubutu mimi." Sultani hakuwa rathi, akamwamuru ampashe habari. Waziri aka-mwambia, "Bundi mmoja ana mtoto mume, naye wa pili ana mtoto ndiye mke, wanafanya shauri la kuwaozana. Nikamsikia yule wa kwanza mwenyi mtoto mume akinena, "Bassi, rafiki yangu, nakubali mimi, lakini nataka umpe binti wako miji hamsini iliyostraribika." Yule mwenzake akajibu, "Inshallah! Hatta nampa hamsi mia, ukipenda mwenyewe. Amilikipo Sultani Mahmoud, miji iliyostraribika tele mno ajabu." Maneno haya yakamwingiza uchungu Sultani katika moyo wake, akaitengeneza miji ali-yoiharibu, akawatendea watu wake vizuri.

## 29. WATOTO NA MISALABA.

**PALIKUWA** na watoto sita, wametiwa chuongi, waka-kaa wote sita katika nyumba moja nzuri ya mawe, na yenyi shamba zuri. Na amri ya nyumba ndiyo hii, killa mtoto mwenyi kukaa huno apewe msalaba wa mti auchukue, na kwa ginsi alivyochochukua msalaba wake ao vizuri ao vibaya, ndivyo mambo yata-kavyompata baadaye ao mabaya ao mema.

Ikaja siku, watoto wote wakakusanya katika chumba ndani, namo ile misalaba imewekwa tayari, mingine mikubwa na mizito, mingine ya kadiri tu, mingine midogo na mepesi. Mwalikuwamo tena na malaika sita, killa mtoto na malaika yake, kazi yake kumtazamisha mtoto na kufuatana naye katika masha yake.

Bassi mtoto wa kwanza akaondoka akanyosha mkono aupokee msalaba, na malaika akautwaa msalaba ulio kwake yeye akampa; nao ule msalaba si mkubwa sana wala mzito, illa kidogo tu, yule mtoto asiukubali, akasema, "Mimi siuchukui hatta msalaba. Nataka mimi kufanya kama nipendavyo siku-zote, ao kucheza, ao kutembea, ao kukaa, vile vile. Sitaki msalaba wo wote." Malaika akamwambia, "Lakini hujui usipochukua msalaba sasa, hupati taji baadaye?" Mtoto akamwambia, "Bassi nia-khirishe kuchukua kule, nifanye nipendavyo kwa muda niwezavyo. Halafu yake labuda sina buddi. Lakini bado kwanza, na saşa msalaba siutaki kabisa mimi." Akatoka yule mtoto nyumbani, akaenda cheza, asifikiri ulimwengu.

Akaondoka mtoto wa pili, malaika yake akamtolea msalaba wake, akautwaa. Malaika akamwambia, "Imekupasa kuuchukua siku zote mwenyewe, haifai kuuweka chini." Yule mtoto akaenda zake akau-chukua vema kwanza, hatta na furaha ya mzigo wake. Halafu yake amechoka, abadilibadili mzigo, kwanza kwa bega hili, tena kwa bega hili, asema, "Mzito sana nao, unanilemea, lakini kutua ah! sithubutu. Nifanyeje? Niutupie mbali? Lakini kurudiwa je? Nataka shauri, nisisumbuke sana vile nao." Akafikiri hatta akaenda kutafuta kamba akapata akaifungia msalaba, aukokotakokota chini nyuma yake. Bassi kuchukua gani kule?

Tena mtoto mwagine akaja kwa msalaba wake,

malaika akamtolea mmoja vile vile. Yule mtoto **akautwaa** akautazamisha, akauna uzito wake, tena akasema, "Naona mimi nataka kuchagua mmoja mwenyewe." Malaika akamjibu, "Lakini huo ndio ulioamriwa na Bwana wako, huo huo sio mwingineo, naye Bwana ndiye ajuaye upi wa kukufaa." Mtoto akamwambia, "Huo sio nichaguao mimi lakini." **Akainama chini** akachagua mmoja uliompendeza nafsi yake akatoka nao ule.

Hatta mtoto mwingine akakaribia, akapewa msalaba, akapokea, lakini kwa uso mzito kama anaona uchungu. Akaenda zake nje, akaenda kwenyi sermala, akatafutatafuta katika vyombo vyake sermala, hatta akapata msumeno, tena kazi yake alikata msalaba ndio kuurakhisisha mzigo wake. Bassi msalaba ume-kuwa sio ule ule uliopewa na Bwana.

**Akaondoka** na mwingine naye wa kicheko na furaha; akataka habari akasema, "Je, misalaba wangu upi? Nataka mkubwa na mzito mimi, nataka kuu-chukua vema sana, alivyouchukua msalaba wake Bwana mwenyewe. Sipendi mdogo." **Akajibu malaika**, "Killa mtu msalaba wake. Ukiwa mzito, anauweza; ukiwa mwepesi, anauweza. Bassi. Huu ndio wako." Nao msalaba si mkubwa sana, na yule mtoto akaonekana ana huzuni, akaenda zake. Marra akawa hauchukui begani mwake vizuri na kwa unenyekevu, kama Bwana, ameinua juu na mikono yake juu, ndio kujiona mwenyewe, illi watu wastaa-jabu, wakaseme, "Tazama, hodari mtoto yule; haoni mzigo kabisa."

Bassi akaja mtoto bado mmoja tena, ndiye mwisho. Yule mtoto akaona hofu akikaribia palipo misalaba, akapewa mmoja na malaika, akaambiwa, "Ndio wako wee." Akasema, "Mimi hapa mdogo, sina nguvu mimi, siuweza msalaba huo, nitalemewa sana." Malaika akamwambia, "Bwana aliyekuletea ndiye ajuaye

nguvu zako. Kuamriwa naye ndiyo kuwezeshwa naye." Yule mtoto akasema, "Bassi nitajaribia. Nisipopata msaada wake, siuzezi. Lakini nitajaribu." Wakatoka wote na watoto na malaika pia. Na wale malaika waliowatunza watoto, nyuso zao nzito, illa wa malaika yule wa mwisho tu, naye uso wake wa kicheko na furaha.

---

### 30. WATOTO NA MAUA.

Na hizi pia habari ya watoto wale wale waliopewa misalaba na malaika. Siku moja waliletewa killa mtu ua moja, lililotoka mbali huko Ulaya, nalo zuri sana kwa kutazama lenyi rangi nyeupe na safi kabisa, na kama thahabu katikati, na shina la nguvu na majani mengi, lanukia vizuri ajabu. Na maua yale yote sawa sawa na namna moja. Wakaambiwa, "Haya maua hamna buddi kuyatunza sana. Yametoka mbali huko Ulaya, ndipo kwao, hayawezi kuota vema na kusitawi, msipoyanywesha maji marra mbili killa siku, assubuhi na jioni, na kukinga mvua nyingi na kuangalia lisipatikane na jua kali, wala baridi kali, wala tufanu, wala madudu, wala funza lisitafunwe chini. Thaifu kweli kweli, lakini ukiliangalia vema, hakosi litasitawi. Hatta Bwana atakuja mwenyewe halafu yake kutazamisha." Watoto wakafurahi, wakatwaa killa mtu ua lake, wakatafuta pema pa kupandia, wakapanda maua katika mashamba yao, wakayatunza vizuri wagine siku nyingi.

Hatta siku moja akaja Bwana kutazama mashamba yao watoto, akataka habari za maua yale. Akakuta la kwanza ncha yake inainama chini inafifia, na udongo wake umekauka mgumu kama chuma. Akamwambia mwenyi shamba, "Ewe, mbona umesahau kumnywesha maji hilo?" Yule mtoto akaona haya akasema, "Mimi

hana kunywesha maji nalinywesha siku mbili tatu. Bassi nikataka kunywesha killa siku, siku kwa siku. Bassi nami pana siku kazi yangu kwenda kuchenza, pana siku nasoma, hivi tu. Bassi sasa labuda ua limekwisha kufa." Bwana akamwambia, "Bado kufa nawe. Usilegee tu, ulitunze marra moja na siku zote. Kutanza kidogo, tena tuacha kidogo, haifai. Shika kazi vema, mwanangu."

Na ua la pili hali yake mbaya sana. Limetupwa chini, kama limekanyagwa, na karibu kukatika kabisa. Kitwa chake kizuri na cheupe kimetiwa tope na taka, hakitambulikani kuwa ua lile lile kwa ginsi lilivyo-geuka. Bwana akamwambia mtoto mwenyi ua, "Ee mwanangu, na hilo limekuwaje?" Yule mtoto aka-anza kulia, "Ee Bwana, nalionna kuzuri kulipatia jua kidogo, na hewa nzuri huko nje. Marra moja ikaja tufanu, ikalitupa pale chini. Nami naona hapana kulichupukisha tena." Bwana akamwambia, "Haya bassi, tujaribie. Lete kijiti upesi, kalifungie. Maua haya hayafi, yana nguvu tele ndani. Na hilo likite-gemea kijiti mti, hakosi litachipuka. Ulitunze vema tu."

Akafika palipo na jingine, limegeuka vibaya kwa umbo lake, limefunikiwa na madudu madogo madogo meusi, wanalitafuna na kufyonza maji yake, ndio chakula chao. Na mwenyewe hapo, amekwenda, cheza, sijui. Bwana akafikiri, "Ah! shidda kuliponya na lile, laponyekana lakini."

Na karibu yake akakuta na jingine, limepatikana na baridi kali usiku, na karibu kufa. Basi likasalia na moja tena, nalo hali yake si njema, lilikuwa linakauka sana, linafilia mbali, lakini mwenyewe yupo amelitunza sana sana, wala haliponi. Akasema, "Hatta mimi sitambui limepatani ua langu, linakufa tu, na mimi sina ya kuliponya. Bassi nifanyeje?" Yule Bwana akatazamisha sana lile ua; kiisha

akamwambia mtoto, "Kweli, mwanangu, limekushinda. Basi naona heri ulichukue kwa msimamizi wa shamba. Yeye atakupa shauri la kulisitawisha tena, kwa maana anajua siri nyingi. Nawe usikose kumwelezea mambo yote yaliyolipata ua lako." Akalichukua.

Maua mangineo yalikuwa yanositawi sana, bwana akafurahiwa nayo.

---

### 31. MTOTO NA PAKA.

ZAMANI za Eduadi wa tatu, mfalme wa Ingereza, palikuwa na mtoto jina lake Dick Whittington, akaaka mashambani. Hatta akasiwa na baba na mama, na mali hana wala kazi haiwezi, kwani mtoto tu, bassi hali yake mbaya sana ya kimasikini. Hatta kizee mmoja maskini akimhurumia akamkaribisha kwake, akakaa naye. Yule kizee akamwongoza vema kwa shauri nzuri, mtoto akawa mtendaji kazi sana na mwema akapendeleva na ujirani wote. Akakua akapata nguvu akawa umri wake kamia miaka arobatasara, yule kizee akapatikana na farathi akafa, kijana akasalia peke yake, hana buddi kutafuta kazi apate kuchuma. Na huyo kijana mwenyi akili njema, killa akutapo mtu mwenyi maarifa na kujua mambo ya kufaa, humwulizauliza habari hatta kuyajua. Akasischia habari za London, ulivyo ajabu sana mji ule, hatta mwenyi njia zake zote za thahabu, na wakaamo wangwana watupu, waume kwa wake, ndivyo mji ulivyo hadithiwa na watu wa kimashamba. Hatta kijana akataka sana kwenda London na kuutazama kwa macho, akasema moyoni mwake, "Nikijaliwa kufika kule kwenyi mali na ukuu, hakosi ntasitawi kuliko hapa shamba."

Ilipokuwa assubuhi, akaondoka akashika njia peke yake, hana kitu illa nguo, na mkeba, na themuni moja

tu bassi ; akaenda kwa furaha yake na kutumaini ; akaenda akaenda hatta akachoka, akakaa kitako. Likaja gari la frasi limepakiwa vitu vingi linakwenda London, mwenyi gari akamwona kijana apumzika akamwuza habari. Kijana akampasha habari zake zote, akamwambia mwenyi gari, "Ee Bwana, nimechoka sana, na mbali kufika London. Unichukue kidogo katika gari, mpaka nipate nguvu, tena nitakwenda kwa miguu." Akakubali, kijana akapanda juu ya gari akachukuliwa, marra akashuka akaenda kwa miguu, marra hupanda tena, marra kutembea, hatta akauwasilia mji mkuu.

Moyo wake ukafurahi mno, kwani amekwisha fika London, halafu akaona uchungu, kwani kwanza auona mji si mzuri wala mkubwa, kwa maana watu wa shamba wameongeza sana habari zake. Akaagana naye mwenyi gari, na pesa hana illa pesa mbili tatu, akapotea huko na huko mjini akitafuta njia za thahabu, na majumba ya matajiri mchana kutwa, asiyapate. Akashikwa na njaa, hawezi kwenda, akaenda kwa baraza ya nyumba akajinyosha akilia hatta aka-sinzia. Akalala pale barazani hatta jua likachomoza assubuhili ; akaamka akaondoka akapotea vilevile mitaani, akitafuta mtu wa kumsikiliza habari zake na kumkaribisha na kumpa kazi.

Hatta akakuta jumba kubwa akasema, "Nibishe hodi hapa. Sijui itakuwaje, nikaribishwe, ao nitupwe. Haithuru, ntabisha tu." Akabisha mlango, "Hodi !" Mjakazi mmoja akaitika, "Hodi !" naye mjakazi mpishi, mkali na mkorofsi, akamwona mtoto maskini wa kimashamba amesimama mlangoni, aka-mkemea sana, "Wataka nini nawe ? Mbona kuni-uthi burre ? Ondoka marra moja." Akimfukuza. Kwa bahati akaja tajiri, mwenyeji nyumba, jina lake Fitzwarren, akamwambia, "Ee mtoto, njoo. Nipe kisa chako. Habari gani ? Umetokapi, waendapi ?"

Mtoto akafurahi, akasumulia habari zote, akampendeza tajiri sana, hatta akamkaribisha nyumbani akamtunza, akasema, "Kae hapa, mpaka upate uchumi."

Na huyu tajiri ana binti, jina lake Alice (Alis), naye umri wake sawasawa na kijana; akasikiliza maneno ya baba akamsikitikia mtoto, kwani maskini hana baba, hana kwake, hatambulikani; akamtendea mema mengi. Lakini yule mjakazi humwonea sana, amtuma kya kazi huko na kazi huko, humkaripia, humtukana, humchokoza, akamlaza kipenuni kwenyi panya na wadudu, napo uthia tu kulala pale usiku. Raha hapana. Mtoto asithubutu kumchongea kwa bwana, kwani aogopa, akavumilia tu; akafanya shauri moyoni mwake kununua paka wa kufukuza panya, apate raha kidogo.

Siku moja anafagia barazani nje, akaona kizee maskini akipita akichukua paka, akamwambia, "Paka je? wauza?" Akaaitika, "Nauza." Akamwambia, "Pesa ngapi?" Akasema, "Pesa kumi." Akasema, "Ah! siwezi, mimi mtoto masikini tu, sina baba, sina mama, sina fetha. Kazi yangu nalala penyi panya wengi, wanisumbua sana. Nataka raha kidogo. Ndio nanunua paka, awafukuze panya, nikapate usingizi kidogo mimi maskini." Kizee akamhurumia akasema, "Haya, nunua." Akasema, "Sina illa pesa mbili tu." Akasema, "Lete." Akachukua paka, akamweka kipenuni, akamlisha killa siku kwa chakula chake yeye. Hatta akitumwa kwenda mahali, kuchukua vitu, barua, hivi, huchukua na paka.

Wakapendana sana yeye na paka wake. Paka akatenda kazi sana, akawafukuza panya wote pia, wala si mfukuza panya tu yule paka, hodari tena kufanya maajabu mengi mtoto aliyomfunza. Siku moja anacheza na paka binti tajiri akaja akawaona wanavyocheza yeye na paka, naye akampenda sana paka yule

na mtoto pia. Na mtoto akasumbuka sana na mpishi yule katika kazi alizotumwa, akapigwa marra kwa marra, akatendewa mabaya mengi. Bassi huyo Alice humfariji, humfanyia urafiki, hatta kijana alimwona Alice kuwa kama malaika wake. Halafu Alice aka-msihi babaye, kijana atiwe chuoni na kufundishwa kuandika, (kwani ajua kusoma vizuri,) na kupata marifa mengi. Akakubali, kijana akaendelea sana kwa kuandika na kujuua maarifa.

Siku zikapita, hatta siku moja tajiri yuko pwani anapakia mali katika marikebu yake kwenda mbali kufanya biashara. Tajiri akawaita watu wote walioko nyumbani, wangwana kwa watumwa, akawatolea shauri wampe killa mtu amana kidogo, awanunulie bithaa. Wakampa killa mtu kwa kadiri yake, illa kijana tu, naye hana kitu wala pesa ; kijana akalia sana kwa uchungu wa moyo wake. Binti tajiri aka-mwita kwa faragha akamwambia "Kopesha paka." Akamtoa paka, rafiki aliyempenda sana, akampeleka ndani ya marikebu akamwekea nakhotha mwenyewe. Tena binti tajiri akamwita nakhotha akampasha habari zote za paka alivyo paka mwenyi akili na hodari na mtendaji kazi sana, apate fayida kubwa nao.

Bassi kijana akatwaliwa paka, akaona huzuni ; na mpishi kazi yake kumzidishia huzuni kwa kumlemea sana, na kumchokoza, na kumchekacheke, "Amana yako bora nayo. Wataka fayida ? Hatta pesa moja hupati." Tena binti tajiri alikwenda kukaa shamba ; bassi kijana maskini hana mtu wa kumfariji, hawezi kukaa kule nyumbani peke yake na kusumbuka killa siku. Hatta akakata tamaa, akasema, "Ntatoroka."

Akaondoka alfajiri asionekane na mtu, akatoka njini kwenda kupotea. Akachoka akakaa kitako juu ya jiwe kwa huzuni yake. Na jiwe lile lime-kwitwa, "Jiwe la Whittington" hatta leo. Bassi

kukaa kule, halafu akalala, kengele za kanisa katika London zikalia, akazinduka akazisikiliza kengele, akaona kama zikimwambia,

“ Urudi, Whittington,  
Liwali wa London ! ”

Akashangaa kwa kusema hivi kengele ; akafikiri, “ Bassi nipate kuwa liwali wa mji huo mkubwa sana, nisistahimili yote ? Haya, nirudi, hatta ulimwengu ukinisonga, haithuru, nipate kuwa liwali.” Akarudi zake nyumbani, asiangalie mtu kama ametoroka. Akatenda kazi sana apate kumpendeza bwana na binti wake.

Marikebu ya tajiri ikasafiri, ikapatwa na thoruba, ikachukuliwa huko na huko baharini, ikafika pwani katika Afrika, upande wa magharibi, mahali penyi mali nyingi. Watu weusi wakawakaribisha Wazungu. Mfalme aliposikia kama Wazungu wamekuja, alituma majumbe kwenda kumwita nakhotha na wangine, waje kwake kula naye. Karamu kubwa sana ikafanyizwa, mfalme akawakaribisha Wazungu akawatendea mazuri na adabu. Vyakula vikaandikwa mezani vingi na vizuri, wakataka kula wote ; kumbe panya wengi wengi wakatoka vitunduni vyao wakavirukia vyakula karibu kuviisha. Mfalme akasumbuka sana, si kwa sababu panya wakaja, kwani huja siku kwa siku, lakini kuja palepale alipokaribisha wageni, ndio iliyomtia uchungu sana. Hatta nakhotha akatoshea, akamwuza mfalme, “ Je ? Hutaki kuondolewa mbali nyama hao wanaokusumbua ? ” Akasema, “ Nataka mimi. Kama mtu akiweza kuwaondosha pia, ningempasha utajiri mwangi usio na kifani hapa kwetu.” Nakhotha akafurahi, akamwambia, “ Mimi nina mnyama marikebuni mle, awezaye kuua panya hatta elfu.” Akamwaarisu habari nyingi za paka na kazi yake, kwani mfalme mwenyewe alikuwa hajaona paka hatta mmoja. Marra nakhotha akatuma mtu kwenda mari-

kebuni kumleta paka. Paka akatiwa tunduni, wakamchukua kwa mfalme.

Siku ya pili karamu ikafanyika vilevile, panya wakatokea kama kwanza, marra paka awarukia, wangine huua, wangine hufukuza, nussu dakika wote wameisha. Furaha ikawa kubwa sana. Mfalme na wakuu wake wakashangaa kwa mshangao usiokoma. Kwanza wakaogopa kumshika paka mwenyi nguvu hizi, hatta wakamwona mnyama mtulivu sana, wakathubutu kumpapasa kidogo. Wakamsihi sana nakhotha kuwaachia paka kukaa pale, akathani watampa zawadi kubwa sana kwa kitu hicho cha tunu, aka-kubali kumwacha. Mfalme akampenda sana paka, akamwambia nakhotha, "Paka huyu mzuri sana, nataka aishi milele, kwani akipatwa na farathi wale panya watarudi vilevile na zayidi." Nakhotha aka-sema, "Huyu paka ana watoto, amezaa marikebuni mle, nao ntakutolea." Mfalme aauliza habari zote za kijana mwenyeji paka, akasikia alivyosikitika sana siku ile alipoagana na paka. Akamwonea rehemaa kasema, "Siwezi kumtwaa paka, ndio uchungu mwangi kwa mwenyeji. Bassi mrudishie paka. Labuda watoto watatosha kwa kuwafukuza panya." Navyo ndivyo, kwani wale watoto hodari sana, kama mamaao.

Bassi paka akatiwa tunduni, akaenda marikebuni ; mfalme akasikia kama fathili za paka kubwa sana, bassi akampa nakhotha mali nyngi sana ajabu, aka-mwambia, "Chukua hiso kampe kijana mwenyi paka." Bassi nakhotha akatenda shughuli zake zote, akaisha, akaagana nao watu, akatweka, akasafiri kwenda zake Ulaya. Baada ya siku nyngi akawasilia hatta London. Hatta tajiri akafurahiwa sana kutazama marikebu inakuja, kwani amethani imepotea kabisa.

Nakhotha akampasha habari zote za safari, aka-mwambia, "Yule kijana amepata fayida kubwa sana ya paka yake." Tajiri akafurahi na binti yake pia.

Akamwita kijana, akamwambia, "Ulipata taabu kwanza na mateso ukavumilia, ukawa mtendaji na amini, bassi Muungu, amekulipia thawabu kuu."

Wakaenda pwani, wakaona makasha mengi maku-bwa, yashushwa pwani, ndio mali zilizomtoka mfalme wa barra, alizomtolea mwenyeji paka. Kijana akashangaa mno, akatoka machozi, akamsihi bwana wake akisema, "Ee Bwana, utwae wewe, kwani wewe mfathili wangu." Asikubali kutwaa hatta kidogo, akasema, "Mali yako wewe peke yako." Nakhotha akamwambia kijana, "Hatta kitu kimoja tena ninacho, kimetoka kwake mfalme huko barra, akaita baharia," akamwambia, "Lete tundu." Akaleta akafungua, paka akatoka kwa furaha ya kuonana naye kijana. Wakakaa.

Tena yule kijana akawa na mali mengi sana, hakuzipoteza, hapana, alizitumia kwa akili sana. Kwanza akampa killa mtu zawadi, hatta na mpishi yule mkorofii alimpa, naye akaona haya sana. Tena alifanya biashara nyingi sana. Mali zake zikaongezeka mwaka kwa mwaka; yule tajiri akamwongoza katika shughuli, ulimwengu wake, akamtolea masshauri mengi mema, ukamfanikia. Hatta kijana akamposa binti tajiri, kwani alimpenda mno tanguzamani, akawa maskini kwanza, sasa mtu mkubwa, wa kutambulikana. Wakafanya arusi kuu ya siku nyingi. Yule kijana akazidi kuwa mtu mkubwa, akawa mtu wa baraza na diwani, akapata cheo cha heshima na jina kuu. Hatima akawa liwali wa London, ndivyo ilivyotimia sauti ya kengele, zili-kyoimba,

"Urudi, Whittington,  
Liwali wa London!"

Hatta mfalme wa Ingereza akaja kula naye, karamu ikafanyika vizuri vizuri isivyo na kifani, mfalme

akamwambia, "Hapana mfalme aliye na rayia kama wewe." Akaitika, "Hapana na rayia aliye na mfalme kama wewe."

Akatoa sadaka nyingi sana, akawalisha maskini wengi. Akakaa siku nyingi kwa raha mustarehe, mwenyi afya na heshima. Akafariki. Jina lake halisahauliki katika Ingereza, ndio Dick Whittington.

---

### 32. MTOTO NA MBAAZI.

ZAMANI za mfalme Alfredi, mfalme wa Ingereza, palikuwa mjaani, naye maskini, akawa na mtoto mmoja, jina lake Jak. Mamaye akampenda sana hatta kumharibia tabia yake, hamwongoi, hamtumii kazi, killa atakacho humpa. Yule mtoto akawa mvivu, na mjinga, na mpotevu sana.

Wakakaa siku, umasikini wao ukazidi, hatta chakula cho chote hawanacho. Mwanamke akalia, akamwambia mwanawewe, "Ng'ombe wetu hatuna buddi kumwuza, tupate chakula." Mtoto akamsikitikia, akamwona mamaye ana huzuni sana, akamwambia, "Haya, mama yangu, ntachukua ng'ombe, ntakwenda mji wa pili, ntamwuza, ntapiga bei sana, ntapata fayida kubwa." Mamaye akathani, labuda mtoto sasa ametubu katika uvivu wake. Akamwamini akamwacha kuchukua ng'ombe.

Yule mvivu marra alipoondoka, akampanda ng'ombe akashika njia. Akienda, akamkuta mtu mwenyi baazi nzuri zimefutikwa kifuanzi, mtoto akaziona baazi, akasema moyoni, "Nzuri sana hizo, nazitaka." Na yule mtu akitazama ng'ombe, akaona mtoto ni mjinga, atauza rahisi; akamwambia, "Ee mtoto, wataka baazi hizo, bassi lete ng'ombe, utapata." Mtoto akafurahiwa mno, akakubali marra moja.

Akashuka juu ya ng'ombe akampa, akazitwaa bazi, akaenda mbio kumwambia mama, akithani naye atapendezewa sana. Mamaye aliposikia habari, akaingiwa na hasira na uchungu mwingi, akazitupa baazi nje.

Wakalala usiku, wasile kitu. Assubuhi na mapema yule mtoto akaamka, akasituka akiona chumba kimetiwa kivuli na majani ya mti asiouona kabisa. Akatoka mbio nje, akaona zile baazi zimeota usiku, zimekua sana, hatta mabua yamefika mawinguni yasioneokane.

Marra mtoto akataka kupanda juu, na mama aki-kataza, asimwangalie mama. Akapanda, akapanda, akapanda, saa nydingi akapanda, hatta akachoka, akapumzika ; akapanda, e-e-e hatta akafika juu ; kumbe inchi ngeni sana, hamna hatta mji, wala nyumba, wala gugu, wala mti ; mawe tu na ukiwa, ndio tabia yale inchi yenyewe. Akasimama hana shauri.

Marra zimwi akamtokea, akamwuza habari, "Umetokapi ? Ulifikaje hapa ?" Akampasha habari ya mbaazi ulivyokua. Akamwambia, "Wajua habari za baba yako ?" Akamwambia, "Sijasikia mimi. Nikimwuliza mama, hulia tu, sithubutu kumwuliza tena." Zimwi akasema, "Bassi ntakufahamisha habari zote za babayo, kwani nazijua. Illa kwanza toa ahadi ya kuwa utanitii maneno yangu. Mimi zimwi, usipotoa utakufa." Mtoto akaogopa akatoa ahadi, zimwi akamwambia, "Bassi habari za baba yako ndizo hizi. Alikuwa tajiri na mtu mwema sana. Hapana siku, asipofathilia mtu, killa jamaa huita kuja kula nae. Akajulikana sana pote, watu wota wakampenda." Palikuwa na shujaa, naye mbaya sana, akasikia habari njema za babayo, akasema, "Nimwue nikatwae mali zake." Akajigeuza kuwa maskini akaja na mkewe nyumbani akaomba sadaka. Wakakaribishwa vizuri. Hatta usiku yule shujaa

akaondoka akamwua baba yako, akawaua watumwa, akataka kumwua mama yako na wewe pia ukiwa mtoto mchanga. Mama akamwomba sana amwachilie na mtoto. Akamwachilia, akasema, "Usimwambie siku zote mtoto habari ya baba ginsi alivyouawa." Akasema, "Simwambii." Akakimbia. "Shujaa akatwaa mali zote, akateketeza nyumba moto, akakimbia yeye na mkewe. Bassi na mimi nataka kukupatia tena mali hizo, nikaotesha mbaazi kwa kusudi upate kuja inchi hii. Bassi shika njia hii ya mbele moja kwa moja, utafika penyi shujaa. Ukitanya nisemavyo, utafurahiwa. Mwue shujaa, lakini mamayo usimwambie habari, mpaka tuonane sisi kwanza." Wakaagana.

Yule mtoto akashika njia hatta kutwa, akaona jumba limesimama shambani, akabisha mlangoni, akatokea mwanamke mrefu sana, akamwomba chakula na kukaribishwa usiku. Akasema, "Siwezi. Mume wangu shujaa, hula nyama ya waana adamu. Ndio kazi yake. Akirudi atakupata marra moja." Mtoto akaingiwa na hofu, akataka kukaribishwa usiku mmoja tu. Mwanamke akamsikitikia aka-sema, "Vema, ntakuficha ndani." Akaingia, aka-viona vyumba vingi na vizuri, vimepambwa sana, ma nyuma yao kuna mahali pabaya sana penyi giza, na vitundu vingi, na watu vitunduni wamefungwa. Ndio mateka ya shujaa, na akiba ya chakula. Na watu wakilia sana kwa huzuni ya kuliwa, mtoto akathania, "Nimetegwa leo."

Marra mwanamke akampeleka jikoni, akampa chakula tele. Akala, hofu ikamwondokea. Likaja shindo kama radi mlangoni nje, hatto nyumba ikatikisika. Ndio shujaa amekujaa anagonga. Mkewe akamtwaan mtoto akamficha katika chungu, aka-fungua mlango, shujaa akaingia ndani. Akasema, "Nyama bichi inaninukia." Akamwambia, "Ha-

pana, mateka tu wale wale vitunduni." Akaingia jikoni, na mtoto nussu kufa, amelala chunguni atetemeka-tetemeka.

Shujaa akakaa kitako akamwambia mkewe, "Pakuwa chakula." Mwanamke akaenda jikoni akapakuwa chakula; akamwandikia, akampa maji kunawa. Mtoto akapenesha jicho, akashangaa shujaa alivyo-kula chakula chingi mno ajabu. Akaisha akanawa, akaondoka, akasema, "Lete koo la kuku." Akaleta akaweka mezani. Shujaa akamwambia kuku, "Zaa yayi." Akazaa yayi la thahabu, akalitwaa, akasema "Zaa tena," akazaa tena vilevile. Killa ase-mapo "Zaa," kuku huzaa yayi la thahabu. Halafu shujaa akasinzia, palepale akapiga koroma kama mizinga.

Yule mtoto akaona amelala, akatoka chunguni, akamtwa kuku akakimbia, akafika penyi mbaazi akashuka naye upesi upesi akafika kwake. Mamaye akaona furaha sana, kwani alithani amepotea kabisa. Mtoto akamtoa kuku, akasema, "Nimeleta amana yangu. Nalikuwa mvivu kwanza. Sasa unisamehe." Kuku akazaa vile vile, mtoto na mamaye wakapata utajiri. Wakakaa raha siku nyingi.

Hatta mtoto akafahamu ahadi yake ya kuwa atamwua yule shujaa kwa ajili ya babaye. Akamwambia mama, "Napanda mabaazi tena." Akakataza sana, akasema, "Haifai. Yule mwanamke atakutambua, utauawa kwa maana ya kuiba kuku." Akasema, "Haithuru, niende tu." Akavalia vingine, akajitia rangi asitambulikane; akaondoka akapanda mbaazi. Akapanda, akapanda, akapanda, hatta akafika. Ikawa jioni, akamkuta mwanamke yuko vilevile. Akataka kukaribishwa, akakataa, akisema, "Hatta siku moja nalikaribisha mtoto kama wewe, akaiba mali akaenda zake. Mume wangu alighathabika sana hatta sasa. Bassi mimi sithubutu

tena." Mtoto akamsihi sana, akamkaribisha ndau, akamlisha chakula, akamficha kashani. Akaja shujaa akanusanusa akasema, "Nyama bichi yanukia." Mkewe akasema, "La, kunguru tu, wameleta kidogo wameitupa." Yule akingurumanguruma tu, hatta akampakulia chakula chingi cha watu asharini, akala akashiba.

Alipokwisha akasema, "Lete mifuko ya fetha." Mkewe akaleta mifuko miwili ya fetha mikubwa, mmoja mwenyi fetha, mmoja mwenyi thahabu. Shujaa akihesabuhesabu hatta akachoka akasinzia, akapiga koroma kama mawimbi ya bahari ikichafuka sana miambani. Mtoto akasikia, akaponyoka kashani, akanyemelea polepole, akaishika mifuko, akaitweka begani, akaenda zake mbio mbaazini. Akashuka akafika, akamkuta mama hawezi, marra akimwona mtoto akapona. Akampa mifuko. Wakapamba sana nyumba, wakakaa raha siku nyingi, siku ya miaka mitatu.

Kiisha miaka mitatu, yule mtoto akaufikiri mbaazi, hatta akasema moyoni, "Nijaribie tena marra moja. Bassi je? sina buddi. Sijamwua yule ali-yemwua babangu. Haya!"

Bassi akapanda, akaenda palepale penyi shujaa, shidda sana kumshawishi mwanamke, akampa chakula akamficha birikani. Akaja shujaa akalia, "Nyama bichi hiyo," akatafutatafuta, akapapasa pote hatta pale birikani pia, asimwone mtoto yule ndani amefutikwa. Shujaa akakaa chakulani, akala akanywa pombe nyingi akashiba, akamwambia mke-we, "Lete kinubi." Akaleta akakiweka mezani. Shujaa akakiambia kinubi, "Cheza." Marra kikacheza peke yake, na sauti yake tamu mno, kikampendeza shujaa, hatta akacheza naye kwa miguu. Akachoka akasinzia.

Yule mtoto akakitamani sana kile kinubi, aka-

toka birikani upesi akakishika. Marra kile kinubi kikalia peke yake, kikimwita bwana, "Ee Bwana ! Ee Bwana !" Shujaa akaamka, akataka kumkamata mtoto, asiweze, kwani amekunywa pombe nyingi, akilevyalevya, mtoto akaenda mbio sana, akafika kwa mbaazi akataka kushuka. Naye shujaa yuko nyuma anakuja. Mtoto akashuka, akafika chini, akamwita mamaye, "Lete shoka, Mama, letë upesi." Naye shujaa yuko anashuka, hajafika chini bado, lakini karibu. Mtoto akapiga shoka, akaukatakata mbaazi, akauangusha na shujaa pia, akafa palepale. Mamaye mtoto akafurahiwa sana, kwani mbaazi umekatika, zimwi akatokea, akampasha habari zote za shujaa, akamwonya mtoto amheshimu mamaye. Mtoto akatulia sana. Wakakaa raha mustarehe misha pia. Ndio mwisho.